SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI



# SERA YA ELIMU

## MWAKA 2006

**YALIYOMO** **(i)**
**VIFUPISHO** **(iii)**
**DIBAJI** **(v)**
**UTANGULIZI** **(vii)**
**SURA YA KWANZA: USULI** **1**
**SURA YA PILI: DIRA, DHAMIRA, MALENGO NA MIKAKATI** **3**
**SURA YA TATU: MUUNDO WA ELIMU** **5**
2.1 Utangulizi 5
2.2. Muundo wa Elimu 5
2.3 Umri wa kuanza Masomo 6
**SURA YA NNE: UPATIKANAJI WA ELIMU NA KWA USAWA** **8**
3.1 Utangulizi 8
3.2 Elimu ya Maandalizi (ECE) 8
3.3 Elimu ya Msingi 10
3.4 Elimu ya Sekondari 11
3.5 Elimu baada ya Elimu ya lazima 13
3.6 Elimu ya juu 15
3.7 Elimu kwa Wenye Mahitaji Maalumu 17
3.8 Skuli za Binafsi 18
3.9 Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Amali 20
3.10 Elimu isiyo Rasmi na Elimu ya Watu Wazima 21
3.11 Elimu Mbadala 23
**SURA YA TANO: UBORA WA ELIMU** **26**
4.1 Utangulizi 26
4.2 Mitaala 26
4.3 Mitihani 27
4.4 Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia 28
4.5 Maktaba 29
4.6 Maabara za Skuli 31
4.7 Sayansi na Teknolojia 32
4.8 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) 33
4.9 Lugha ya Kufundishia 34
4.10 Uteuzi wa Lugha 35
4.11 Utamaduni 36
3.12 Elimu ya mazoezi ya viungo na Michezo 37
**SURA YA SITA: WALIMU NA KAZI YA UALIMU** **39**
5.1 Utangulizi 39
5.2 Uajiri na Ugavi wa Walimu 39
5.3 Muundo wa Kazi na Malipo 40

5.4 Mafunzo ya Ualimu 41
5.5 Vituo vya Walimu 43
**SURA YA SABA: UONGOZI KATIKA ELIMU 45**
6.1 Utangulizi 45
6.2 Muundo wa Wizara 45
6.3 Mgawanyo wa Madaraka katika Elimu 46
6.4 Ukaguzi 47
6.5 Ufuatiliaji na Tathmini 48
6.6 Utafiti 50
6.7 Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa katika Elimu (EMIS) 51
**SURA YA NANE: CHANGAMOTO 53**
7.1 Utangulizi 53
7.2 Elimu ya Afya ya Uzazi kwa Vijana (ASRH) 53
7.3 Elimu ya VVU na UKIMWI 55
7.4 Elimu ya Mazingira 57
7.5 Jinsia 58
7.6 Matumizi mabaya ya Dawa za Kulevya 60
7.7 Ajira za Watoto 61
7.8 Unyanyasaji wa Watoto 62
7.9 Afya na Usalama Katika Mazingira ya Skuli 63
7.10 Ushauri Nasaha 65
**SURA YA TISA: UGHARAMIAJI WA ELIMU 67**
8.1 Utangulizi 67
8.2 Fedha za Umma 67
8.3 Mfuko wa Elimu 68
8.4 Mchango wa Jamii 69
8.5 Mchango wa Wazazi 70
8.6 Mchango wa Sekta Binafsi 71
8.7 Fedha za Nje 72
8.8 Udhamini kwa Wanafunzi 73
8.9 Matumizi mazuri ya Fedha 74

**BIBLIOGRAFIA 76**

## VIFUPISHO

ASHR - Elimu ya Afya ya Uzazi kwa Vijana
Adolescent Sexual and Reproductive Health
AYA- African Youth Alliance
CBO - Jumuia za Kiraia
Community Based Organization
CEDAW Convention on the Elimination of Discrimination Against Women
CRC Convention on the Rights of the Child
CSEE Mtihani wa Cheti cha Elimu ya Sekondari
Certificate of Secondary Education Examination
DEO Afisa Elimu Wilaya
District Education Officer
GDP - Pato la ndani Kiuchumi
Gross Domestic Product
ECD Makuzi ya Mtoto
Early Childhood Development
ECE - Elimu ya Maandalizi
Early Childhood Education
EFA - Elimu Kwa Wote
Education For All
EMIS - Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa katika Elimu
Education Management Information System
EQUIP - Programu ya kuinua Ubora wa Elimu
Education Quality Improvement Program
FAWE - Jumuiya ya Ustawi na Maendeleo ya Wanawake
Forum for African Women Educationists
HIV/AIDS - Ukosefu wa Kinga Mwilini
Human Immunodeficiency Virus/Acquired Immunodeficiency Syndrome
GER Uandikishaji wa Jumla bila Kuzingatia Umri
Gross Enrolment Ratio
ICT Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
Information, Communication Technology
IEC Elimu, Habari na Mawasiliano
Information, Education, Communication
MDGs Malengo ya Millenia
Millennium Development Goals
MEES Elimu ya Maadili na Mazingira
Moral Ethics and Environmental Studies
MOECS Wizara ya Elimu, Utamaduni na Michezo
` Ministry of Education, Culture and Sports
MOH Wizara ya Afya
Ministry of Health
MTEF Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati
Medium-Term Expenditure Framework
MYEWCD Wizara ya Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto
Ministry of Youth, Employment, Women and Children Development
NECTA Baraza la Mitihani la Taifa la Tanzania
National Examinations Council of Tanzania
NER Uandikishaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Umri
Net Enrolment Ratio

NGOs Taasisi zisizo za Kiserikali
Non-Governmental Organizations
OCGS Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali
Office of the Chief Government Statistician
PER Mpango wa Mapitio ya Matumizi
Public Expenditure Review
REO Afisa Elimu Mkoa
Regional Education Officer
SACMEQ South African Consortium for Monitoring Education Quality
STIs - Maradhi ya Kujamiiyana
Sexually Transmitted Infections
SUZA Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar
The State University of Zanzibar
SWAps Mfumo Shirikishi katika Utekelezaji wa Mipango ya Kisekta
Sector Wide Approaches
TIE Taasisi ya Elimu ya Tanzania
Tanzania Institute of Education
TC Vituo vya walimu
Teachers Centre
TTC Vyuo vya Ualimu
Teacher Training Colleges
UNFPA Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohusiana na Idadi ya Watu
United Nations Population Fund
UNICEF Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani
United Nations Children's Fund
ZATU Chama cha Walimu Zanzibar
Zanzibar Teachers' Union
ZEMAP Mpango Mkuu wa Elimu
Zanzibar Education Master Plan
ZIPA Tume ya Uwekezaji Vitega Uchumi
Zanzibar Investment Promotion Agency
ZPRP Mpango wa Kupunguza Umasikini Zanzibar
Zanzibar Poverty Reduction Plan
ZSSF Mfuko wa Hifadhi ya Jamii

Zanzibar Social Security Fund

## DIBAJI

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa muda wa kipindi cha mwaka mmoja imekuwa ikifanya kazi ya kuandaa Sera Mpya ya Elimu ambayo imeweka dira na muundo mpana kwa ajili ya maendeleo ya elimu ya muda wa kati na muda mrefu. Sera hii inafasiri dira kuu ya serikali ya Zanzibar (2020) iliyoandaliwa mwaka 2002, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar pamoja na maazimio ya kimataifa kuhusu elimu, kama vile Azimio la Elimu Kwa Wote ifikapo mwaka 2015 na Malengo ya Maendeleo ya Millenia.

Sera hii inachukua nafasi ya Sera ya Elimu ya Zanzibar ya mwaka 1991 ambayo ilifanyiwa mapitio mwaka 1995 na baadaye kutekelezwa kwa vitendo kwenye Mpango Mkuu wa Utekelezaji na Maendeleo ya Elimu wa Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 1996 mpaka 2006. Ingawa kwa upande mmoja sera na utekelezaji wa mikakati ni mambo ambayo yamepata mafanikio mengi, kwa upande mwengine yameibua changamoto mbali mbali zinazopelekea ulazima wa kufanyika mabadiliko.

Uandaaji wa Sera mpya ya Elimu ulikuwa ni matokeo ya vikao vya wadau mbali mbali kama vile vyombo vya Serikali, Sekta za Watu Binafsi, Taasisi Zisizo za Kiserikali, Jumuia za Kiraia na Washirika wa Maendeleo. Wadau hao waliweza kushiriki katika mijadala/midahalo na kuibua masuala mbali mbali yanayoikabili sekta ya elimu. Serikali imeyazingatia kwa udhati kabisa mawazo/maoni yote ambayo yalitokana na vikao vya ngazi mbalimbali.

Pongezi zetu za dhati ziwaendee wale wote ambao walikubali kukutana na Kikundi Kazi na kutoa mawazo yao. Ingawa, haikuwezekana kuweka kwenye sera hii mawazo yote yaliyotolewa na kila mtu, ni matumaini yetu kuwa sera imeyazingatia maoni yaliyotolewa na wadau mbali mbali.

Wizara inapenda kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyengine katika kufanikisha uandaaji wa Sera hii, hususan wajumbe wote wa Kikundi Kazi kilichoteuliwa kuandaa Sera ya Eimu Zanzibar na kufanya juhudi kubwa ya kukusanya mawazo na maoni na hatimaye kuweza kuyaunganisha pamoja na kuandika sera iliyokamilika.

Uandaaji wa sera hii usingeweza kukamilika bila ya kupatikana kwa msaada wa kifedha kutoka kwa Serikali ya Sweden kupitia shirika lake la Maendeleo la Sida. Wizara ya Elimu inautambua na kuuthamini sana msaada huu wa Sida uliotolewa na kufanikisha mchakato wote wa uandaaji wa sera hii.

Ni wazi kuwa Serikali Ya Zanzibar imekuwa ikitoa kipaumbele cha mwanzo kwenye masuala ya elimu na ndio maana mheshimiwa Rais amedhamiria ipasavyo kuhakikisha kuwa maendeleo ya elimu yanapatikana kulingana na matakwa/mahitaji ya wananchi, jamii na ulimwengu kwa ujumla. Mimi kwa nafasi yangu kama kiongozi mwenye dhamana ya kusimamia masuala ya elimu, naahidi kuwa nitaendelea kuwajibika ipasavyo na kutoa msukumo ufaao katika kuhakikisha kuwa malengo yote tuliyojiwekea kwenye Sera Ya Elimu yanatekelezwa na kutimizwa kwa ufanisi mkubwa na wa kujivunia.

Ni matumaini yangu kuwa umma kwa ujumla wake utaunga mkono mabadiliko haya ya sera na kutoa mchango wake ipasavyo katika kuifanya sera hii kuwa chombo muhimu cha kuimarisha elimu. Ni ukweli usio na shaka kuwa mafanikio yake yatahitaji sana ushiriki wa wananchi na kujitolea.

Haroun Ali Suleiman

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

Zanzibar

Februari 2006

# UTANGULIZI

## MUKTADHA

Zanzibar iliungana na Tanganyika mwaka 1964 na kufanya Jamhuri Ya Muungano wa Tanzania. Serikali ya Muungano inasimamia masuala ya ulinzi, mambo ya nje, hazina na mambo ya fedha, ambapo Zanzibar ina mamlaka yake ya kuandaa sera na kusimamia masuala ya mapato na matumizi. Chini ya Sheria ya Muungano ya mwaka 1964 Zanzibar ina mihimili yake mitatu ya mamlaka ambayo ni Serikali (Raisi) na vyombo vya uendeshaji wa nchi, chombo chake cha kutunga sheria ( Baraza la Wawakilishi) na Mahakama ( Mwanasheria Mkuu na Jaji Mkuu). Kwa hivyo, Zanzibar ina uwezo na mamlaka ya kuendesha na kusimamia mambo yake ya ndani yakiwa ni pamoja na utoaji na ugharimiaji wa elimu kwa umma.

Kwa mujibu wa Sensa ya Idadi ya Watu na Makaazi ya mwaka 2002, Zanzibar ilikuwa na jumla ya idadi ya watu 981,754, asilimia 51% walikuwa wanawake, 57% walikuwa watu wa vijijini, na ukuaji wa watu ulikuwa asilimia 3 kwa mwaka. Asilimia 54 ya idadi ya watu wote ni watu wenye umri kati ya miaka 15-55 ambao ndio wenye uwezo wa kufanya kazi.

Serikali imechukua juhudi mbali mbali za kufanya mabadiliko ya kimuundo na kisera yenye lengo la kukuza hali za uchumi wa uhakika na mazingira endelevu ya kiuchumi. Ufikiwaji wa malengo haya kunaimarisha kiwango cha juu cha ukuaji wa uchumi, kushusha mfumuko wa bei na kupunguza gharama za utoaji wa huduma mbali mbali.

Serikali ilifanya mabadiliko hayo, kufuatia mapendekezo yaliyotolewa na Taasisi ya Breton Wood, ili kuisadia serikali kujaribu kuweka uwiano wa ndani na nje. Wastani wa kiwango hasi cha ukuaji wa Pato la Ndani la Kiuchumi cha asilimia 5.2 mwaka 1980-1990, kilipata mageuzi chanya na kuwa cha asilimia 3 mwaka 2003. Hata hivyo, kiwango cha ukuaji kimekuwa cha kusuasua/kikibadilika badilika.

Kiwango cha mfumuko wa bei, ambacho kilikuwa cha asilimia 33.9 baina ya mwaka 1980 na 1990, asilimia 7.2 mwaka 1991 na 2000 hivi sasa ni cha asilimia 4. Pamoja na mafanikio haya, kiwango cha ukuaji wa pato la mtu kinaathiriwa na hali ya kutegemea zaidi kilimo na kiwango kidogo cha masuala ya ujuzi. Utafiti umeonesha kuwa kuna uhusiano mkubwa baina ya uandikishaji wa kiwango cha chini, ufahamu mbovu na matokeo ya masomo yasiyoridhisha.

Mwisho hali hii hupelekea kiwango cha umasikini kuongezeka. Kuikabili hali hii ni lazima kuzingatia kwa umakini mkubwa suala la elimu kama uwekezaji na kwamba ndiyo inayoandaa rasilimali watu kwa ajili ya kufanya kazi zenye tija. Hili linamaanisha kuwa mfumo wa elimu unapaswa kutoa wahitimu ambao wataanza kufanya kazi katika umri unaostahiki na kuwa na sifa zinazohitajika.

Zanzibar inafanya kila juhudi kukabiliana na changamoto zilizopo.

# SURA YA KWANZA
# USULI

## 1.0 HISTORIA.

Mara baada ya Mapinduzi ya 1964 zaidi ya miaka arubaini iliyopita, elimu bila ya malipo ilitangazwa kwa Wazanzibari wote bila kujali rangi, dini au jinsia. Mabadiliko mengi yametokea katika miaka ya kati. Katika miaka ya karibuni Zanzibar imetayarisha sera na nyaraka tafauti zenye lengo la kuelezea fursa, usawa na ubora katika upatikanaji wa huduma.
Nyaraka hizi pia zimeibua mapungufu yanayoukabili mfumo wa elimu. Katika mwaka 1991 serikali ilichapisha sera ya elimu ya Zanzibar ambayo inaelezea malengo ya msingi ya kisekta na mwelekeo wake. Sera hiyo ilifanyiwa marekebisho katika mwaka 1995 ili kuhakikisha pia inaendana na malengo na maazimio ya mikataba muhimu ya kimataifa. Miongoni mwa malengo na maazimio hayo ni tangazo la Elimu kwa Wote la mwaka 1990 (EFA), Azimio la haki ya mtoto (CRC), Azimio la kutokomeza ukandamizaji dhidi ya wanawake (CEDAW) na mkutano wa dunia wa mwaka 1994 katika kuhakikisha fursa na ubora wa elimu unapatikana pia kwa wenye mahitaji maalumu.

Ili kutekeleza sera ya mwaka 1995 iliyofanyiwa marekebisho, Wizara inayosimamia utoaji wa elimu iliandaa Mpango Mkuu wa Elimu (ZEMAP) mwaka 1996 ukiwa na malengo mahususi ya utekelezaji wa mipango kwa kipindi cha miaka kumi ijayo. Mambo muhimu yaliyomo katika mpango huu yanajumuisha upatikanaji wa fursa, usawa, ubora wa elimu, uhalisia, ukuzaji wa sayansi na teknolojia na kuimarisha utoaji wa huduma ya elimu ya maandalizi.

Mpango huu ulitekelezwa kupitia mikakati minne ifuatayo;

- Kukuza weledi, uwezo na kuboresha ustawi wa walimu .
- Kukuza ushirikiano na taasisi zisizo za kiserikali ( NGOs) katika maendeleo na utoaji wa elimu kwa kuwapa motisha.
- Kuimarisha usimamizi katika ngazi ya skuli, kamati za skuli, jamii pamoja na washirika wa serikali za mitaa.
- Kuhamasisha uchangiaji wa hiari katika elimu.

Mikakati hii imeandaliwa ili kuhakikisha umiliki na usimamizi wa jamii katika maendeleo ya elimu, kukuza ushirikiano, utawala bora na uwazi katika kuandaa na kutekeleza mipango ya maendeleo, kujenga uwezo na kutumia misaada ya washirika wa maendeleo kwa ufanisi.

## 1.1 CHANGAMOTO.

Kuna ushahidi kwamba serikali imekabiliwa na upungufu wa rasilimali katika kufikia malengo yake yaliyoingizwa katika sera zilizopita yanayohusiana na fursa, usawa na ubora. Elimu ya msingi imeimarishwa katika sehemu zote za jamii na kwa sasa imesaidia kufikia usawa wa kijinsia katika miaka 10 ya elimu ya lazima. Kwa hakika hata baada ya elimu ya msingi, yaani miaka miwili ya elimu ya sekondari, usawa wa elimu umefikiwa. Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo idadi ya wanawake imeizidi ya wanaume. Pamoja na mafanikio haya, bado kuna malengo ambayo hayajafikiwa. Kwa mfano, takwimu zinaonesha kwamba, ni mtoto mmoja tu kati ya watoto saba alipitia elimu ya maandalizi kabla kuanza elimu ya msingi. Vile vile, uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya msingi hauridhishi.

Katika mwaka 2002, wanafunzi wenye umri wa kuandikishwa katika ngazi ya elimu ya msingi (NER) walifikia asilimia 78.9 na uandikishaji wa jumla bila kuzingatia umri (GER) ulikuwa unakaribia asilimia 100. Kwa elimu ya lazima, katika mwaka huo huo wanafunzi wenye umri wa kuandikishwa (NER) na uandikishaji wa jumla bila kuzingatia umri (GER) ulifikia asilimia 65.6

na 84.6 kwa kufuatana. Takwimu hizi zinaonesha kwamba idadi kubwa ya wanafunzi katika elimu ya msingi na elimu ya lazima wana umri mkubwa. Ikiwa tutafanya uchunguzi wa asilimia ya wale wanaomaliza miaka miwili baada ya miaka 10 ya elimu ya lazima, tunapata taswira ya kuvunja moyo, kwani ni asilimia 14 tu ya wanafunzi walioandikishwa katika ngazi ya elimu ya msingi ndio waliomaliza kidato cha nne.

Kuna masikitiko mengi kwamba ubora ya elimu inayotolewa kwa vijana umeshuka sana. Kwa wale wanaomaliza elimu ya lazima ni dhaifu katika lugha zote mbili, lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Kwa ujumla, wanakosa ujuzi na taaluma katika mawasiliano yaliyo bora, mambo yanayoendana na wakati, sayansi na hisabati, hali hii ni tafauti ukilinganisha na watoto wa umri wao katika nchi za jirani. Hayo yamebainishwa na utafiti uliochunguza ubora wa elimu ya msingi, (SACMEQ) uliofanyika katika miaka ya 1995 na 2000. Pia kuna malalamiko kuwa, wanafunzi wanamaliza elimu ya lazima bila kuwa na ujuzi wowote wa maana na hivyo wanakuwa hawakuandaliwa kuingia katika soko la ajira. Idadi ya watu wazima wenye uwezo wa kusoma na kuandika imeshuka katika miaka michache iliyopita.

## 1.2 HAJA YA KUWA NA SERA MPYA YA ELIMU.

Sasa hivi tafiti mbalimbali zimefanyika. Miongoni mwa hizo ni:
Tathmini ya EFA ya mwaka 2000, mapitio ya Mpango Mkuu wa Elimu (ZEMAP) ya kipindi cha kati (2002) na mapitio ya sekta ya elimu Zanzibar (2003). Ripoti hizo zimethibitisha mafanikio katika sekta ya elimu, udhaifu, malengo ambayo hayajafikiwa na changamoto mpya zinazoukabili mfumo wa elimu. Mfano wa changamoto hizo ni; utandawazi, mchakato wa ubinafsishaji, sera za uchumi zenye ushawishi wa serikali, kufikia malengo ya elimu kwa wote, malengo ya milenia (MDGS), shabaha ya mpango wa kupunguza umasikini (MKUZA), malengo ya dira 2020 pamoja na malengo mengine mbali mbali ya kitaifa na kimataifa.

Utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Elimu (ZEMAP) umefuata mfumo wa miradi ambapo marekebisho na uimarishaji wa sekta ya elimu hautekelezwi kwa pamoja na hivyo kuzorotesha maendeleo ya elimu. Mfumo huu wa utekelezaji umepelekea kutokuwa na usawa baina ya wilaya na mikoa na hivyo kuharibu malengo na shabaha zilizowekwa na sekta ya elimu. Hivyo kuna haja ya kuwa na mfumo shirikishi utakaowaunganisha wadau wote wa sekta ya elimu kuwa kitu kimoja na hivyo kupelekea jitihada za maendeleo ya elimu kuratibiwa ili kuhakikisha mafanikio ya malengo na maazimio katika elimu yanafikiwa. Mtazamo wa Wizara na washirika wa maendeleo ni kufuata mfumo shirikishi katika utekelezaji wa mipango ya kisekta (SWAp). Msemo huu mpya (SWAP) umegusa nyoyo na akili za viongozi wa elimu na watayarishaji mipango na wameukumbatia na kuukubali.

Mpango shirikishi wa kisekta (SWAp) unaaminika kuwa ndio hasa utakaopelekea mafanikio ya malengo ya EFA, MDGs na mikataba mingine ya kimataifa. Inaaminika kwamba inaweza kutoa utatuzi wa changamoto zinazoikabili sekta ya elimu.

Sababu hizo ndizo zilizopelekea kutayarishwa Sera mpya ya elimu ya Zanzibar ili iweze kuwa na malengo halisi yatakayoendana na jitihada za serikali pamoja na mashirika ya kimataifa katika kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Sera hii vile vile itaendana na mpango wa serikali wa kupunguza umasikini (MKUZA), malengo ya milenia (MDGs), malengo ya elimu kwa wote (EFA) na shauku ya kufikia malengo yaliyo elezwa na dira ya 2020.

## SURA YA PILI
## DIRA, DHAMIRA, MALENGO NA MIKAKATI

### 2.0 DIRA.

Kuwa na jamii ya kidemokrasia, yenye amani inayohitaji kupata elimu bora na kuwekeza katika elimu ya muda mrefu kama njia ya kukabiliana na changamoto za kimaendeleo.

### 2.1 DHAMIRA.

Kupata fursa, usawa, elimu bora kwa wote na kukuza taaluma endelevu. Hivyo taaluma inahitaji kuimarishwa na kurithishwa kwa kizazi kijacho. Kuhakikisha kuwa elimu tunayotoa katika skuli zetu italeta maendeleo katika jamii na kumudu kukabiliana na changamoto zinazotukabili. Kwa hivyo yale yanayofundishwa lazima yakidhi mahitaji ya msingi kwa muda mrefu. Hii ina maana, maarifa wanayopata wanafunzi yawasaidie kubadilika na kuwa wasimamizi wazuri wa mabadiliko kwa lengo la kuitumikia jamii na kuimarisha mazingira.

### 2.2 MALENGO.

**Malengo ya jumla ya elimu ni:**

a) Kukuza na kuendeleza maadili ya utamaduni, itikadi, desturi za Watanzania ili kuimarisha umoja na utambulisho wa kitaifa.
b) Kukuza upatikanaji na matumizi sahihi ya ujuzi na maarifa kwa ajili ya maendeleo endelevu ya jamii.
c) Kuwawezesha raia wote kuelewa na kuheshimu misingi ya katiba,wajibu na haki za binaadamu.
d) Kukuza uelewa wa matumizi sahihi, usimamizi na uhifadhi wa mazingira.
e) Kuongeza upendo, heshima na nidhamu katika kazi, ili kuongeza ufanisi
f) Kuhamasisha ufuataji wa kanuni, kuendeleza amani na uvumilivu, upendo, haki, uelewa wa haki na wajibu wa binadamu, umoja wa kitaifa, ushirikiano wa kimataifa kama unavyoelezwa katika mikataba ya msingi ya kimataifa.

### 2.3 MALENGO YA ELIMU.

Dira na dhamira ya elimu itafikiwa kupitia malengo ya kimkakati yafuatayo:

**(i) Kupanua fursa na Usawa.**
**Mikakati.**

- Kupanua upatikanaji wa fursa ya elimu ya lazima kwa miaka kumi na mbili kwa wanafunzi wote kuanzia elimu ya maandalizi mpaka kufikia kiwango cha kidato cha nne.
- Kurahisisha upatikanaji wa elimu endelevu kupitia mfumo wa elimu ya jadi au kwa njia ya mafunzo ya stadi za kazi.
- Kutoa fursa sawa ya elimu kwa makundi maalumu kama vile watu wenye mahitaji maalumu.

**(ii) Kukuza ubora na ufanisi wa mfumo wa elimu.**
**Mikakati.**

- Kuongeza ubora wa elimu kwa wanafunzi ili waweze kukuza ujuzi wao wenyewe na kutambua uwezo wao kama raia.
- Kuboresha elimu na mafunzo kwa walimu ili ujuzi na maarifa yaendane na mabadiliko na matarajio ya jamii na kukidhi mahitaji ya wanafunzi.
- Kuwapatia wanafunzi ujuzi unaohitajika kwa ajili ya maisha yao.

**(iii) Kuhakikisha upatikanaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa walimu, wanafunzi na wafanyakazi.**
**Mikakati.**

- Kuwapatia walimu ujuzi juu ya matumizi ya mtandao na teknolojia ya habari na mawasiliano kama zana muhimu za kujifunzia na kufundishia.
- Kuwapatia wanafunzi ujuzi na maarifa ya kutumia kompyuta.
- Kusambaza kompyuta sehemu za kazi zitakazosaidia kuleta ubora na ufanisi katika mfumo wa elimu.

**(iv) Kukuza uwezo wa kisayansi na kiteknolojia.**
**Mikakati.**

- Kupanua fursa za upatikanaji wa elimu ya mafunzo ya amali katika maeneo mbali mbali ili kukidhi mahitaji ya watu binafsi na jamii.
- Kuhamasisha wanafunzi na jamii kupenda masomo ya sayansi na hisabati.

**(v) Kuimarisha Elimu ya Juu.**
**Mikakati.**

- Kuibadilisha jamii ya Wazanzibari kuwa rasilimali watu yenye uwezo wa kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya mazingira.

**(vi) Kukuza Utawala Bora katika Elimu.**
**Mikakati.**

- Kukabidhi madaraka na wajibu katika ngazi za chini za uongozi.
- Kuendeleza kada ya uongozi na wafanyakazi katika sekta ya elimu ili wafanye kazi kwa ufanisi na kujitolea.
- Kuimarisha ushirikiano wa sekta za umma na sekta binafsi.

**(vii) Mkakati wa kuweka mazingira salama ya afya kwa kujifunza na kufundisha.**

- Kuzuia kuenea kwa VVU / UKIMWI na magonjwa mengine ya kuambukiza yanayotokana na kujamiiana.
- Kujenga mazingira mazuri, salama na rafiki kwa mwanafunzi na kuhakikisha anakuwa huru dhidi ya ubaguzi, udhalilishaji na unyanyasaji.

**(viii) Mkakati wa kufanya matumizi bora ya rasilimali.**

- Kutumia vyema wataalamu.
- Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kununua zana za kujifunzia na kufundishia pamoja na kumuendeleza mwalimu kitaaluma.
- Kutekeleza mikakati ya kupunguza gharama.

## SURA YA TATU
## MUUNDO WA ELIMU

### 3.0 UTANGULIZI.

Nchi nyingi za Kiafrika ikiwemo Zanzibar, zina mifumo na miundo ya elimu ambayo haiendani na mahitaji ya jamii. Mifumo na miundo hiyo inawaweka wanafunzi skuli kwa muda mrefu na inatoa wahitimu ambao hufanya kazi katika baadhi ya sekta rasmin. Wengi wao wanapomaliza elimu ya lazima ama wanabakia bila ya ajira au hawawezi kukitumia kile walichojifunza kwa ajili ya kujiajiri wenyewe.

Serikali ya Zanzibar kwa kulielewa hili, iliamua kubadilisha mfumo wa elimu uwe kulingana na mahitaji. Njia moja ya kufikia malengo hayo ni kuanzisha mfumo mzuri wa elimu ambao utaweza kusimamia vizuri mgawanyo wa rasilimali zilizopo ikiwemo mgawanyo wa walimu.Vile vile itaondoa mgongano wa mifumo iliopo miongoni mwa watu.

### 3.1 MUUNDO WA ELIMU

#### 3.1.1 Utangulizi

Miundo ya mifumo ya elimu kwa nchi nyingi inatambua angalau ngazi nne (4) za elimu ambazo zinaangalia hatua za mwanzo za makuzi ya mwanaadamu. Ngazi hizi ni; ngazi ya elimu ya maandalizi, msingi, sekondari na elimu ya juu. Mifumo mengine huigawa katika ngazi ndogo ndogo kama vile sekondari ya awali na sekondari ya juu.

Katika hali nyengine, ngazi hizi hugawiwa zaidi kutokana na utashi wa kuongeza fursa katika ngazi za elimu zinazofuata au kubainisha ngazi za kipaumbele au kuanzisha mtiririko mzuri utakaoleta ufanisi.

#### 3.1.2 Hali ya sasa

Mfumo wa elimu uliopo unajumuisha ngazi kadhaa. Ngazi hizi ni ngazi ya elimu ya msingi ambayo itakuwa ya miaka saba, elimu ya sekondari ambayo ina mikondo miwili – mkondo mmoja umegawika katika sehemu mbili ( mkondo wa kwanza utakuwa wa miaka mitatu na wa pili utakuwa wa miaka miwili) na mwengine utakuwa wa miaka minne mfululizo. Mikondo yote miwili inapelekea elimu ya juu ambayo itakuwa ni ya miaka miwili.

Hii ina maana kwamba, katika ngazi ya elimu ya sekondari kuna miundo miwili iliyosambamba, ambayo ni muundo wa kawaida wa 3-2-2 na ule wa mchepuo wa 4-2. Muundo uliopo kwa elimu ya msingi na elimu ya sekondari ni 7-3-2-2 (kwa wasiofaulu mchepuo) na 7-4-2 (kwa waliofaulu mchepuo). Muundo uliopo unatoa elimu ya lazima ya miaka 10 (7-3) kwa wanafunzi wote.

##### 3.1.2.1 Mafanikio.

- Zanzibar ni miongoni mwa nchi chache zilizoko kusini mwa jangwa la Sahara zinazotoa elimu ya lazima ya miaka 10.
- Muundo uliopo unatoa fursa ya upatikanaji wa elimu ya sekondari ya awali kwa wanafunzi wote.

##### 3.1.2.2 Mapungufu.

- Muundo uliopo unatatiza uchambuzi na mgawanyo wa walimu na skuli katika ngazi mbalimbali za elimu.
- Muundo hautowi kipaumbele kwa elimu ya maandalizi na elimu ya juu.

- Mwaka mmoja zaidi wa darasa la matayarisho ya elimu ya sekondari katika sekondari ya awali unaongeza muda wa kusoma na mahitaji ya rasilimali.

**3.1.2.3 Tamko la Sera.**

- Mfumo wa elimu rasmin utakua 2-6-4-2-3$^{+}$ (kwa maana kwamba, elimu ya maandalizi ni miaka 2, elimu ya msingi ni miaka 6, elimu ya sekondari mpaka kidatu cha nne ni miaka 4, elimu sekondari ya juu kidatu cha tano na sita ni miaka 2 na elimu ya juu itakua kwa uchache miaka 3.
- Elimu rasmin itagawiwa katika ngazi ya elimu ya maandalizi, msingi, sekondari, sekondari ya juu na elimu ya juu.

**3.1.2.4 Mikakati**

- Kutafsiri na kuunganisha mfumo wa elimu uliopo ili uendane na mapendekezo ya Sera mpya.
- Kutoruhusu uchaguzi wa masomo katika ngazi za awali za elimu.
- Kuanzisha miaka 2 ya elimu ya maandalizi kuwa sehemu ya elimu ya lazima, ikifuatiwa na miaka 6 ya elimu ya msingi na miaka 4 ya elimu ya sekondari ya awali.
- Kuanzisha ushirikiano na Taasisi zinazoshughulikia elimu.

## 3.2 UMRI WA KUANZA MASOMO.

### 3.2.1 Utangulizi

Kuanza skuli katika umri mdogo ni muhimu kwa kujenga msingi imara wa mafanikio katika kujifunza. Sera imeona kuwa umri wa 4-5 ndio muda mzuri kwa mtoto kujifunza na kufundishika.

### 3.2.2 Hali ya sasa

Sera iliyopo inamtaka mtoto kuanza skuli katika ngazi ya elimu ya msingi akiwa na umri wa miaka 7, hali hii imepelekea wanafunzi wengi kumaliza elimu ya lazima wakiwa na umri wa miaka 16 au zaidi. Hivyo basi, watoto wanaoanza skuli wakiwa na umri wa miaka 7 au zaidi hukosa sehemu muhimu ya elimu ya maandalizi. Mbaya zaidi, watoto hawa huchanganywa katika darasa moja na watoto waliobahatika kusoma elimu ya maandalizi. Watoto wasiobahatika kusoma elimu ya maandalizi kwa kawaida wapo katika mazingira magumu ya kujifunza.

**3.2.2.1 Mafanikio.**

- Watoto humaliza elimu ya lazima wakiwa na umri unaowawezesha kutafuta fursa za kuendelea na masomo au kuanzisha biashara zao wenyewe.

**3.2.2.2 Mapungufu.**

- Watoto wengi huanza elimu ya msingi wakiwa na umri wa miaka 7 au zaidi.
- Madarasa mengi yana wanafunzi wenye umri na uwezo tafauti hali inayopelekea utoaji wa elimu kuwa mgumu.
- Ni vigumu kuyagawa madarasa kwa kigezo cha umri.
- Haizingatii wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**3.2.2.3 Tamko la Sera.**

- Umri wa kuanza elimu ya maandalizi utakuwa ni miaka minne, elimu ya msingi ni miaka sita, elimu ya sekondari ya awali ni miaka 12 na sekondari ya juu ni miaka 16.

**3.2.2.4 Mikakati.**

- Kuweka umri maalumu wa kuanza skuli
- Majina ya skuli yaendane na ngazi ya elimu.
- Kuhakikisha wanafunzi wote wanaanza masomo katika elimu ya maandalizi wakiwa na umri wa miaka 4 kwa utaratibu maalumu.

## SURA YA NNE
## UPATIKANAJI WA ELIMU NA KWA USAWA

### 4.0 UTANGULIZI.

“Elimu ni haki ya msingi ya binaadamu". Ni ufunguo wa kufikia katika maendeleo endelevu, amani na utulivu miongoni mwa nchi mbali mbali na kwa hivyo ni nyenzo ambayo haiepukiki katika kufikia ushiriki madhubuti kwenye masuala ya kijamii na kiuchumi ambayo yanaathiriwa na utandawazi unaoenea kwa kasi katika karne ya ishirini na moja. Kuyafikia malengo ya Elimu kwa Wote (EFA) ni suala la lazima.

Upatikanaji wa mahitaji ya msingi kwa watu wote katika kujifunza ni suala ambalo linawezekana na ni lazima lifikiwe kwa haraka (Mpango wa utelezaji wa Dakar).

Kwa mujibu wa Azimio hili la Mpango wa Elimu Ulimwenguni la mwaka 2000, Zanzibar kama zilivyo nchi nyengine duniani imeongeza kasi ya uwajibikaji wake katika utoaji wa elimu kwa wote bila ya kuzingatia kabila, rangi ya ngozi, matabaka au uwezo wa kiuchumi. Mkazo mkubwa umekuwa ukiwekwa katika suala la kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu katika ngazi zote. Kiwango cha uandikishaji wa watoto katika ngazi ya elimu ya msingi bila ya kuzingatia umri kilikuwa ni cha asilimia 100.3 mwaka 2004 ambapo takriban mlingano wa kijinsia ulikuwa uwiano wa 1: 1. Katika ngazi ya elimu ya lazima (yaani elimu ya msingi na miaka miwili ya elimu ya sekondari- kidato cha 1 na II) kwa ujumla uandikishaji ulifikia asilimia 91.5. Elimu ya lazima inapaswa kuwa kwa ajili ya watu wote lakini baada ya elimu hiyo, elimu hutolewa kwa masharti ya kufaulu. Kwa bahati mbaya uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya maandalizi na ngazi ya elimu ya juu ni wa kiwango cha chini kwa sababu upatikanaji wa elimu katika ngazi hizi si suala la lazima.

Pamoja na mafanikio hayo, lengo la usawa wa kielimu bado halijafikiwa ipasavyo. Ingawa elimu inatolewa bila ya malipo, umasikini ni kikwazo kikubwa kinachowafanya watoto kukosa fursa ya elimu. Katika baadhi ya wilaya, ushiriki wa watoto wa kike katika kupata elimu ni wa kiwango cha chini sambamba na hilo utoaji wa elimu kwa watoto wenye mahitaji maalumu unahitaji kupewa mazingatio maalumu.

### 4.1 ELIMU YA MAANDALIZI.

#### 4.1.1 Utangulizi

Umri wa miaka 4-6 ni umri muhimu kwa ajili ya makuzi ya mtoto, maendeleo yake na kupata elimu. Huu ni wakati ambapo kwa wastani mtoto anakuwa anakuza tabia chanya za kujifunza, anakuza uwezo wa kufikiri, anapata ujuzi wa kujitatulia matatizo na anakuza ujuzi wake wa lugha.

Ufanyaji kazi wa akili ya mtoto unakuwa umo katika kukua na kuweza kutambua mambo yaliyomo katika mazingira yake kwa kutumia vitu ambavyo vinaweza kuchezewa kwa kuvishika.

Katika ngazi hii mtaala unapaswa uwe ule unaomlenga mtoto na kujifunza ni lazima kutoe fursa mbali mbali za kumfanya anayejifunza kutambua maumbo na rangi tafauti. Elimu ya maandalizi inamtayarisha mtoto kuanza elimu ya msingi kwa ufanisi.

#### 4.1.2 Hali ya sasa.

Elimu ya maandalizi inatolewa na Serikali, taasisi, jumuia na watu binafsi kwa watoto wenye umri wa miaka 4-6. Hadi hivi sasa zipo jumla ya skuli 181 ambazo zinatoa elimu ya maandalizi. Miongoni mwa skuli hizi, 24 ni za serikali, 157 zinamilikiwa na watu binafsi ambapo kati ya hizo skuli 65 zinaendeshwa na jamii chini ya mfumo wa Madrassa na kufadhiliwa na Shirika la Mfuko wa Agakhan.

Sekta hii hadi sasa imeshaandikisha watoto 15,601 wenye umri huo ambao ni sawa na asilimia 13.8 tu. Elimu inayotolewa kwa watoto hao inatilia mkazo zaidi stadi za msingi za kusoma na kuhesabu na inatoa mkazo mdogo sana kwenye masuala mengine muhimu kwa ajili ya ukuaji wa mtoto.

Kwa bahati mbaya hakuna skuli za maandalizi ambazo zinawazingatia watoto wenye mahitaji maalumu wa umri wa kundi hili. Pia zipo tafauti miongoni mwa taasisi mbali mbali zinazotoa elimu za maandalizi. Tafauti hizo zinajidhihirisha katika masuala ya mitaala, umri wa kuanza skuli, muda, masaa ya kufundishia, ubora na ufanisi.

##### 4.1.2.1 Mafanikio.

- Mchango wa taasisi za watu binafsi umeisaidia sekta hii kuonesha kua inakuwa vizuri ukilinganisha na wakati ambapo Serikali ilikuwa inamiliki uendeshaji skuli za maandalizi peke yake.
- Mipango inaandaliwa kuweka uwiano baina ya serikali na sekta za watu binafsi katika kuandaa na kutumia mtaala mmoja - kwa kuanzia.

##### 4.1.2.2 Mapungufu.

- Kwa vile ngazi ya elimu ya maandalizi si ya lazima, serikali haikuitilia maanani na kuishughulikia ipasavyo.
- Kutokuwepo kwa uwiano katika utoaji wa elimu ya maandalizi imepelekea skuli nyingi kuwepo maeneo ya mjini na hivyo kuleta tafauti kubwa ya upatikanaji wa elimu hiyo baina ya vijijini na mjini.
- Hakuna miongozo ya kisera kwenye masuala mengi yanayohusiana na makuzi ya mtoto.
- Watoto wenye mahitaji maalumu hawapatiwi Elimu ya Maandalizi.
- TEKNOHAMA haitolewi kwa watoto katika ngazi za awali.
- Hakuna maingiliano ya kikazi baina ya wanaotoa huduma ya uangalizi kwa watoto na walimu wa skuli za maandalizi.

##### 4.1.2.3 Tamko la Sera.

- Elimu ya mandalizi kwa watoto wenye umri kati ya miaka 4-5 itakua rasmi na itaingizwa katika mfumo rasmi wa elimu ya lazima.
- Ushirikiano na wazazi, jamii, taasisi zisizokuwa za serikali na wadau wengine utakuzwa na kuendelezwa ili kuimarisha afya ya mtoto, lishe, makuzi na maendeleo yake.
- Sera na miongozo imara itaandaliwa kwa lengo la kuimarisha mashirikiano ya sekta husika kwenye makuzi ya mtoto.
- Jamii na taasisi zisizo za serikali zitashirikishwa ipasavyo kwenye shughuli zote za utekelezaji wa masuala ya elimu ya maandalizi na zitashajiishwa kuanzisha vituo vya elimu ya maandalizi hususan vijijini.

- Mtaala wa elimu ya maandalizi utaingiza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
- Juhudi za makusudi zitachukuliwa kuhakikisha watoto wenye mahitaji maalumu wanapatiwa elimu ya maandalizi.

**4.1.2.4 Mikakati.**

- Kuunganisha nguvu zilizopo katika miundo mbinu ya serikali na uwezo wa walimu sambamba na utendaji mzuri wa skuli za jamii hususan kwenye utoaji wa elimu na uhusiano baina ya mwalimu na mwanafunzi.
- Kuweka umri mahususi wa kuanza elimu ya maandalizi.
- Kuimarisha nyenzo za mafunzo kwenye ngazi ya maandalizi.
- Kushajiisha uanzishwaji wa skuli za maandalizi.
- Kutoa miongozo kwa ajili ya vituo vya maandalizi ili kukidhi mahitaji ya makuzi ya mtoto na kuhakikisha ubora unadhibitiwa.
- Kufanya utafiti ili kuangalia uwezekano wa kuvitumia vyuo vya Kuraani katika utoaji wa elimu ya maandalizi.
- Kuhakikisha kuwa jamii zinashiriki kikamilifu katika uendeshaji wa skuli kwa kutilia mkazo mada zilizomo katika mtaala na usimamizi wa rasilimali.
- Kutoa elimu ya maandalizi inayofaa na yenye uhalisia na kutoa mkazo maalumu kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na wale wenye mahitaji maalumu ya kielimu.
- Kutayarisha programu zitakazowaelimisha watoto Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) mapema iwezekanavyo.
- Kuhakikisha kuna usawa wa kijinsia katika wilaya zote.
- Kukuza mashirikiano mazuri kati ya wizara, vituo vya afya, jamii, taasisi zisizo za kiserikali na vyombo mbali mbali vya serikali katika utoaji wa elimu, huduma za afya, lishe na mahitaji mengine ya watoto hususan wenye umri kati ya miaka 0 - 3.

## 4.2 ELIMU YA MSINGI.

**4.2.1** Utangulizi**.**

Elimu ya msingi inapaswa kuwa ya lazima, bila ya malipo na yenye ubora kwa vile ni ngazi ambayo wanaipata watoto wengi. Elimu katika ngazi hii inaongozwa na dhana ya ujumla juu ya maendeleo ya makuzi ya mtoto na kutilia mkazo mahitaji maalum ya kila mtoto katika ngazi hii wanafunzi wanakuzwa ujuzi na uelewa wa kuhesabu, kusoma, kufikiri na kuhoji kimantiki, kwenye ngazi hii stadi mbali mbali kwa ajili ya kujifunza zaidi zinakuzwa.

**4.2.2 Hali ya sasa.**

Elimu ya msingi ni sehemu ya elimu ya lazima inayotolewa bila ya malipo kwa watoto wenye umri kati ya miaka 7-13. Ngazi hii ya elimu inahusisha miaka saba ya elimu ya lazima. Hivi sasa idadi ya wanafunzi walioandikishwa ni 199,938 sawa na asilimia 100.3 ya uandikishaji, ukuaji wa kasi ya uandikishaji unatokana na juhudi zinafanywa na wazazi katika ujenzi wa madarasa ya kusomea. Ingawa elimu ya msingi ni ya lazima na inatolewa bila ya malipo bado kiwango cha uandikishaji kwa watoto wenye umri wa kuwa elimu ya msingi ni ndogo. Kwa mfano, kiwango cha uandikishaji kwa mwaka 2002 kilikuwa asilimia 77.3 kwa wanaume na asilimia 78.7 kwa wanawake. Hali hii inaonesha kwamba kuna idadi kubwa ya watoto wenye umri wa kwenda skuli ambao ama hawakuandikishwa au waliandikishwa wakiwa na umri mkubwa.

**4.2.2.1** Mafanikio**.**

- Ngazi ya elimu ya msingi Zanzibar imepewa umuhimu mkubwa kisheria na uandikishwaji wa watoto katika ngazi hii ni wa lazima.
- Kiwango cha uandikishaji kwa watoto wenye umri wa ngazi ya elimu ya msingi kinaongezeka.
- Kuna mwamko mkubwa kwa wazazi na jamii katika kuwaandikisha na kuwapeleka watoto wao skuli.
- Ushiriki wa jamii katika ujenzi wa madarasa umeisaidia Serikali kwa kiasi kikubwa.
- Kuna vituo visivyopungua vitano kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu.

#### 4.2.2.2 Mapungufu.

- Elimu ya msingi bado inaendelea kukabiliwa na uchache wa madarasa na baadhi ya skuli zina msongamano mkubwa wa wanafunzi madarasani.
- Watoto hawaandikishwi katika umri sahihi kutokana na upungufu wa madarasa.
- Kuna tafauti ya upatikanaji wa fursa ya elimu kati ya Wilaya na Wilaya na hata ndani ya Wilaya moja uliosababishwa na kutozingatia maeneo sahihi ya ujenzi wa skuli.
- Kiasi cha asilimia 22.3 ya watoto wenye umri wa kwenda skuli hawasomi skuli.
- Hakuna matumizi ya TEKNOHAMA.
- Skuli nyingi haziwezi kupanuliwa kutokana na maeneo yake kuvamiwa na makaazi ya watu.

#### 4.2.2.3 Tamko la sera.

- Serikali itahakikisha kuwa watoto wote waliofikia umri wa kuandikishwa skuli wanaandikishwa, wanahudhuria skuli ipasavyo, wanafaulu vizuri na kumaliza skuli ya msingi kwa ufanisi.
- Ujenzi wa skuli utazingatia maeneo yenye mahitaji ili kuondoa tafauti zilizopo katika kupata fursa ya elimu baina ya wilaya na ndani ya wilaya na pia kuleta mazingira mazuri ya kujifunzia.
- Mtaala wa elimu ya msingi utajumuisha TEKNOHAMA.

#### 4.2.2.4 Mikakati.

- Ujenzi wa skuli utazingatia maeneo yenye mahitaji kama mkakati wa kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu.
- Kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya msingi kwa kutumia mfumo shirikishi wa utoaji wa elimu kama vile; usomeshaji kwa kuchanganya madarasa, elimu masafa, kusomesha kwa kutumia njia ya redio na televisheni.
- Kuhakikisha kwamba shughuli za ukarabati wa majengo ya skuli zinaendelea.
- Kutayarisha vigezo vya kubainisha mazingira mazuri ya kujifunza yanayopasa kuwepo katika madarasa ya ngazi ya elimu ya msingi.
- Kuhamasisha matumizi ya TEKNOHAMA.
- Kuanzisha mfumo wa kuratibu uhusiano baina ya skuli za maandalizi, skuli za msingi, skuli za sekondari, jamii na sekta ya watu binafsi.

## 4.3 ELIMU YA SEKONDARI.

### 4.3.1 Utangulizi.

Msingi wa elimu ya sekondari unajengwa kutokana na ujuzi na maarifa yaliyopatikana kutoka ngazi ya elimu ya msingi. Elimu hii huwaandaa wanafunzi katika kutoa hoja za msingi na

kukuza uwezo wa uchambuzi na ufafanuzi. Inadhamiria kuwaandaa wanafunzi katika kutafuta elimu zaidi na mafunzo mbali mbali kulingana na mahitaji, uwezo na juhudi zao.

Ufaulu katika ngazi ya elimu ya sekondari una umuhimu mkubwa katika kupata ajira zinazoendana na uchumi wa kisasa na ndio msingi wa kufikia elimu ya juu.

**4.3.2 Hali ya sasa.**

Elimu ya sekondari ya awali inatolewa kwa mfumo wa mikondo miwili. Mkondo wa kwanza ni wa miaka mitano ambao mwanafunzi husoma kwa miaka mitatu katika mzunguko wa mwanzo, mwishoni mwa mzunguko huu mwanafunzi hufanya mtihani na wanaofanikiwa huendelea na mzunguko wa pili wa miaka miwili. Mwishoni mwa mzunguko wa pili wanafunzi hufanya mtihani wa Taifa wa kidato cha nne. Kwa wastani wa asilimia 40 ya wanafunzi ambao hufanya mitihani yao ya mzunguko wa kwanza huchaguliwa kuendelea na mzunguko wa pili. Mkondo wa pili wa sekondari ni wa miaka minne mfululizo, ambapo mwishoni wanafunzi hufanya mitihani ya taifa ya kidato cha nne.

Kiasi cha asilimia 3 ya wanafunzi wanaofanya mtihani wa darasa la saba huchaguliwa kuendelea na elimu ya ngazi ya sekondari katika mkondo wa pili. Takwimu za mwaka 2004 zinaonesha kuwa kiasi cha wanafunzi 57,760 waliendelea na elimu ya sekondari ya awali kupitia mkondo wa kwanza na wanafunzi 2,071 waliendelea kwa kupitia mkondo wa pili.

Jumla ya wanafunzi 59,831 wa sekondari ya awali ambao ni sawa na asilimia 50.3 waliandikishwa. Wanawake walikuwa asilimia 50.4, asilimia hii ni kubwa ukilinganisha na ya wanaume. Mchango wa sekta binafsi katika ngazi ya elimu ya sekondari ni mdogo ambapo idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika sekta hii ni 1,393 tu ambao ni sawa na asilimia 2.3 ya wanafunzi wote walioandikishwa.

Uandikishaji wa watoto wenye umri wa kuwa katika ngazi ya elimu ya sekondari imefikia asilimia 14, hii inaonesha kuwa ngazi hii ina idadi kubwa ya wanafunzi wenye umri mkubwa. Ngazi ya elimu ya sekondari imekua kwa haraka kutokana na kukua na kuimarika kwa ufanisi katika ngazi ya elimu ya msingi.

Kupitia mchakato wa kuimarisha skuli, skuli nyingi za sekondari za wakati huu zilianzia kama skuli za msingi, zikajumuisha ngazi ya sekondari ya awali na baadae kuwa sekondari ya kawaida.

**4.3.2.1 Mafanikio.**

- Zanzibar imefanikiwa kutoa angalau miaka mitatu ya elimu ya sekondari kwa wanafunzi wengi.
- Kuwepo kwa skuli za sekondari katika kila wilaya.
- Kuna uwiano wa kijinsia kwa kiasi fulani.
- Inaonekana kuwa ukuaji wa skuli binafsi katika ngazi ya elimu ya msingi unapelekea ukuaji wa sekta ya elimu ya sekondari.

**4.3.2.2 Mapungufu.**

- Mitihani ya kumalizia elimu ya msingi kama njia ya kuwachuja wanafunzi inatoa fursa kwa asilimia ndogo ya wanafunzi kuingia katika skuli za sekondari za michepuo.

- Madarasa mengi yana wanafunzi zaidi ya 40, idadi ambayo imepindukia kigezo kilichowekwa.
- Mfumo wa mikondo miwili una athari hasi za kisaikolojia kwa wanafunzi.
- Kiwango halisi cha uandikishaji kiko chini.
- Uchache wa maabara za sayansi na uhaba wa walimu.
- Wanafunzi wengi hususan wale wa vijijini hawajapata uelewa wa matumizi ya TEKNOHAMA.
- Hakuna nyenzo kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**4.3.2.3 Tamko la sera.**

- Elimu ya sekondari ya miaka minne itatolewa kwa wote.
- Mipango ya kutosha na yenye ufanisi itaandaliwa ili kuleta maendeleo ya elimu ya sekondari yenye ubora.
- Njia mbadala kwenye elimu rasmi ya sekondari zitaandaliwa ili kutoa fursa kwa wanafunzi nje ya mfumo wa elimu rasmi.
- Mazingira mazuri ya skuli yatakayozingatia watu wenye mahitaji maalum yataandaliwa.
- Mtaala wa elimu ya sekondari utajumuisha TEKNOHAMA.

**4.3.2.4 Mikakati.**

- Kujenga skuli za sekondari za mfano katika wilaya zote.
- Kuandaa mpango maalumu utakaobainisha maeneo yenye mahitaji ya kujengwa skuli mpya za sekondari.
- Kuanzisha njia mbadala za utoaji wa elimu ya sekondari, kwa mfano matumizi ya TEKNOHAMA na elimu masafa.
- Kuanzisha mibadala ya elimu rasmi ya sekondari.
- Kuanzisha uhusiano na elimu ya msingi, vituo vya walimu, mafunzo ya ualimu, mafunzo ya amali na ufundi.

## 4.4 ELIMU BAADA YA ELIMU YA LAZIMA.

### 4.4.1 Utangulizi.

Fursa za elimu baada ya elimu ya lazima zinatafautiana miongoni mwa nchi tafauti. Lakini pale ambapo kiwango cha elimu ya msingi ni cha chini, fursa za elimu baada ya elimu ya lazima zinakua chache na pale kiwango kinapokuwa cha juu, fursa zinaongezeka.

Lengo la jumla la elimu baada ya elimu ya lazima ni kuongeza fursa zaidi za elimu ya juu na kuwaandaa wanafunzi kuingia kwenye kada za kitaalamu au kuwapatia ujuzi wenye soko. Pia elimu hiyo inapaswa kuwajengea utashi wa kuendelea kujifunza kwa muda mrefu.
Katika muundo na mfumo wa elimu baada ya elimu ya lazima kutakuwa na uhusiano wa moja kwa moja kwenye muundo wa elimu.

Pamoja na kuwapatia wanafunzi fursa zaidi ya kuendelea na masomo, mfumo wa elimu baada ya elimu ya lazima unapaswa kutoa fursa kwa ajili ya:

- Kujiunga na taasisi za elimu baada ya masomo ya sekondari kwa wanafunzi wenye sifa.
- Kujiendeleza katika kujipatia sifa za juu kwenye utaalamu wa aina moja.
- Kujitafutia sifa za kuendelea na masomo kwa wale ambao hawana sifa hizo.

- Wale wote wanaotaka kubadilisha kada zao za kazi na wanataka kupata mafunzo au kujifunza tena kwa ajili ya kufanya kazi tafauti kuweza kufanya hivyo.

### 4.4.2 Hali ya sasa.

Fursa za masomo baada ya elimu ya lazima hutolewa kwa wanafunzi wanaoendelea mkondo wa pili wa elimu ya sekondari baada ya kufaulu masomo yao. Wanafunzi wengi ambao hufeli mitihani yao ya kidato cha pili hujiunga na madarasa ya elimu ya kujiendeleza, vituo vya elimu ya amali au huchanganyika na wenzao ambao hawajaajiriwa.

Kuna vituo kadhaa vya Serikali na vya binafsi vinavyotoa elimu baada ya ngazi ya elimu ya lazima ambavyo hutoa fursa za masomo katika fani za elimu ya amali na taaluma. Hali halisi inaonesha kwamba ni wahitimu wachache sana wa elimu ya lazima ambao hupata ufadhili wa serikali wa kujiunga na taasisi za elimu baada ya elimu ya lazima, wengi wao hujiunga na taasisi hizo kwa ufadhili wao wenyewe.

#### 4.4.2.1 Mafanikio

- Kuwepo kwa ukuaji wa fursa katika ngazi ya elimu baada ya elimu ya lazima unaotokana na ongezeko la taasisi mbali mbali za serikali na watu binafsi.
- Kuanzishwa kwa taasisi nyingi zaidi za elimu baada ya elimu ya lazima kutokana na juhudi za serikali na watu binafsi.
- Kuanzishwa kwa programu za kukuza elimu mbadala na ujuzi kwa ajili ya vijana ambao hawako skuli na kwa wahitimu wa elimu ya lazima.
- Kufanyika kwa utafiti hivi karibuni juu ya mahitaji ya soko la ajira.

#### 4.4.2.2 Mapungufu.

- Kutokuwepo uhusiano rasmi baina ya taasisi mbalimbali za elimu baada ya elimu ya lazima.
- Elimu baada ya elimu ya lazima hutolewa zaidi maeneo ya mijini.
- Hakuna udhibiti wa ubora wa elimu baada ya elimu ya lazima.
- Kutokuwepo kwa huduma za ushauri nasaha katika skuli za sekondari.
- Elimu baada ya elimu ya lazima inatoa upendeleo zaidi kwa wanaume.

#### 4.4.2.3 Tamko la sera.

- Fursa ya elimu baada ya elimu ya lazima zitaongezwa, kuenezwa, zitakuwa huru na kuzingatia matakwa ya wanafunzi na mahitaji ya soko.
- Kutawekwa mfumo wa kuwazingatia wanafunzi wenye vipaji na kushughulikia mahitaji yao.
- Kutayarisha kanuni na taratibu zitakazo simamia na kuhakikisha ubora wa taasisi zinazotoa elimu baada ya elimu ya lazima.
- Kutahakikishwa usawa wa kijinsia kwenye taasisi zinazotoa elimu baada ya elimu ya lazima.
- Serikali itaweka mazingira mazuri kwa ajili ya sekta binafsi kuanzisha taasisi za utoaji wa taaluma.
- Ushirikiano kati ya taasisi zilizopo na mpya utakuzwa katika kuimarisha utoaji wa elimu baada ya elimu ya lazima.

#### 4.4.2.4 Mikakati.

- Kuanzisha huduma za ushauri katika ngazi ya elimu ya lazima ili kuwawezesha wanafunzi kufanya uchaguzi sahihi wa masomo.
- Kuingiza njia za kujifunzia katika programu za elimu baada ya elimu ya lazima ambazo zitakidhi matakwa na mahitaji ya wanafunzi.
- Kuongeza upatikanaji wa fursa ya elimu katika ngazi ya sekondari ya juu.
- Kuanzisha taasisi mpya za mafunzo ya elimu ya amali pamoja na kuziimarisha zilizopo.
- Kutoa mafunzo kwenye nyanja za ujasiriamali ili kushajiisha watu kubuni ajira na kujiajiri.
- Kuhakikisha usawa wa kijinsia katika kutoa mafunzo na ajira.
- Kuanzisha bodi ya kusimamia na kutoa tunzo za kitaaluma kwa kila ngazi.
- Kushajiisha jamii kujiendeleza zaidi katika mafunzo.
- Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha vituo zaidi vya mafunzo ya elimu ya amali.
- Kuanzisha chombo kitakachosaidia kuendeleza jitihada za wanafunzi kitaaluma.
- Kutoa fursa za mafunzo kwa mayatima na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.
- Kuanzisha uhusiano wa karibu baina ya taasisi zinazotoa elimu baada ya elimu ya lazima na waajiri.

## 4.5 ELIMU YA JUU.

### 4.5.1 Utangulizi

Elimu ya juu ina lengo la kuwapatia wanafunzi uelewa wa hali ya juu, ujuzi na uwezo wa kiutawala ambao ni muhimu katika kuleta ufanisi. Elimu ya juu pia inatoa fursa kwa watoa maamuzi, wataalamu, viongozi wa serikali na sekta binafsi kupata ujuzi mpya wa maendeleo, ubunifu na uwezo wa kufanya maamuzi ipasavyo. Pamoja na hayo, elimu ya juu inatoa fursa ya kujiendeleza kielimu na kufanya utafiti kwenye nyanja muhimu. Pia ni chanzo cha upeo mkubwa wa uelewa na ujuzi unaohitajika kwa ajili ya maendeleo ya taifa. Sambamba na hayo, ili kuondoa tafauti kati ya elimu ya juu na ulimwengu wa ajira, elimu ya juu lazima iwe na uhusiano na shughuli binafsi na viwanda katika kubadilishana ujuzi, uelewa na msaada wa kifedha.

### 4.5.2 Hali ya sasa

Elimu ya juu inatolewa kwenye taasisi moja ya serikali na mbili za watu binafsi. Taasisi hizi ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Chuo Kikuu cha Zanzibar na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu.

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Chuo Kikuu cha Elimu vinatoa fani za lugha, sayansi ya jamii na sayansi kwa ujumla inayohusisha ualimu. Chuo Kikuu cha Zanzibar kinatoa fani za sheria, sharia na usimamizi wa biashara.

Pia wako wanafunzi wengi wa Zanzibar ambao wanasomea fani mbali mbali kwenye vyuo vikuu vya Tanzania Bara. Vile vile, kuna fursa ya elimu ya juu inayotolewa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na vyuo vyengine nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Machi 2004, taasisi hizo tatu za Zanzibar zilikuwa zimedahili jumla ya wanafunzi 948 kati ya hao wanawake ni 207 sawa na asilimia 21.8.

#### 4.5.2.1 Mafanikio.

- Kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

- Kuwepo kwa mazingira mazuri kwa ajili ya kuanzisha na kuongeza idadi ya taasisi binafsi za elimu ya juu.
- Kuongezeka kwa fursa za wanafunzi wa Zanzibar kujiunga na vyuo vya elimu ya juu vilivyopo Tanzania.
- Kuwepo kwa tawi la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Kuongezeka fursa kwa wataalamu wa ndani kufundisha katika ngazi ya chuo kikuu.
- Kuimarika kwa uhusiano na vyuo vikuu vyengine vya ndani na nje ya Tanzania.
- Vyuo vikuu vya ndani ya nchi vimevutia idadi kubwa ya wanafunzi wa kigeni.

**4.5.2.2 Mapungufu.**

- Bado wanafunzi wengi hawapati fursa ya kujiunga na ngazi ya elimu ya juu hususan wanawake.
- Uhaba wa vitivo na programu katika taasisi za elimu ya juu zilizopo.
- Wanafunzi wengi wanakosa fursa ya kujiunga na elimu ya juu kutokana na uhaba wa fedha na nyenzo.
- Uhaba wa wahadhiri wa kudumu wenye sifa.
- Matumizi hafifu ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa ajili ya kufundishia, utawala na utafiti.

**4.5.2.3 Tamko la sera.**

- Serikali itazishajiisha sekta za umma na sekta binafsi kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya juu, kushughulikia mahitaji ya kijamii na kiuchumi na kupanua wigo wa taaluma.
- Juhudi za makusudi zitachukuliwa ili kuongeza kiwango cha ushiriki wa Wazanzibari kwenye elimu ya juu hususan wanawake na wale wenye mahitaji maalum.
- Vyuo vikuu vitaelekeza nguvu zake kwenye ubora wa elimu ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira na kuwa chombo cha tafiti za kitaifa katika kuleta maendeleo.
- Vyuo vikuu vitaandaa programu za elimu masafa.
- Taasisi za elimu ya juu zitaanzisha kitengo cha mfumo wa utambuzi kwa wanafunzi utakaowawezesha kuwa na uhuru zaidi na kwa ajili ya uhamishaji wa wanafunzi miongoni mwa taasisi ili kumruhusu mwanafunzi kuweza kukidhi mahitaji yake katika kujiendeleza kwa uwezo wake.
- Programu na fani mbali mbali zinazotolewa kwenye elimu ya juu zitafanyiwa mapitio ili zilete ufanisi kwa gharama nafuu.
- Taasisi za elimu ya juu zitatumia teknolojia ya habari ya hali ya juu ili kuviunganisha vitivo na vitengo vya fani maalum kwa ajili vyombo vya utoaji wa fani za teknolojia ya habari na kwa kazi za utawala.

**4.5.2.4 Mikakati.**

- Kuandaa programu za elimu ya juu kulingana na mahitaji.
- Kutoa msukumo na vivutio kwa sekta binafsi kuanzisha taasisi za elimu ya juu.
- Kuzitumia taasisi za elimu ya juu ipasavyo.
- Kushajiisha na kuimarisha upatikanaji wa elimu ya juu kupitia elimu masafa na huria.
- Kushajiisha programu za kuwaendeleza wafanyakazi wa vyuo vya elimu ya juu.
- Kuimarisha mafunzo, uhusiano na maingiliano na ulimwengu kupitia vifaa vya TEKNOHAMA.

- Kutoa msukumo kwenye shughuli kuu za kiuchumi katika nchi ili kukuza ukuaji wa masuala ya kiuchumi, kijamii na kuingiza kipato.
- Kuanzisha vituo vya ubora wa taaluma.
- Kuanzisha bodi ambayo itaratibu programu mbali mbali na kutathmini masuala yanayohusiana na elimu ya juu.
- Kuoanisha viwango vya taaluma na uhusiano baina ya taasisi za elimu ya juu ndani na nje ya nchi.

## 4.6 ELIMU KWA WENYE MAHITAJI MAALUM.

### 4.6.1 Utangulizi.

Wanafunzi wenye mahitaji maalum ni pamoja na wale wenye ulemavu wa aina tafauti, wazito katika kujifunza na wale wenye vipaji vikubwa. “Elimu kwa Wote” inaelekeza kuwa kila mtu apate fursa ya elimu, ili kuongeza kasi ya maendeleo katika jamii. Pia inatilia mkazo kuwepo kwa programu mbali mbali ambazo zinatoa elimu bora kwa watu wenye mhitaji maalum ili kuwajenga katika kujiamini na kuweza kutawala mazingira yao vizuri. Miongoni mwa watoto wenye mahitaji maalumu, wamo wenye vipaji na ujuzi ambao iwapo utaimarishwa na kutumika unaweza kuchangia vizuri kwenye maendeleo ya taifa. Kwa mujibu wa malengo ya Elimu kwa Wote, tamko la "Salamanka" na Mpango wa Utekelezaji wa Elimu kwa wenye mahitaji maalumu yanasisitiza kuwepo kwa mikakati ya uimarishaji wa elimu mjumuisho ili kuziwezesha skuli kuwahudumia watoto wote hususan wenye mahitaji maalumu.

### 4.6.2 Hali ya sasa.

Hakuna rikodi halisi ya kiwango cha watoto wenye ulemavu miongoni mwa wanafunzi walioko skuli. Hata hivyo ulemavu wa kusikia, ububu na kuona ni matatizo yanayojitokeza sana. Mwaka 2004 kulikuwa na skuli za msingi tano tu ambazo zilikuwa na madarasa yenye watoto wenye mahitaji maalum ya kielimu. Wanafunzi wasiozidi 2,000 waliandikishwa katika madarasa haya**.** Hiki ni kiwango kidogo cha watoto wenye mahitaji maalum ya kielimu. Hata hivyo idadi hii haikujumuisha wale ambao ni wazito katika kujifunza na wenye vipaji maalumu. Kuwajumuisha watoto wenye ulemavu kwenye skuli za kawaida kunakabiliwa na baadhi ya vikwazo vya kijamii na kiutamaduni. Miongoni mwa vikwazo hivyo ni mitazamo ya baadhi ya wazazi na walimu kwamba kuwemo kwa watoto wenye ulemavu katika skuli za kawaida kutaathiri wepesi wa uendeshaji wa madarasa, kwa vile skuli zenyewe hazina vifaa vya kutosha kukidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu.

#### 4.6.2.1 Mafanikio

- Kuanzishwa kwa mtaala wa elimu mjumuisho katika mafunzo ya ualimu.
- Kuanzishwa kwa taasisi zisizo za serikali zinazotetea haki za watu wenye ulemavu.
- Kuwepo kwa ushirikiano wa karibu baina ya Wizara na jumuia za watu wenye ulemavu.
- Washirika wa maendeleo wapo tayari kutoa msaada kwenye programu za elimu zinazotoa msukumo maalum kwa watoto wenye mahitaji maalum.

#### 4.6.2.2 Mapungufu.

- Skuli nyingi hazijazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.
- Kuwepo kwa uelewa mdogo juu ya mahitaji mahususi ya watoto wenye mahitaji maalumu ya kielimu.

- Uhaba wa walimu wenye sifa za kuwashughulikia wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu.
- Elimu mjumuisho bado haijatekelezwa kwa mafanikio.
- Uhaba wa fedha na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.
- Elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum inatolewa zaidi sehemu za mjini.
- Kutokuwepo uchunguzi wa kiafya wa mara kwa mara.
- Hakuna utaratibu mzuri wa kuwatambua mapema na kuwatathmini watoto wenye vipaji vya juu, wazito wa kujifunza na wenye ulemavu.
- Mwamko mdongo wa jamii juu ya umuhimu wa elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum.
- Kukosekana kwa programu mahususi za maelekezo, kwa mfano lugha ya alama kwa watoto wenye ulemavu wa kusikia.

**4.6.2.3 Tamko la sera.**

- Elimu mjumuisho itaimarishwa kuhakikisha kuwa watoto wenye mahitaji maalum wanapata fursa sawa, vikwazo vinavyowakabili katika kujifunza vinatatuliwa na kupatiwa mahitaji yao katika kujifunza.
- Watoto wenye uzito wa kujifunza na wale wenye vipaji vya hali ya juu watatambuliwa na kuainishwa na kupewa fursa za kujifunza kutokana na kasi ya uwezo wao.
- Watoto wenye ulemavu na wengine wenye mahitaji maalumu, watachanganywa pamoja na watoto wenzao na kupatiwa elimu bora.

**4.6.2.4 Mikakati.**

- Kuwatambua watoto wenye mahitaji maalumu mapema iwezekanavyo na kutathmini mahitaji yao ya kielimu na kiafya.
- Kukuza na kuimarisha elimu kwa watoto wenye mahitaji maalumu.
- Kuandaa utararibu kwa ajili ya kusimamia ushiriki wa watu wenye ulemavu katika masuala yanayoathiri maisha yao.
- Kuanzisha vituo maalumu kwa ajili ya watoto wenye matatizo makubwa ya ulemavu.
- Kuanzisha vituo vya walimu vyenye kutoa huduma mbali mbali.
- Kutetea haki ya kupata elimu, kama haki ya msingi ya binaadamu, kwa watoto wenye mahitaji maalumu.
- Kujumuisha elimu ya wenye mahitaji maalumu katika kukuza programu za ualimu.
- Kuandaa programu maalumu kwa wanafunzi ambao ni wazito wa kujifunza na watoto wenye vipaji vya hali ya juu.
- Kuanzisha huduma za rufaa.
- Kutoa fursa za ajira kwa watoto wenye mahitaji maalumu.
- Kuanzisha uhusiano na ushirikiano mzuri na Jumuia ya Watu wenye Ulemavu, Wizara inayohusika na kusimamia maendeleo ya Vijana, Ajira, Wanawake na Watoto, Wizara inayosimamia masuala ya afya, washirika wa maendeleo na jamii kwa ujumla.

## 4.7. SKULI ZA WATU BINAFSI.

### 4.7.1 Utangulizi.

Skuli za serikali pekee hazitoshelezi kutoa elimu kwa watoto wote katika ngazi zote. Kwa hivyo mchango wa watu binafsi kama washirika muhimu katika kuleta maendeleo ya elimu hauepukiki. Kwa kawaida skuli za watu binafsi zinaanzishwa ili kukidhi mahitaji yaliyopo na

ambapo jamii ina uwezo na iko tayari kulipia gharama za elimu itolewayo. Ni nadra, kwa skuli hizo kuanzishwa kwa dhamira ya kupata maendeleo makubwa ya kielimu. Skuli za watu binafsi zinaweza kuanzisha programu za skuli zilizo huru na za ugunduzi zitakazowapelekea walimu na wanafunzi kupata maarifa mapya.

**4.7.2 Hali ya sasa.**

Skuli za watu binafsi kwa Zanzibar, zilianzishwa tena mwaka 1992. Hadi kufikia mwaka 2004, kulikuwa na skuli 157 za maandalizi zenye wanafunzi 12,078 na skuli 24 za msingi zenye wanafunzi 5,842. Kulikuwa na skuli 12 tu zenye wanafunzi 1,828 zinazotoa elimu ya sekondari. Mchango wa sekta binafsi katika kiwango cha uandikishaji kwa watoto wote ulikuwa ni asilimia 10.7 kwa ngazi ya maandalizi, asilimia 2.9 kwa ngazi ya msingi na asilimia 1.3 kwa ngazi ya sekondari ya awali ambapo kwa jumla zilichangia uandikishaji wa asilimia 2.5 katika elimu ya lazima. Hivi sasa skuli nyingi za watu binafsi zinaendeshwa na taasisi za kujitolea zisizo za kiserikali.

**4.7.2.1 Mafanikio.**

- Sekta binafsi inafanya vizuri na kwa kweli imekuwa ikichangia kuongeza fursa za kupata elimu katika ngazi zote.
- Skuli za binafsi zinafuata miongozo na mitaala inayotumika katika skuli za serikali.
- Sekta ya watu binafsi inatoa uhuru kwa wanafunzi na wazazi kuchagua programu wanazozitaka.
- Ufanisi wa ufundishaji katika skuli binafsi ni mkubwa zaidi ukilinganisha na wa skuli za serikali.
- Skuli za watu binafsi zinaonesha kuwa na ubunifu unaowavutia wanafunzi wengi zaidi.

**4.7.2.2 Mapungufu.**

- Wanafunzi wanaojiunga na skuli za binafsi ni sharti watoe ada, jambo ambalo huwanyima fursa ya elimu wale ambao hawana uwezo.
- Skuli nyingi za binafsi za sekondari hazina walimu wenye sifa ambao wamewaajiri ajira ya kudumu.
- Skuli nyingi za binafsi ziko zaidi maeneo ya mjini.
- Skuli za watu binafsi zimekuwa zikiendeshwa kwa uhuru mkubwa zaidi.
- Skuli za binafsi hazitowi fursa kwa walimu kujiendeleza.
- Walimu katika skuli za binafsi hawana usalama wa taaluma au usalama wa kazi yao.
- Skuli za binafsi hazizingatii mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu.
- Miundo mbinu katika baadhi ya skuli haikidhi viwango vinavyohitajika.

**4.7.2.3 Tamko la sera.**

- Ushirikiano na sekta binafsi katika utoaji wa elimu utahamasishwa na kuimarishwa.
- Kutakuwa na bodi ya usimamizi na ukaguzi yenye dhamana ya kusimamia skuli binafsi.

**4.7.2.4 Mikakati.**

- Kuimarisha nyanja za mawasiliano na skuli za binafsi ili kukuza ushirikiano.
- Kuzishajiisha skuli binafsi kuzingatia dhamira mahususi zilizoelezwa kwenye mfumo wa elimu.

- Kukifanyia marekebisho kitengo kinachohusika na shughuli za usimamizi na ukaguzi.
- Kuelezea aina za skuli binafsi na kuainisha majukumu na wajibu wao kwa Wizara ya elimu.
- Kushajiisha na kusimamia uwekezaji wa sekta binafsi katika ngazi zote za elimu.
- Kuwashirikisha walimu wa skuli binafsi katika kukuza progaramu za kitaaluma.
- Kuanzisha uhusiano na Mamlaka ya Kukuza Vitega uchumi Zanzibar (ZIPA), Wizara inayosimamia masuala ya Fedha na Uchumi, Vituo vya Walimu na Taasisi zisizokuwa za serikali.

## 4.8 ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA AMALI.

### 4.8.1 Utangulizi.

Matumizi ya sayansi na teknolojia ni jambo la lazima kutokana na ongezeko la mahitaji ya ujuzi wa kiufundi katika kujipatia kipato. Muendelezo wa ujuzi na mafunzo ya vitendo yanahitajika katika soko la ajira.

Njia moja wapo ya kupata wataalamu nchini ni kuwapa watu mafunzo ya ufundi na amali. Mafunzo haya ni muhimu kwani hutoa fursa kwa mtu kujiajiri.

### 4.8.2. Hali ya sasa.

Hivi sasa nchini kuna upungufu wa wataalamu wa fani ya elimu ya ufundi na mafunzo ya amali. Wakati uandikishaji katika skuli za kawaida umeongezeka maradufu katika kipindi cha miaka 10, uandikishaji katika elimu ya ufundi na mafunzo ya amali hauongezeki. Kuna taasisi kidogo sana zinazotambulika kutoa mafunzo ya aina hiyo kwa hapa Zanzibar.

Katika mwaka 2004 kulikuwa na chuo kimoja na skuli 4 ambazo zilitoa elimu ya ufundi zikiwa na jumla ya wanafunzi 700 (Hotuba ya bajeti ya mwaka 2003/4) kati ya hao wanafunzi 228 sawa na asilimia 32.6 walikuwa wanawake. Kwa kuongezea, kulikuwa na taasisi 5 zilizokuwa zikitoa elimu ya ufundi. Skuli hizi zinatoa mafunzo ya ufundi wa kijadi kama vile useremala, uhunzi, upishi, ushoni, kutandaza nyaya za umeme majumbani na uashi. Hivi karibuni fani mpya za mafunzo ya ufundi zimeanzishwa, kama vile elimu ya kompyuta, uhasibu na fedha. Pamoja na hayo, zimeanzishwa programu za elimu isiyo rasmi, ambayo inaimarisha ukuaji wa ujuzi wa kusoma, kuandika na kuhesabu, yakiwemo baadhi ya mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi vya wanawake. Hali hii imepelekea idadi ndogo tu ya wataalamu kutoka nje ya nchi.

#### 4.8.2.1 Mafanikio.

- Ufaulu mzuri wa skuli za ufundi kwenye mitihani ya taifa.
- Kuwepo kwa idara za serikali zinazosimamia mafunzo ya ufundi na elimu ya amali.
- Hakuna vikwazo vya kijinsia katika kujiunga na skuli za ufundi.
- Mipango iko mbioni kuanzisha vituo vya elimu ya amali pamoja na shughuli za uzalishaji mali.
- Kuwepo kwa rasimu ya sera ya elimu ya mafunzo ya amali.

#### 4.8.2.2 Mapungufu.

- Vigezo vya kujiunga na taasisi za elimu ya amali na ufundi haviko wazi.
- Wanafunzi hawapati uzoefu wa ujuzi wa elimu ya amali na ufundi katika ngazi yoyote ya elimu isipokuwa wale wanaoingia katika skuli za mchepuo wa ufundi.

- Mafunzo ya elimu amali hayaendani na malengo ya taifa.
- Wahitimu wanawake ni wachache wanaoajiriwa.
- Baadhi ya wanafunzi wana mawazo finyu juu ya elimu ya ufundi.
- Uhaba wa walimu, wataalamu na vifaa.
- Ufinyu wa bajeti katika sekta ya elimu ya amali.
- Kutokuwapo kwa uratibu miongoni mwa vyuo vya mafunzo ya ufundi.
- Elimu ya ufundi na amali itolewayo haikidhi mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**4.8.2.3 Tamko la sera.**

- Elimu ya ufundi na mafunzo ya amali itaandaliwa kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya soko la ajira.
- Elimu ya awali ya mafunzo ya amali na ufundi itatolewa katika ngazi ya elimu ya sekondari ya kawaida kama njia ya kuwarahisishia vijana upeo wa kuchagua fani tafauti wazitakazo
- Kutakuwa na bodi itakayokuwa na majukumu ya kusimamia, kufuatilia, kuthibitisha na kudhibiti utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya amali.
- Serikali itowe uhuru katika uanzishwaji na umiliki wa taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo ya amali.

**4.8.2.4 Mikakati.**

- Kuainisha na kukuza ujuzi unaohitajika katika kukidhi mahitaji ya soko la ajira.
- Kuviendeleza na kuvitanua vituo vya elimu ya amali na ufundi.
- Kuwapatia mafunzo walimu kwa ajili ya mafunzo ya amali na ufundi.
- Kuishirikisha jamii katika kutoa mafunzo kwa wanafunzi wapya wa elimu ya amali.
- Kuongeza bajeti ya elimu ya ufundi na amali katika ngazi ya elimu ya sekondari na elimu ya lazima.
- Kuanzisha chombo cha kitaifa kitakachosimamia maendeleo ya elimu ya amali.
- Kuwapatia fursa ya mafunzo ya ufundi na amali watoto wenye mahitaji maalumu.
- Kuanzisha ujuzi wa awali wa mafunzo ya amali katika ngazi ya elimu ya lazima.
- Kuingiza mafunzo ya TEKNOHAMA kuwa sehemu ya mafunzo ya amali.
- Kuanzisha vituo vya biashara na teknolojia ili viweze kutoa wataalamu na kukuza vituo vichanga.
- Kuanzisha karakana tafauti zenye madhumuni ya kutoa mafunzo ya amali ya awali katika skuli za sekondari.
- Kuanzisha uhusiano na Wizara inayosimamia masuala ya biashara na viwanda, mafunzo ya amali na sekta binafsi.

## 4.9 ELIMU ISIYO RASMI NA ELIMU YA WATU WAZIMA.

### 4.9.1 Utangulizi.

Elimu isiyo rasmi imeaandaliwa si kwa sababu ya kufuta ujinga tu, lakini pia kukuza ufanisi na uzalishaji. Ina nafasi kubwa katika kupunguza umaskini. Kwa vile elimu isiyo rasmi ni mafunzo endelevu, inahitaji kubadilika badilika ili kukidhi mahitaji ya wanaojifunza. Elimu hii hutolewa kupitia programu tafauti kama vile programu za kisomo, elimu ya kujiendeleza, mafunzo ya amali na elimu mbadala.

Kwa kawaida, elimu ya watu wazima hutolewa kwa watu wazima ambao kwa sababu moja au nyengine hawakupata elimu rasmi na wale ambao wangependa kukuza elimu na ujuzi wao. Elimu hii nayo, hutolewa kupitia programu tafauti zikiwemo programu za kisomo, elimu ya kujiendeleza na mafunzo ya amali.

**4.9.2 Hali ya sasa.**

Elimu ya watu wazima inatolewa na serikali na taasisi binafsi. Katika mwaka 2004 kulikuwa na vituo vya kisomo 130 vilivyoandikisha wanakisomo 7,708 kati ya hao 5,437 sawa na asilimia 70.5 ni wanawake. Elimu ya kujiendeleza inatolewa kwenye vituo 39 ambavyo zaidi viko maeneo ya mjini na vina wanafunzi 4,414 miongoni mwao 2,535 sawa na asilimia 57.4 ni wanawake. Programu nyingi za kisomo na kujiendeleza zinaendeshwa katika skuli za kawaida na walimu ambao hulipwa posho maalum.

Kwa kuongezea, kuna vituo vyengine ambavyo hutoa mafunzo ya ujuzi wa kitaalamu kama vile biashara na uhasibu, sheria, mafunzo ya ukatibu muhutasi na mafunzo ya kompyuta. Programu za mafunzo ya amali hutolewa katika vituo 74 vyenye jumla ya wanafunzi 1,520 ambapo wanafunzi wanawake ni 75 (sawa na asilimia 4.9). Programu za wanawake zinalenga kuwapatia wanawake uwezo wa kujiongezea kipato kupitia shughuli za kiuchumi. Katika mwaka 2004 kulikuwa na vituo 63 vilivyowashirikisha wanawake 1,181 katika shughuli mbali mbali kama vile ushoni, upishi, kilimo, ufinyanzi, kilimo cha mwani na biashara ndogo ndogo. Pia kuna vituo vya elimu isiyo rasmi vinavyotoa taaluma mbali mbali – kama vile ushoni na biashara. Wakati huo huo kuna vituo vichache vya amali vinavyotoa mafunzo kwa wale wenye mahitaji maalum kupitia Asasi za Kiraia.

**4.9.2.1 Mafanikio.**

- Kiwango cha kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kimeongezeka kutoka asilimia 61 mwaka 1986 (sensa ya kisomo) kufikia asilimia 73.4 mwaka 2002 ( Sensa ya Idadi ya watu na makaazi)
- Mafunzo ya elimu amali yametoa nafasi za kazi na ajira binafsi.
- Mwamko na hamu ya vijana kujiunga na vituo vya elimu amali imeongezeka.
- Kuna skuli za binafsi zimejikita kikamilifu katika elimu ya amali.
- Kuwepo kwa vituo vya elimu ya amali kwa ajili ya walemavu.

**4.9.2.2 Mapungufu.**

- Kutokuwepo kwa vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia na mishahara midogo kunaathiri kiwango cha uandikishaji.
- Programu za usomaji zinaathiriwa na uhaba wa vituo rasmi vilivyosajiliwa, uchache wa walimu wenye sifa za kitaaluma na muda wa masomo usio mwafaka kwa wanakisomo.
- Ushajihishaji mdogo kutokana na programu za kisomo kuwa dhaifu kiutendaji.
- Hakuna uratibu na usimamizi wa shughuli za elimu ya watu wazima.
- Madarasa mengi ya elimu ya kujiendeleza yako maeneo ya mjini.
- Vituo vya mafunzo ya amali vina uhaba wa zana na vifaa.
- Miradi ya wanawake ya kujiongezea kipato haina wataalamu na kukosa soko kwa bidhaa wanazozalisha.
- Programu za elimu ya watu wazima hazijatumia kikamilifu nyenzo za TEKNOHAMA.

- Hakuna vituo vya mafunzo ya amali vya umma kwa wale wenye mahitaji maalumu ya kielimu.

**4.9.2.3 Tamko la sera.**

- Elimu ya watu wazima itaimarishwa na kufanyiwa marekebisho ili iendane na mabadiliko na kukidhi mahitaji ya wanakisomo na wanajamii.
- Elimu ya watu wazima itaimarishwa, itaendeshwa na kuendelezwa kwa ushirikiano na wadau wengine.
- Programu za elimu ya kujiendeleza zitaandaliwa katika mfumo wa mafunzo endelevu ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi ya kuhitimu au kuendelea na masomo.

**4.9.2.4 Mikakati.**

- Kuhamasisha njia mbali mbali za kutolea mafunzo zitakazowawezesha wanakisomo kupata stadi za msingi na za ziada ili kufikia mahitaji ya kazi kwa makundi tafauti
- Kuasisi kampeni juu ya umuhimu wa elimu endelevu.
- Kuimarisha elimu endelevu.
- Kutoa ushauri na mafunzo yanayostahiki kwa washiriki muhimu wa programu za elimu ya watu wazima.
- Kuzitathmini upya shughuli za kujiongezea kipato zinazofanywa na wanawake ili kufikia ubora.
- Kuendeleza matumizi ya TEKNOHAMA katika kuimarisha programu za elimu ya watu wazima.
- Kuandaa taratibu kwa ajili ya kuleta ushirikiano baina ya sekta na wizara mbali mbali
- Kukuza uhusiano na muingiliano baina ya elimu rasmi na elimu ya watu wazima.

## 4.10 ELIMU MBADALA.

### 4.10.1 Utangulizi.

Elimu ya lazima ni haki ya kila mtoto ambapo serikali ina wajibu wa kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata fursa hiyo kikamilifu, sambamba na wale ambao kwa sababu moja au nyengine wameikosa au hawakuhitimu elimu hiyo kupitia mfumo wa skuli za kawaida. Waliokosa elimu ya lazima wanapaswa kupatiwa njia mbadala za kuweza kuhitimu elimu hiyo kwa utaratibu mwengine.

Kwa hivyo, fursa za elimu mbadala lazima ziwepo, ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata angalau msingi wa elimu. Inapasa kuelezea nyenzo za kielimu kwa njia ya moduli za kujifunzia na ni lazima kukuza stadi za kusoma ambazo wanakisomo walizikosa katika skuli za kawaida. Ni lazima pia iwafundishe tabia njema itakayopelekea kufikia malengo yanayohitajika katika mafunzo ya kitaaluma.

### 4.10.2 Hali ya sasa.

Watoto wengi wenye umri wa kwenda skuli hawahudhurii skuli au wameacha elimu ya lazima kutokana na sababu mbali mbali, zikiwamo uhaba wa nafasi, umbali kutoka nyumbani hadi skuli, elimu isiyo bora, mtaala usio na uhalisia, wazazi kutokuwa na mwamko juu ya umuhimu wa elimu, ndoa za mapema, ujauzito na kutoipa elimu kipaumbele. Kwa kuongezea kutokana na hali ya skuli nyingi kukabiliwa na uhaba wa nafasi za kuwaweka watoto wote wanaoandikishwa, idadi kubwa ya wanafunzi huanza skuli wakiwa na umri mkubwa; hali ambayo huwaweka katika hatari ya kuacha skuli kabla ya kumaliza elimu ya lazima. Kwa hivi sasa, asilimia 20 ya watoto

wanaopaswa kuweko skuli za msingi hawasomi na asilimia 25 wameacha kabla ya kumaliza elimu ya lazima. Watoto wengi miongoni mwa hawa hukua na ujinga wa kutojua kusoma na kuandika au wanakuwa na elimu ndogo sana kutokana na kukosa kufaidika na fursa ya elimu ya lazima kwa wote.

Programu ya elimu mbadala bado ni changa na haijaenea nchi nzima. Hadi sasa kuna vituo 13 vya elimu mbadala vyenye wanafunzi 501, miongoni mwa hao wanafunzi 102 sawa na asilimia 20.4 ni wanawake. Watoto hawa wanahudhuria elimu mbadala kwa muda wa mwaka mmoja, ambapo mafunzo yao yanaendeshwa katika skuli za kawaida lakini katika madarasa tafauti na baadaye hujumuishwa katika madarasa ya kawaida ya skuli kwa mujibu wa uwezo wake.
Programu hii bado haijazifikia jamii za vijijini ambako idadi kubwa ya watoto hawajapelekwa kabisa au wametoroka skuli mapema.

**4.10.2.1 Mafanikio.**

- Kuanzishwa madarasa ya elimu mbadala katika skuli mbali mbali.
- Baadhi ya wanafunzi katika programu hizi zilizobuniwa wamefaulu vizuri na wameteuliwa kujiunga na skuli za michepuo.
- Kuongezeka kwa mwamko na hamu ya kujiunga katika vituo vya elimu mbadala miongoni mwa vijana.

**4.10.2.2 Mapungufu.**

- Programu za elimu mbadala zimelenga zaidi katika elimu ya msingi.
- Wanafunzi waliooa au kuolewa, wajawazito na walio katika makundi hatarishi hawajafaidika na programu hizi.
- Programu hizi bado hazijatoa fursa za kutosha.
- Kutofautiana kwa uwezo miongoni mwa wanafunzi, kunapelekea ugumu katika kuwagawa wanafunzi kwa mujibu wa uwezo wao.
- Inakuwa vigumu kuwapanga wanafunzi katika ngazi mahususi wakati wanapoanza masomo.
- Hakuna mafunzo rasmi ya walimu kwa ajili ya programu hii.
- Programu inahitaji nidhamu ya hali ya juu kwa wanafunzi na wazazi.
- Uhaba wa nyenzo kwenye vituo vya mafunzo kunapunguza kujifunza kwa vitendo.
- Kuweko kwa vituo vichache vijijini kunawazuia vijana kushiriki kikamilifu.
- Uhaba wa fedha.
- Ushiriki mdogo wa Taasisi Zisizo za Kiserikali na Jumuia za Kiraia.

**4.10.2.3 Tamko la sera.**

- Programu za elimu mbadala zitaimarishwa na kukuzwa ili kuweza kutoa fursa ya elimu ya lazima na mafunzo ya awali ya elimu ya amali kwa lengo la kukidhi mahitaji ya wanafunzi ambao hawakufaidika na mfumo wa elimu rasmi.
- Serikali itatoa motisha kwa Taasisi zisizo za kiserikali na Asasi za Kiraia kuanzisha na kusimamia programu za elimu mbadala kwa vijana na watoto ambao hawako skuli.

**4.10.2.4 Mikakati.**

- Kuandaa programu mbali mbali za elimu mbadala.
- Kuandaa mtaala utakaomlenga mwanafunzi.
- Kuwapatia mafunzo walimu na wale wanaojitolea ili kuunga mkono programu za elimu mbadala.

- Kutetea uwepo wa programu za elimu mbadala kufika kwenye jamii za vijijini.
- Kuanzisha skuli za elimu mbadala zilizo karibu na wanavijiji.
- Kujumuisha stadi za maisha na mafunzo ya ufundi katika mtaala.
- Kuweka ushirikiano wa karibu baina ya Serikali, Taasisi zisizo za Kiserikali na Jumuiya za Kiraia katika suala la kutoa elimu.
- Kuanzisha uhusiano baina ya Taasisi zisizo za Kiserikali, Jumuia za Kiraia, kamati za skuli na jamii.

## SURA YA TANO
## UBORA WA ELIMU

### 5.0 UTANGULIZI.

Nchi nyingi za Afrika zimeshuhudia idadi kubwa ya uandikishaji wa wanafunzi usioendana na mabadiliko ya ubora wa elimu. Hali hii imesababisha kuanguka kwa ubora wa elimu. Hata hivyo, katika hali ya mazingira magumu upo uwezekano wa kubuni mikakati kwa gharama nafuu itakayoinua ubora wa elimu bila ya kuathiri uandikishaji au usawa katika elimu. Mpango wa Utekelezaji wa Mkutano uliofanyika Dakar umeeleza kwamba elimu inayotolewa lazima ikuze vipaji na uwezo wa wanafunzi, mienendo yao ili waweze kukuza maendeleo yao binafsi na kuleta mabadiliko kwenye jamii zao. Swali la msingi ni aina gani ya maarifa, ujuzi, uwezo au maadili ambayo mwanafunzi atayapata na yataweza kumsaidia katika kumnufaisha yeye binafsi na jamii yake. Hii inahitaji uchambuzi wa kina wa mitaala, mitihani, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na mbinu bora za ufundishaji, lugha ya kufundishia na mazingira mazuri ya kujifunzia. Kwa kuongezea lazima kuwe na tathmini ya uhakika yenye kupima matokeo ya elimu.

### 5.1 MITAALA.

#### 5.1.1 Utangulizi.

Mitaala ni kipengele muhimu kinachochangia ubora wa elimu. Mtaala uliotayarishwa vizuri, wenye uwiano na uhalisia, lazima uwape wanafunzi ujuzi, maarifa na mwelekeo sahihi. Mtaala usioendana na uhalisia hasa katika ngazi ya chini ya elimu unawaathiri wanafunzi kwa kujifunza tamaduni za kigeni ambazo haziendani na malengo ya mfumo wa maisha.

#### 5.1.2 Hali ya sasa.

Mitaala ya elimu ya msingi kwa Zanzibar inatayarishwa na Wizara ya Elimu kupitia Kitengo cha Kukuza Mitaala na hutumika katika skuli za serikali na binafsi. Mitaala katika ngazi ya Sekondari za Tanzania inatayarishwa na Taasisi ya Elimu Tanzania. Tathmini ya hivi karibuni inaonesha kuwa mitaala ina idadi kubwa ya masomo na mada katika ngazi zote. Hii inapelekea baadhi ya mada kutosomeshwa kwa undani na kuwanyima wanafunzi muda wa kuweza kujisomea wenyewe, pia njia za kufundishia zimeathirika kwa kiasi kikubwa.

##### 5.1.2.1 Mafanikio.

- Kuwepo kwa kitengo cha Mitaala katika Wizara ya Elimu.
- Mitaala katika ngazi ya msingi imetayarishwa kulingana na mazingizra.

##### 5.1.2.2 Mapungufu.

- Mitaala ina idadi kubwa ya masomo na mada katika ngazi zote.
- Kukosekana vigezo muafaka vya ufaulu vitavyomruhusu mwanafunzi kuvifikia kabla ya kuingia katika ngazi nyengine ya elimu.
- Mtaala umeegemea zaidi katika ujuzi wa ufahamu na kuacha ujuzi mwengine.
- Walimu huwa hawamalizi mitaala kwa sababu skuli huingiliwa na shughuli nyengine zinazoathiri utendaji wake na kuwepo kwa utaratibu wa shifti mbili.
- Marekebisho ya mitaala haiendani na matayarisho ya mwalimu na uandaaji wa vitabu vya kusomea.
- Mtaala wa sekondari hauzingatii maarifa na ujuzi unaopatikana kutoka katika mtaala wa ngazi ya elimu ya msingi wa Zanzibar.

- Mtaala hauna mawanda mapana na umekosa fani mbadala kwa wanafunzi wasio kuwa wana taaluma au wana nadharia.

**5.1.2.3 Tamko la Sera.**

- Kuanzishwe taasisi ya mitaala yenye mamlaka ya kutayarisha, kupitia na kuandaa upya mitaala ya elimu ya maandalizi, msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, vyuo vya elimu baada ya sekondari na mafunzo ya elimu isiyo rasmin.
- Kuwepo na muongozo utakaoelekeza muda wa kusomesha kwa ngazi zote za elimu ambao ni lazima ufuatwe.

**5.1.2.4 Mikakati.**

- Kuupitia upya mtaala na kuurekebisha.
- Kubainisha masomo na muda (saa) wa kusomesha katika kila ngazi ya elimu.
- Kuanzisha Taasisi ya Ukuzaji Mitaala.
- Kutayarisha vigezo vya kupima ubora wa elimu katika kila ngazi.
- Kuweka viwango vya orodha ya vitabu kwa wanafunzi wa ngazi tafauti za elimu.
- Kutayarisha mtaala wenye mawanda mapana.
- Kuanzisha uhusiano na vituo vya walimu, bodi za mitihani, Taasisi ya Elimu Tanzania na sekta binafsi.

## 5.2 MITIHANI.

### 5.2.1 Utangulizi.

Mitihani inatathmini hali halisi ya ufundishaji na kujifunza na inatoa taswira ya kilichosomeshwa na namna kilivyosomeshwa. Kwa maana nyengine mitihani inafuatilia, inatathmini na inachochea kufikiwa kwa dhamira na malengo ya elimu. Kwa kuongezea mitihani inaweza kuwa chombo imara cha kuhakikisha ufanisi katika kujifunza. Hata hivyo matokeo mabaya ya mtihani hupunguza muamko wa kufikia malengo ya juu ya elimu.

### 5.2.2 Hali ya sasa.

Kwa sasa mitihani inatumika katika kuchagua wanafunzi watakaoendelea na masomo katika ngazi nyengine ya juu ya elimu. Mitihani huchuja wanafunzi au huwaweka katika daraja wanalostahiki na haitoi tathmini kamili ya mafanikio ya malengo ya mitaala. Tanzania kuna bodi mbili zinazoshughulikia mitihani ambazo ni Divisheni ya Mitihani ya Zanzibar na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA). Divisheni ya Mitihani ya Zanzibar hushughulikia mitihani ya ndani ya darasa la saba na kidato cha pili na mitihani ya ualimu (isiyotahiniwa na NECTA). Kwa upande wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) wanasimamia mitihani ya kidato cha nne na cha sita. Hata hivyo Divisheni ya Mitihani ya Zanzibar imekosa wataalamu wa masuala ya mitihani. Tathmini ya matokeo ya mitihani ya skuli za sekondari inategemea alama zitokanazo na tathmini ya darasani na mtihani wa mwisho. Hata hivyo, dhana ya tathmini ya darasani haijaeleweka vyema.

**5.2.2.1 Mafanikio.**

- Kuwepo kwa divisheni inayoshughulikia masuala ya mitihani.

**5.2.2.2 Mapungufu.**

- Mitihani inapima zaidi ujuzi katika mfumo wa uandishi na kupuuza ujuzi mwengine ambao hauwezi kupimwa kwa maandishi.

- Mitihani ya ndani inahamasisha wanafunzi kukariri kwani hupima zaidi uwezo wa kukariri na utambuzi wa maarifa.
- Haizingatii kupima mtiririko wa ujuzi kama vile taaluma za uchambuzi, matumizi, uunganishi na tathmini.

**5.2.2.3 Tamko la Sera.**

- Kuanzishwe chombo kitakachotunga, kusimamia na kuendesha mitihani kwa elimu rasmi na elimu ya watu wazima Zanzibar.
- Chombo cha mitihani kitakuwa na jukumu la kutoa vyeti kwa mitihani ya elimu rasmi na kuweka uwiano baina ya taaluma zitolewazo.

**5.2.2.4 Mikakati.**

- Kutayarisha majaribio yatakayopima ujuzi wa wanafunzi katika ngazi mbali mbali.
- Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa bodi ya mitihani katika shughuli zote za mitihani.
- Kufanya mapitio ya mchakato mzima wa kutathmini wanafunzi.
- Kutathmini ufaulu wa wanafunzi katika ngazi mbali mbali za elimu kabla ya kumaliza elimu ya lazima
- Kuanzisha njia nyengine za upimaji wa uwezo wa mwanafunzi kama SACMEQ na MLA na kuzifanya ni njia rasmin.
- Kuanzisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kuimarisha shughuli za mitihani.
- Kutayarisha mitihani inayoendana na wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
- Kuanzisha uhusiano wa karibu na Baraza la Mitihani la Taifa, Taasisi ya Elimu ya Tanzania, Kitengo cha Mitaala, Bodi za mitihani za Kitaifa na za Kimataifa.

## 5.3 VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA.

**5.3.1 Utangulizi.**

Vifaa vya kufundishia na kujifunzia ni nyenzo muhimu katika utekelezaji wa mtaala na utoaji wa elimu bora. Vifaa lazima viwe na uhalisia, toshelevu na vinavyofaa kulingana na hali ya jamii, vyenye gharama nafuu na viweze kupatikana kwa walimu na wanafunzi. Vifaa vya kufundishia na kujifunzia lazima vitayarishwe ili viweze kuibua hamu ya mwanafunzi kujifunza. Kwa kuongezea ubora wa elimu unajumuisha ushirikishwaji wa wanafunzi katika matumizi ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

**5.3.2 Hali ya sasa.**

Kwa sasa Wizara imetoa vitabu vya kiada kwa madarasa mengi ya msingi. Kutokana na uhaba wa fedha, kuna upungufu mkubwa wa vifaa vya kujifunzia katika ngazi zote za elimu hususan katika ngazi ya sekondari. Jitihada zinaendelea kufanyika kukabili hali hii kwa kupitia programu ya Kuimarisha Ubora wa Elimu (EQUIP) na kwa kuanzisha vifaa mbadala vya kufundishia na kujifunzia vinavyopatikana katika mazingira halisi na mitandao ya intaneti. Pamoja na jitihada hizo walimu wengi si wabunifu na wanakosa taaluma ya ziada ya kutumia ujuzi wake.

**5.3.2.1 Mafanikio.**

- Baadhi ya skuli za msingi zimepatiwa vitabu vya kiada, jitihada zinaendelea kuhakikisha kuwa madarasa mengine yanapatiwa vitabu ili kufikia lengo la kugawa kitabu kimoja kwa kila mwanafunzi.

- Waandishi wazawa wameanza kuandika vitabu ambavyo vinaweza kutumika kama vitabu vya ziada kwa kila skuli.
- Vituo vya Walimu vinachangia kutoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na utoaji wa vifaa vyengine.

#### 5.3.2.2 Mapungufu.

- Ukosefu mkubwa wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika skuli.
- Utegemezi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kutoka nchi za nje.
- Uhaba wa vifaa vya ziada vya kufundishia vinavyo hitajika kwa kujifunzia.
- Hakuna motisha inayotolewa kwa walimu wenye bidii na wabunifu.
- Uingizaji wa vifaa vya kufundishia visivyofaa na visivyoendana na mazingira.

#### 5.3.2.3 Tamko la Sera.

- Wataalamu wa ndani wenye vipaji vya kutayarisha vifaa vya kufundishia kwa kutumia rasilimali zilizopo watahamasishwa na kupewa motisha ili watayarishe vifaa vyenye uhalisia vitakavyoendana na mazingira halisia.
- Ianzishwe bodi itakayohakiki na kuthibitisha ubora wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.
- Utengenezaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia uwe huru ili uweze kuwavutia waandishi zaidi wa kujitegemea.
- Teknolojia ya Habari na Mawasiliano itumike katika utoaji fursa sawa katika rasilimali za elimu.
- Kuwe na Sera ya Vitabu.

#### 5.3.2.4 Mikakati.

- Kushajiisha na kusimamia utayarishaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa kutumia rasilimali zilizopo.
- Kuwaandaa walimu kuwa wabunifu na kuwapa taaluma kwa kutumia rasilimali zilizopo.
- Kushajiisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kama chanzo muhimu cha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.
- Kuwepo na usawa katika matumizi ya vitabu ili kuhamasisha na kukuza utumiaji wa vifaa mbali mbali vya kufundishia na kujifunzia.
- Kuanzisha Bodi itakayokuwa na jukumu la kuchagua na kuthibitisha matumizi ya vitabu vya kiada na ziada.
- Kushajiisha matumizi sahihi na utengenezaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.
- Kuanzisha uhusiano na Taasisi ya Elimu ya Tanzania (TIE), wachapishaji wa vitabu, waandishi, maktaba za kitaifa na kimataifa, vyama vya walimu na taasisi zisizo za kiserikali.

## 5.4 MAKTABA.

### 5.4.1 Utangulizi.

Utamaduni wa kusoma unatoa nafasi kubwa kwa msomaji kujifunza kwa kujitegemea, kutafuta taarifa, kukuza ufahamu na kupata ujuzi wa utafiti. Maktaba inayofanya kazi vizuri na yenye vitabu vya kutosha, inatoa fursa nzuri ya kukuza ujuzi na ufahamu kwa jamii au katika ngazi ya Taifa. Maktaba pia inaweza kuimarishwa kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili

kumuwezesha msomaji kupata elimu na taarifa mbali mbali za kiulimwengu. Jambo hili lina umuhimu mkubwa katika kuimarisha ufundishaji na kupunguza kusoma kwa kukariri.

**5.4.2 Hali ya sasa.**

Skuli nyingi za Zanzibar hazina maktaba ya darasani au hata ya skuli. Hata hizo skuli chache zenye maktaba zina tatizo kubwa la upungufu wa vitabu, majarida na magazeti yenye uhalisia na yanayoendana na wakati. Zipo maktaba katika vituo vya walimu, ambapo walimu wanaweza kupata baadhi ya vitabu. Mpaka sasa kuna maktaba kuu mbili tu, moja Unguja na moja Pemba. Maktaba nyengine ziko katika vyuo vikuu na baadhi ya taasisi za serikali na binafsi. Kuna mipango ya kuanzisha vituo vya hifadhi za nyaraka katika kila Wizara. Baadhi ya maktaba zina vitabu visivyotosheleza na vilivyopitwa na wakati. Pia kuna uhaba wa utoaji wa huduma nyengine za maktaba kama vile vinasa sauti, mikanda ya video, redio na televisheni.

**5.4.2.1 Mafanikio.**

- Kuanzishwa maktaba katika vituo vya walimu ambazo zitakuwa ndizo chanzo muhimu cha upatikanaji wa zana za kujifunza na kufundishia kwa walimu na walimu wanafunzi.
- Wasomaji wanaweza kutumia vifaa vya maktaba ya Taasisi nyengine.
- Kumeongezeka muamko katika skuli juu ya haja na umuhimu wa kuanzisha Maktaba.
- Maktaba za kitaifa zina uhusiano wa kiuanachama na jumuia za maktaba za kimataifa na Shirika la msaada wa vitabu la kimataifa.
- Maktaba za kitaifa zinaendesha programu za kila wiki kuwasaidia watoto jinsi ya kutumia maktaba.

**5.4.2.2 Mapungufu.**

- Hakuna maktaba za jamii vijijini.
- Uhaba wa vitabu.
- Hakuna utamaduni wa kujisomea.
- Upungufu wa wakutubi waliosomea.
- Hakuna kumbukumbu ya vifaa vilivyotayarishwa kwa kutumia rasilimali za ndani.
- Ukosefu wa vifaaa vya elektroniki.
- Hakuna utayari kwa wanasiasa katika kuziendeleza maktaba.
- Kutokuwepo kwa umoja na ushirikiano mzuri katika maktaba za ndani.
- Uhaba wa rasilimali.

**5.4.2.3 Tamko la sera.**

- Maktaba kuu iwe ndio kituo kikuu cha Taifa cha upatikanaji wa taarifa na kitakua na jukumu la kuziendeleza maktaba za skuli na za kijamii
- Kila skuli iwe na maktaba au kituo chenye vitabu vya kutosha na wakutubi waliosomea.

**5.4.2.4 Mikakati.**

- Kufufua maktaba za skuli na za darasani.
- Kushajiisha jamii kujenga maktaba na kuanzisha utamaduni wa kujisomea.
- Kufufua maktaba za kuhamahama na za jamii.
- Kuhamasisha uanzishwaji wa maktaba binafsi.
- Kutanua na kuimarisha maktaba kuu.

- Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa maktaba.
- Kuanzisha mfumo wa uwekaji kumbukumbu za vifaa vyote vinavyotayarishwa Zanzibar na Wazanzibari.
- Kukuza utumiaji wa Teknolojia ya Habari na mawasiliano ili kurahisisha upatikanaji wa vifaaa vya kusomea.
- Kuzipitia upya taratibu za kisheria za huduma za maktaba.
- Kuanzisha uhusiano zaidi na baadhi ya jumuia za maktaba za Kimataifa, skuli, taasisi binafsi na jumuia zisizo za kiserikali.

## 5.5 MAABARA ZA SKULI.

### 5.5.1 Utangulizi.

Utafiti wa kimaabara unaimarisha na kuamsha ari ya kujifunza na kudadisi kwa mwanafunzi. Maabara ni sehemu muhimu ambayo shughuli zote za majaribio ya kisayansi na ufafanuzi hufanyika. Usomeshaji bora wa sayansi lazima upelekee uzoefu wa kazi za vitendo.

### 5.5.2 Hali ya sasa.

Zanzibar kuna skuli chache zenye maabara za sayansi ambazo pia zinakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi wenye taaluma za maabara, uhaba wa vifaa, kemikali na vifaa vya usalama. Kutokana na uhaba wa maabara zenye vifaa vya kutosha, Zanzibar imeanzisha kambi za sayansi zinazotoa njia mbadala za mafunzo ya sayansi. Mafunzo na uzoefu unaopatikana kwenye kambi hizi unazisaidia skuli. Baadhi ya vifaa vya sayansi na kemikali vimenunuliwa kwa msaada wa washirika wa maendeleo na kusambazwa skuli. Kwa kiasi fulani upatikanaji wa vifaa umehamasisha skuli zenyewe kujenga maabara.

#### 5.5.2.1 Mafanikio.

- Skuli nyingi zina vyumba ambavyo vinaweza kubadilishwa na kuwa maabara.

#### 5.5.2.2 Mapungufu.

- Ukosefu wa vifaa vya sayansi, kemikali, vifaa vya usalama na vifaa vyengine muhimu.
- Uhaba wa wasaidizi na mafundi wa maabara waliosomea.
- Maabara nyingi haziko katika mazingira mazuri ya kufundishia sayansi.

#### 5.5.2.3 Tamko la sera.

- Kuwe na maabara zenye vifaa vya sayansi vya kutosha, wasimamizi au mafundi wa maabara waliosomea katika kila skuli.

#### 5.5.2.4 Mikakati.

- Kuzipatia vifaa na kuziimarisha maabara za skuli.
- Kuzihuisha kambi za sayansi.
- Kuwapatia mafunzo wasaidizi na mafundi wa maabara.
- Kuweka vigezo vya mahitaji ya vifaa na usalama kwa maabara za skuli.
- Kuzifanya maabara ziweze kutumika kwa wote.
- Kuanzisha uhusiano na jumuia zinazosaidia usomeshaji wa sayansi, huduma za majanga ya moto, Idara za hali ya hewa, kilimo, uvuvi, vituo vya hali ya hewa na vyenginevyo.

## 5.6 SAYANSI NA TEKNOLOJIA.

### 5.6.1 Utangulizi.

Sayansi na Teknolojia inaathari kubwa kwa kizazi cha sasa kuliko kwa kilichopita. Mafanikio ya Sayansi yanaendelea kukuza elimu kwa haraka zaidi na kutowa mchango katika maendeleo ya mfumo wa teknolojia ambao kwa kiasi kikubwa unaathiri mfumo wetu wa maisha na wa kazi.

Sayansi na teknolojia ina mchango katika kuzalisha wataalamu na kuinua uchumi. Usomeshaji mzuri wa sayansi, hisabati na teknolojia unakuza uchambuzi yakinifu kama vile kufikiri kwa kina na kutoa maamuzi stahiki. Wanafunzi wanahitaji kupatiwa ujuzi huu kupitia majaribio, uchunguzi na kwenye utatuzi wa tatizo.

### 5.6.2 Hali ya sasa.

Kwa sasa, usomaji na usomeshaji wa sayansi unakumbwa na uhaba wa vifaa pamoja na uhaba wa walimu wenye sifa. Usomeshaji wa sayansi unawarejesha nyuma wanafunzi kadiri siku zinavyokwenda. Wanajamii wamekosa mwamko juu ya umuhimu wa sayansi, kwani hawaoni uhusiano uliopo baina ya sayansi na maisha yao ya kila siku. Teknolojia kama matokeo ya sayansi haijaeleweka vizuri na hivyo haifafanuliwi kwa usahihi katika skuli. Mazingira ya kufundishia na kujifunzia sayansi, teknolojia na hisabati si ya kuridhisha.

#### 5.6.2.1 Mafanikio.

- Kukuza programu ya mafunzo ya walimu na kuwaendeleza walimu wa sayansi.
- Vijana hupendezewa na masomo ya sayansi.
- Kuna motisha maalum kwa walimu wa sayansi.
- Matumizi ya teknolojia yanaongezeka katika maisha ya kila siku.

#### 5.6.2.2 Mapungufu.

- Uhaba wa fedha unakwamisha maendeleo ya sayansi na teknolojia.
- Kutokuwepo kwa mazingira mazuri ya kufundishia /kujifunza sayansi.

#### 5.6.2.3 Tamko la sera.

- Sayansi na teknolojia itakua ni kipengele cha lazima katika mfumo mzima wa elimu.
- Kuanzishwe programu maalum ili kukuza ufundishaji na kujifunza sayansi, hisabati na teknolojia.
- Sayansi na teknolojia itarahisishwa na kuoanishwa na ukuaji wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

#### 5.6.2.4 Mikakati.

- Kuanzisha skuli za sayansi za mfano.
- Kuifanya sayansi na teknolojia yenye uhalisia na kivitendo zaidi.
- Kuanzisha vituo maalum vya sayansi kwa ajili ya kuwavutia wanafunzi wenye vipaji maalum.
- Kuwazawadia wanafunzi waliofaulu vizuri masomo ya sayansi.
- Kuhamasisha klabu za sayansi zenye kufaa na kukubalika.
- Kuchukua hatua za makusudi katika kuhamasisha ushiriki wa wanawake kwenye masomo ya sayansi, hisabati na teknolojia.
- Kutoa mafunzo ya kutosha pamoja na motisha kwa walimu wa sayansi, hisabati na teknolojia.

- Kurahisisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika ukuzaji wa sayansi, hisabati na teknolojia.
- Kuanzisha programu za kutosha na zinazoendana na wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
- Kuanzisha uhusiano na wizara husika, taasisi, kamisheni zinazohusiana na sayansi na teknolojia pamoja na mashirika yenye kukuza na kuendeleza sayansi.

## 5.7 TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (ICT).

### 5.7.1 Utangulizi.

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inarahisisha mawasiliano ndani na nje ya nchi. Maendeleo ya hivi karibuni ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yamefungua njia mpya ya ufundishaji, uwasilishaji wa maarifa, kuleta ufanisi katika utowaji huduma za uongozi wa elimu.Teknolojia ya Habari na Mawasiliano pia imekuza kuwepo kwa huduma za maktaba na kukuza uwezo wa watu kujisomea.

### 5.7.2 Hali ya sasa.

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano imeanzishwa katika taasisi za elimu hivi karibuni. Hadi sasa kuna skuli 12 zenye fursa ya kutumia kompyuta, lakini hazitumiki kwa ufanisi katika kufundishia na kujifunzia. Somo la sayansi ya kompyuta hutolewa katika skuli mbili za sekondari ambazo wanafunzi wake hutahiniwa. Kompyuta nyingi zilizopo skuli ni za kizamani na zaidi hutumika kwa masuala ya kiutawala. Huduma ya mtandao wa intaneti haipatikani isipokuwa katika skuli mbili. Ingawa vituo vingi vya walimu vina kompyuta, bado walimu hawazitumii ipasavyo. Vifaa vyengine vya TEKNOHAMA kama vile projekta, televisheni, skana, redio na vyenginevyo vinapatikana katika skuli chache za sekondari ya juu na vyuo. TEKNOHAMA katika Wizara haitumiki kikamilifu katika kukuza ufanisi wa utendaji wa kazi za kila siku.

#### 5.7.2.1 Mafanikio.

- Kuwepo kwa mfumo wa mawasiliano unaofanya kazi
- Kuongezeka kwa Taasisi binafsi zinazotoa huduma na fursa ya mafunzo ya kompyuta.
- Kuongezeka kwa uelewa wa matumizi ya kompyuta kwa walimu.
- Kuwepo kwa mtaala wa somo la sayansi ya kompyuta.
- Kuenea kwa matumizi ya kompyuta kwenye maeneo ya kazi.

#### 5.7.2.2 Mapungufu.

- Kompyuta nyingi ni za kizamani.
- Skuli zinashindwa kutumia fursa za maendeleo yaliyopo ya TEKNOHAMA yaliyoibuka hivi karibuni.
- Athari za TEKNOHAMA na utandawazi hazijafahamika vizuri.
- Mchango wa TEKNOHAMA katika kukuza elimu bado ni mdogo.
- Kutokuwepo kwa matengenezo na ukarabati unaofaa wa kompyuta na vifaa vyengine vinavyoshabihiana.
- Matumizi mabaya ya huduma ya mtandao kwa watoto na vijana.
- Uhaba wa walimu waliosomea na mafundi.
- Kutokuwepo kwa sera ya taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

#### 5.7.2.3 Tamko la sera.

- Teknolojia ya Habari na Mawasiliano itaimarishwa kwa matumizi ya kiofisi na mtandao.
- Somo la kompyuta litaanzishwa katika skuli, vyuo na kwenye taasisi nyengine za elimu.
- Matumizi ya mfumo shirikishi wa TEKNOHAMA utatumika katika kutoa elimu endelevu wakati wowote na pahala popote.

#### 5.7.2.4 Mikakati.

- Kutoa mafunzo na kuendeleza taaluma ya walimu katika TEKNOHAMA.
- Kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.
- Kuimarisha mtandao baina ya Wizara, Idara na Taasisi nyengine pamoja na kuziunganisha na mataifa ya nje.
- Kuanzisha mafunzo ya kompyuta kwa uchache skuli moja ya sekondari kwa kila Wilaya.
- Utumiaji wa vifaa vya TEKNOHAMA katika kufundishia na kuimarisha uongozi wa elimu.
- Kuvipatia vituo vya walimu vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.
- Kuanzisha uhusiano na watoa huduma za mtandao, maktaba kuu, Chuo cha ualimu pamoja na mashirika ya kimataifa.

## 5.8 LUGHA YA KUFUNDISHIA.

### 5.8.1 Utangulizi.

Lugha ni zana muhimu katika mchakato wa kujifunzia. Wataalamu wa elimu wameonesha kuwa lugha ya kufundishia ina umuhimu mkubwa kwani ni chombo cha kufikishia elimu. Utafiti na uzoefu umeonesha kuwa matumizi ya lugha mama kama lugha ya kufundishia inakuza ufahamu na makuzi ya kiakili ya mtoto. Mara nyingi lugha ya kufundishia hususan katika ngazi ya elimu ya juu inaweza kuwa ni tafauti na lugha mama.

### 5.8.2 Hali ya sasa.

Kwa Zanzibar, lugha ya Kiswahili hutumika kufundishia katika ngazi ya elimu ya msingi na lugha ya Kiingereza hutumika kufundishia katika ngazi ya elimu ya sekondari pamoja na elimu ya juu. Jitihada mbali mbali zimefanyika katika kukuza ujuzi wa lugha hususan lugha ya Kiingereza.

Miongoni mwa jitihada hizo ni kuanzishwa kwa somo la Kiingereza darasa la kwanza na kufunguliwa kwa darasa la matayarisho la sekondari ambalo limelenga kuinua uwezo wa wanafunzi katika lugha ya Kiingereza.

#### 5.8.2.1 Mafanikio.

- Kuwepo kwa Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni pamoja na Baraza la Kiswahii la Zanzibar.
- Kiswahili ni lugha ya Taifa na lugha rasmi.
- Kiingereza kinatumika zaidi kwenye biashara na utalii.

#### 5.8.2.2 Mapungufu.

- Ufanisi wa darasa la matayarisho la kuingia sekondari kama njia ya marekebisho sio mzuri.
- Kuna uhaba wa vitabu vya ziada kwa walimu na wanafunzi kwa masomo ya Kiswahili na Kiingereza.
- Kutokuwepo kwa mbinu bora za kufundishia lugha.
- Uhaba wa walimu wenye sifa katika fani ya lugha.
- Uhaba wa maabara za lugha na vifaa vyenginevyo.

#### 5.8.2.3 Tamko la Sera.

- Kiswahili kitaendelea kutumika kama lugha ya kufundishia katika skuli za serikali kwa ngazi ya maandalizi na msingi isipokua lugha ya Kiingereza itatumika kufundishia masomo ya hisabati na sayansi kuanzia darasa la tano.
- Lugha ya Kiingereza itaendelea kutumika kama lugha ya kufundishia kwa ngazi ya elimu baada ya msingi isipokua kwenye masomo ya Dini.
- Kiswahili kitakua ni somo la lazima kuanzia ngazi ya maandalizi mpaka sekondari (kidato cha nne).
- Skuli za binafsi zitaomba ridhaa ya kutumia lugha nyengine kama lugha za kufundishia.
- Lugha ya Kiswahili na Kiingereza zitatumika katika kutoa mafunzo ya ujuzi wa mawasiliano katika mfumo mzima wa elimu.

#### 5.8.2.4 Mikakati.

- Lugha ya Kiingereza itaanza kufundishwa katika ngazi ya awali.
- Kuchukua hatua za makusudi za kukuza lugha ya Kiswahili na Kiingereza.
- Kuimarisha mafunzo ya mbinu za kufundishia lugha.
- Kufundisha lugha za alama kama lugha ya kufundishia watu wenye ulemavu wa kusikia.
- Kuendeleza uwezo wa walimu katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.
- Kuanzisha uhusiano na Mabaraza, Taasisi na Mashirika yanayoshughulikia lugha.

## 5.9 UTEUZI WA LUGHA.

### 5.9.1 Utangulizi.

Kujifunza lugha tofauti hukuza na kutanua maingiliano ya tamaduni tafauti. Kwa Zanzibar, Kiswahili ni lugha ya Taifa na ni lugha rasmi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inadhamira ya dhati ya kuimarisha Kiswahili kama lugha ya Taifa. Ukuaji wa sekta ya utalii, utandawazi, uchumi wa soko huria unalazimisha watu wengi kujifunza lugha nyengine zaidi.

### 5.9.2. Hali ya sasa.

Kiingereza na Kiarabu kinasomeshwa katika ngazi ya msingi na sekondari. Lugha ya Kifaransa husomeshwa kwa baadhi ya skuli za sekondari. Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar, ambayo kwa sasa ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar inatoa kozi katika ngazi ya diploma za lugha ya Kiingereza, Kiarabu, Kifaransa, Kihispania, Kireno na Kijerumani. Kwa bahati mbaya ukosefu wa maabara za kufundishia lugha na zana nyenginezo, hupelekea ufundishaji wa lugha hizi kuwa mgumu na kukosa ufanisi.

#### 5.9.2.1 Mafanikio.

- Kuwepo kwa taasisi inayofundisha lugha za kigeni.
- Kuwepo kwa fursa za ajira kwa wanaozungumza zaidi ya lugha moja.

#### 5.9.2.2 Mapungufu.

- Taasisi nyingi zinazofundisha lugha za kigeni, isipokuwa Kiarabu na Kiingereza, ziko maeneo ya mjini.
- Kuna uhaba wa walimu wa lugha wenye sifa.

#### 5.9.2.3 Tamko la Sera.

- Lugha za kigeni zitaendelea kutolewa katika ngazi tafauti kulingana na mahitaji ya kiuchumi ya wasomaji.

#### 5.9.2.4 Mikakati.

- Kuhamasisha skuli binafsi kusomesha lugha za kigeni
- Kuanzisha maabara za lugha.
- Kuimarisha matumizi ya vyombo vya mawasiliano katika kufundisha lugha za kigeni.
- Kuhamasisha mabadilishano ya zana za kujifunzia lugha na Taasisi nyengine zinazofundisha lugha.
- Kuanzisha ushirikiano na Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), vyuo vya ualimu, Kitengo cha Ukuzaji Mitaala na Taasisi nyenginezo.

## 5.10 UTAMADUNI.

### 5.10.1 Utangulizi.

Urithi wa utamaduni wenye kushikika na usioshikika umetambulikana kuwa ni kitu muhimu kinacholitambulisha Taifa, kukuza ubunifu na kulinda tamaduni tafauti. Hivyo basi, ubora wa elimu unahimiza programu zinazoheshimu wanajamii na utamaduni wao. Kwa maneno mengine, elimu lazima izingatie umuhimu wa utamaduni katika kumjenga mwanafunzi kimaadili, kimwili, kiakili na kihamasa. Ni vyema ieleweke kwamba elimu ni lazima ipelekee kujitambua na kumuwezesha mwanajamii kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa.

### 5.10.2 Hali ya Sasa.

Utamaduni wa Zanzibar umefungamana na imani kubwa za Dini tafauti, lugha moja, jadi, maadili na mila. Mitaala ya skuli imeingiza vipengele vichache sana vya utamaduni. Watoto wengi hawafahamu nchi yao na utajiri wa urithi wa utamaduni. Uelewa mdogo wa dhana ya utamaduni umepelekea kukuzwa kwa vipengele vichache tu vya utamaduni kama vile ngoma na nyimbo, navyo vimekuwa havitumiki kwa malengo ya kielimu. Skuli hazina programu zilizopangiliwa vizuri ambazo zingeweza kutumia fursa ya utajiri wa utamaduni wa Zanzibar katika kuimarisha elimu. Hata hivyo, kuna baadhi ya shughuli za utamaduni zisizo rasmin zinazofanyika kama vile baadhi ya skuli kutembelea maeneo ya kihistoria.

#### 5.10.2.1 Mafanikio.

- Kuwepo kwa Idara ya Utamaduni na Idara ya Nyaraka na Mambo ya Kale.
- Kutambua utamaduni kama alama ya utambulisho wa Taifa.
- Kuimarika kwa maingiliano ya kijamii kutokana na matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano.
- Kuimarika kwa utambulisho wa Kitaifa kwa kutumia lugha, mavazi, mila na desturi.

- Kuongezeka kwa safari za wanafunzi na wanajamii kutembelea maeneo ya kihistoria hususan makumbusho na kushiriki kwenye sanaa.

#### 5.10.2.2 Mapungufu.

- Shughuli za utamaduni katika skuli bado hazijapangiliwa vizuri.
- Vipengele muhimu vya utamaduni havijatumika ipasavyo katika kutoa elimu.
- Vipaji vya utamaduni bado havijatambuliwa na kuendelezwa.

#### 5.10.2.3 Tamko la Sera.

- Utajiri wa urithi wa utamaduni wa taifa wenye kushikika, wa masimulizi na usioshikika utatambuliwa na kujumuishwa katika mtaala wa skuli.

#### 5.10.2.4 Mikakati.

- Kuingiza vipengele muhimu vya utamaduni wa Zanzibar katika maudhui ya mitaala.
- Kupanga na kuendeleza shughuli za utamaduni ili ziweze kuchangia kikamilifu maendeleo ya wanafunzi.
- Kuimarisha na kushajiisha wanafunzi kutumia rasilimali zilizopo kama vile makumbusho, nyaraka na maktaba.
- Skuli kutoa nafasi kwa ajili ya kuhifadhi utamaduni na kufanya sanaa za maonesho.
- Kuhamasisha uanzishwaji wa programu zitakazohimiza tabia na desturi zifaazo zitakazojenga umoja, amani na mshikamano.
- Kuchangia, kuhamasisha na kusaidia uimarishaji wa utamaduni kwenye uandaaji wa mitaala ya skuli.
- Kuendeleza juhudi za vyombo vya habari zinazowalenga watoto na vijana kwenye skuli.
- Kuimarisha matumizi sahihi ya Kiswahili kama lugha ya Taifa na kuhimiza kujifunza na kutumia Kiingereza kama lugha muhimu ya kigeni.
- Kuanzisha ushirikiano na Idara inayohusika na utamaduni, taasisi zisizo za kiserikali na jamii.

## 5.11. ELIMU YA MAZOEZI YA VIUNGO NA MICHEZO.

### 5.11.1 utangulizi.

Elimu ya mazoezi ya viungo na michezo ina thamani kubwa katika suala la utoaji wa elimu. Michezo inachangia katika ustawi wa mwanafunzi kimwili na kijamii, kwa hivyo inapaswa kuingizwa katika programu za skuli. Inatoa fursa kwa watoto kujifunza, kufanya kazi kwa mashirikiano, kuonana na watu wengine, kujenga urafiki mpya na kukuza fikra za ziada. Michezo hutoa fursa kwa mwanajamii na Taifa kutambulika.

### 5.11.2 Hali ya sasa.

Michezo na mazoezi ya viungo yanaendelezwa skuli kuanzia ngazi ya elimu ya maandalizi hadi elimu ya juu. Wanafunzi wenye umri mdogo wanafanyishwa shughuli za michezo na mazoezi ya viungo ili kulinda afya ya miili yao na akili. Kuna shughuli nyingi za mazoezi ya viungo na michezo katika skuli za maandalizi ingawa si programu zilizoandaliwa kitaalamu kuwasaidia wanafunzi. Kwa ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu, wanafunzi wanapata nafasi ya kushiriki kwenye michezo iliyo maarufu kama mpira wa miguu, kuogelea, mpira wa wavu, mpira wa meza, mpira wa kikapu kama ni sehemu iliyo nje ya mtaala. Hata hivyo, mazoezi ya viungo na michezo haikuwekewa programu zilizopangiliwa kitaalamu katika ngazi hizi. Hakuna vifaa vya kutosha katika kuendeleza michezo hii maarufu. Programu pekee ya

elimu ya mazoezi ya viungo na michezo iliyopangiliwa ipo Chuo cha Ualimu Nkrumah na inatoa walimu wengi waliosomea fani hiyo ambao hatimaye hupelekwa katika skuli mbalimbali za sekondari.

**5.11.2 .1 Mafanikio.**

- Kuwepo kwa Idara ya Michezo.
- Kukuza tabia njema za wanafunzi kupitia mashindano ya michezo.
- Kupata vigezo vizuri kupitia michezo maarufu.
- Kuwepo kwa programu ya somo la mazoezi ya viungo na michezo katika Chuo cha Ualimu Nkrumah.
- Michezo inapendwa sana na vijana wengi na wakuzaji wa ndani wa michezo.
- Kuwepo kwa sera ya michezo.

**5.11.2 .2 Mapungufu.**

- Somo la elimu ya mazoezi ya viungo na michezo halijaingizwa kwenye ratiba ya vipindi vya skuli.
- Uhaba wa viwanja vya michezo, makocha wenye sifa pamoja na vifaa vya michezo.
- Uhaba wa vifaa vya michezo kwa watoto wenye mahitaji maalumu.

**5.11.2 .3 Tamko la Sera.**

- Somo la elimu ya mazoezi ya viungo na michezo litajumuishwa katika mitaala ya skuli.
- Skuli zitafanya michezo mbalimbali na kutoa vifaa.
- Wanafunzi wenye vipaji wataenziwa na watapewa fursa za kukuza vipaji vyao.

**5.11.2 .4 Mikakati.**

- Kutoa mafunzo ya michezo kwa walimu.
- Kutoa vifaa vya michezo.
- Kuanzisha utaratibu utakaopelekea kuvitambua vipaji vya michezo.
- Kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali kutoka kwa watu binafsi, mashirika ya wafanyabiashara, taasisi zisizo za kiserikali katika kukuza mazoezi ya viungo na michezo katika skuli.
- Kutoa vifaa vya michezo kwa makundi maalumu kama vile wanawake, wanafunzi wanawake na watoto wenye ulemavu.
- Kuimarisha burudani za ndani na nje kwa watoto.
- Kuweka muda maalum kwa ajili ya somo la elimu ya viungo na michezo katika ratiba za vipindi vya masomo vya kila siku.
- Kuanzisha uhusiano na mabaraza ya michezo ikiwemo Idara inayohusika na michezo pamoja na taasisi za michezo za kitaifa na kimataifa.

## SURA YA SITA
## WALIMU NA KAZI YA UALIMU

### 6.0 UTANGULIZI

Malengo ya Elimu kwa Wote (EFA) yanayaelekeza mataifa kuinua hadhi, hamasa na weledi kwa walimu. Walimu ni sehemu muhimu sana katika kunyanyua ubora wa elimu ikiwa skuli au katika programu mbali mbali zinazohusiana na jamii. EFA inatilia mkazo kuheshimiwa kwa walimu katika nyanja zote, kupewa stahiki za kutosha, kupewa fursa za mafunzo na kukuzwa kitaaluma. Maendeleo ya taaluma na ufanisi wa uongozi katika kazi ya ualimu ni nyenzo muhimu katika kuinua ubora wa elimu. Walimu wenye sifa na wenye kupewa motisha pia ni miongoni mwa mambo yanayopelekea kupatikana kwa mafanikio ya elimu.

### 6.1 UAJIRI NA UGAVI WA WALIMU.

#### 6.1.1 Utangulizi.

Ufanisi katika kuajiri walimu, ugavi uliobora pamoja na kuwatumia vizuri walimu ni muhimu sana katika kuhakikisha ufanisi wa kazi ya ualimu. Vigezo na miongozo iliyowazi katika kuwatambua, kuwavutia, kuwapa fursa za mafunzo na kuhakikisha kuwa walimu waliosomea na wenye sifa wanabaki katika kazi ya ualimu. Vigezo na taratibu hizo lazima zisimamie uteuzi wa walimu wenye sifa za kupata mafunzo watakaoweza kumuandaa mwanafunzi katika kukabiliana na changamoto za kitaifa na kimataifa.

#### 6.1.2 Hali ya Sasa.

Katika mwaka 2004 kulikuwa na walimu 7,633 katika skuli za serikali, kati ya hao 4,403 sawa na asilimia 57.7 ni wanawake. Katika hali ya kawaida inaonekana kwamba kuna idadi ya kutosha ya walimu, lakini ugavi wa walimu bado ni tatizo.Wizara inayoshughulikia elimu ndiyo pekee inayohusika na uajiri wa walimu katika skuli za serikali, lakini kutokuwepo ufanisi mzuri katika kitengo cha takwimu katika Wizara kwa kawaida hupelekea uajiri na ugavi wa walimu kutozingatia mahitaji halisi.

Uwiano wa walimu kwa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya lazima ni wanafunzi 31 kwa mwalimu mmoja (31:1). Uwiano wa walimu kwa wanafunzi katika skuli za serikali ni wanafunzi 33 kwa mwalimu mmoja (33:1); wakati katika skuli za binafsi ni wanafunzi 16 kwa mwalimu mmoja (16:1). Mlinganyo kama huo unatofautiana sana kati ya Wilaya moja na nyengine. Kwa mfano wilaya ya Kaskazini B Unguja ndiyo yenye wastani mdogo wa walimu ambayo ina uwiyano wa wanafunzi 27 kwa mwalimu mmoja (27:1), wakati wilaya ya Micheweni Pemba ina uwiano wa wanafunzi 46 kwa mwalimu mmoja (46:1). Wilaya zote isipokuwa Wilaya ya Micheweni zina uwiano wa wanafunzi chini ya vigezo vya Kimataifa ambavyo ni wanafunzi 40 kwa mwalimu mmoja (40:1).

Ingawa idadi ya walimu inaongezeka, ongezeko hilo ni kwa baadhi ya masomo tu. Masomo ya kiingereza, hisabati na sayansi yanabaki kuwa na uhaba wa walimu, hali inayopelekea baadhi ya walimu kuwa na idadi kubwa ya vipindi vya kusomesha.

##### 6.1.2.1 Mafanikio.

- Idadi ya walimu wa sekondari waliopata mafunzo ya ualimu imeongezeka.
- Idadi kubwa ya walimu wanawake inathibitisha uwepo na udhibiti wa walimu.

#### 6.1.2.2 Mapungufu.

- Skuli nyingi hazina nyumba za walimu kitu ambacho hupelekea ugavi wa walimu kuwa mgumu.
- Ukosefu wa uratibu mzuri baina ya uajiri na ugavi wa walimu.
- Ukosefu wa chombo maalum cha kuajiri na kugawa walimu.
- Kazi ya ualimu haionekani kama ni kazi ya heshima.
- Ukosefu wa uwajibikaji kwa baadhi ya walimu.

#### 6.1.2.3 Tamko la Sera.

- Kutakuwa na chombo kimoja tu cha uajiri wa walimu.
- Uajiri wa walimu utakuwa wazi, utakaozingatia mahitaji na utafanywa kulingana na vigezo maalum ili kuhakikisha kupata walimu wenye sifa.
- Walimu watapewa uzoefu na fursa ya kufanya kazi mjini na vijijini kwa muda maalum ulioelezwa na Serikali kama ni sehemu ya kujifunza na ili kupata ugavi sawa wa walimu.
- Idadi ya walimu wasiosomea haitozidi asilimia 10 ya walimu wote na katika skuli zote.

#### 6.1.2.4 Mikakati.

- Kuimarisha mfumo wa kukusanya takwimu za kielimu kwa kupata data sahihi na kwa wakati ili zitumike katika kuwagawa walimu wakati wanapo ajiriwa.
- Kufanya marekebisho ya uwiano wa wanafunzi kwa darasa, idadi ya walimu na idadi ya vipindi kwa mwalimu.
- Kuwapa maafisa wa elimu wa wilaya majukumu ya kugawa walimu katika skuli kwa mujibu wa mahitaji.
- Kujenga nyumba za walimu.
- Kufanya kampeni maalum kwa ajili ya kuwaajiri na kuwabakisha walimu wenye vipaji maalum.
- Kutilia nguvu kuwepo kwa kipindi cha majaribio kwa walimu.
- Kuanzisha uhusiano na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF), kampuni za ujenzi, Maafisa elimu wilaya, Chama cha Walimu, Wakaguzi wa elimu na Baraza la Manispaa.

## 6.2 MUUNDO WA KAZI NA MALIPO.

### 6.2.1 Utangulizi.

Walimu wanahitaji kupatiwa mafunzo wakiwa kazini na kupata ushauri endelevu wa kitaaluma. Muundo wa kazi ya ualimu unaelekeza kuwa mishahara ya walimu izingatie mafunzo aliyopata mwalimu. Muundo wa kazi ya ualimu lazima uzingatie tabia njema, uzoefu na mafunzo. Wakati mwingi walimu wanapata tabu kutokana na ukosefu wa muongozo ulio wazi na unaotambulika ambao unawapa fursa za kujiimarisha na kujiendeleza wakiwa kazini. Lazima ziwepo fursa nyingi kwa mwalimu kuweza kujiendeleza katika fani tafauti. Kutokuwepo kwa fursa hizo, kunapelekea walimu wengi kujihisi kama kwamba wametengwa na mwishowe kuvunjika moyo.

### 6.2.2 Hali ya Sasa.

Upo utaratibu wa kuongeza mishahara kwa walimu unaozingatia uzoefu katika kazi. Lakini utekelezaji wake unakwama kutokana na ufinyu wa bajeti. Matokeo yake, hakuna uwazi katika

kuongeza mishahara ya walimu isipokuwa kwa kuzingatia kiwango cha elimu kutoka ngazi moja kwenda nyengine. Mishahara ya walimu haikidhi haja na haiwatii moyo walimu wenye sifa kubakia katika kazi ya ualimu. Baadhi ya walimu hufidia mishahara yao kwa kufanya kazi katika sekta nyengine na kudharau kazi yao ya kusomesha.

#### 6.2.2.1 Mafanikio.

- Kuwepo kwa muundo wa utumishi wa mishahara ya walimu.
- Kuna utayari wa Serikali katika kurekebisha mishahara ya walimu.
- Chama cha Walimu kimeanzishwa.
- Kuwepo kwa fursa za kujiendeleza.

#### 6.2.2.2 Mapungufu.

- Upandishaji cheo kwa walimu hauko wazi na wala haufuati muundo wa utumishi wa mishahara uliokubaliwa.
- Nyongeza ya mshahara ya mwaka haizingatii utendaji bora wa kazi.
- Hakuna mfumo rasmin wa mawasiliano baina ya Wizara na Chama cha Walimu.
- Upandishwaji vyeo unazingatia zaidi taaluma kuliko utendaji.

#### 6.2.2.3 Tamko la Sera.

- Kutakuwa na muongozo maalum kwa mwalimu utakaozingatia uzoefu, utendaji wa kazi na mafunzo.
- Kutaundwa chombo chenye jukumu la kuangalia/kurekebisha mazingira ya kazi kwa walimu kwa mujibu wa muundo wa utumishi.
- Kutakuwa na mfumo wa kueleweka kwa kila mwaka ambao utasimamia utekelezaji wa utoaji motisha kwa walimu kulingana na muundo wa utumishi.

#### 6.2.2.4 Mikakati.

- Kuupitia muundo wa utumishi wa walimu.
- Kuboresha kiwango cha motisha kwa walimu.
- Kuunda mfumo sahihi wa mapitio ya utendaji wa kazi.
- Kuingiza na kushirikisha Chama cha Walimu ndani ya sheria ya elimu.
- Kuingiza mafunzo kazini kama ni mfumo wa kuwaendeleza walimu.
- Kuanzisha uhusiano wa karibu kati ya Tume ya Utumishi, Chama cha Walimu, Hazina na skuli.

## 6.3 MAFUNZO YA UALIMU.

### 6.3.1 Utangulizi.

Ualimu ni kazi inayoendana na mabadiliko. Kukua kwa utafiti na sayansi huzaa falsafa mpya, mbinu mpya za kufundishia na huibua maudhui mapya katika mtaala. Ufanisi katika mafunzo kabla ya kazi lazima yakubali mabadiliko kama ni kichocheo cha uhalisia wa kazi ya ualimu. Mafunzo lazima yawashajiishe walimu kuwa na hamu ya kufanya kazi ya ualimu na kukuza vipaji vyao kulingana na mabadiliko ya wakati. Kuwaendeleza walimu kuwe ni utaratibu endelevu ambao unajumuisha mafunzo kazini. Kwa mujibu wa tamko la Elimu kwa Wote, hakuna mabadiliko katika elimu yatakayopatikana bila ya kuwashirikisha walimu kikamilifu.

#### 6.3.2 Hali ya Sasa.

Kwa hivi sasa, vipo vyuo vinne (4) vya ualimu vinavyotoa mafunzo ya ualimu katika ngazi ya cheti na diploma. Vile vile, Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) vina programu za kufundisha walimu wa sekondari katika ngazi ya shahada ya kwanza. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania pia kinatoa mafunzo ya ualimu katika ngazi ya shahada ya kwanza ya elimu. Wahitimu wengi hujikita zaidi katika masomo ya sanaa na jamii kuliko masomo ya hisabati na sayansi.

Vile vile, walimu wengine hupatiwa mafunzo kupitia programu ya elimu masafa. Zaidi ya walimu 200 wasiopata mafunzo ya ualimu wamehitimu katika daraja la III A kupitia programu hii ya elimu masafa.

#### 6.3.2.1 Mafanikio.

- Kuwepo kwa vyuo vya ualimu vya kutosha.
- Kuwepo kwa programu za mafunzo ya elimu masafa.
- Kuongezeka mwamko miongoni mwa walimu juu ya haja ya kujiendeleza wenyewe kitaaluma.
- Kuwepo kwa programu ya kuwaendeleza walimu hasa katika masomo ya sayansi.

#### 6.3.2.2 Mapungufu.

- Mafunzo ya ualimu yanaendeshwa bila ya kuwa na sera na miongozo iliyowazi.
- Matokeo ya mafunzo ya ualimu hayaendani na mahitaji ya skuli hasa katika masomo ya sayansi na hisabati.
- Vyuo vya ualimu havipatiwi fedha za kutosha.
- Uhaba wa walimu wakufunzi wa kada ya ualimu.
- Muda wa mafunzo hautoshelezi kuwaandaa walimu kuwa na ujuzi pamoja na uwezo unaotakiwa.
- Hakuna uhusiano kati ya mafunzo kabla ya kuajiriwa na yale ya baada ya kuajiriwa.
- Hakuna programu mahususi kwa mafunzo ya walimu wa maandalizi.
- Vyuo vya ualimu vinakosa ubunifu.
- Hakuna usimamizi na ufuatiliaji kwa walimu wahitimu baada ya kumaliza mafunzo.

#### 6.3.2.3 Tamko la Sera.

- Kianzishwe chombo kitakachohakikisha udhibiti wa ubora wa mafunzo ya ualimu.
- Muda wa mafunzo utategemea ujuzi, taaluma na uwezo unaotakiwa.
- Programu za mafunzo ya ualimu ziwe za ubunifu na ziendane na mabadiliko.
- Vyuo vya ualimu vitakuwa ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).
- Mafunzo ya walimu kazini yatakuwa endelevu, yatapangiliwa vizuri na ni sehemu ya kuwaendeleza walimu.
- Teknolojia ya Habari na Mawasiliano itaendelezwa ili iwe ni chombo cha kuimarisha usomeshaji na kujifunza.

#### 6.3.2.4 Mikakati.

- Kuwa na mpango maalumu unaoonesha uwiano na mahitaji ya walimu.
- Kuanzisha kada maalum kwa walimu wakufunzi.
- Kuboresha mtaala wa mafunzo ya ualimu utakaozingatia mahitaji ya ufaulu katika taaluma na mbinu mpya zinazoendana na wakati.

- Kutumia mbinu mbali mbali za kufundishia katika mafunzo ya ualimu na katika kuandaa andalio la somo.
- Walimu wote wapatiwe mafunzo juu ya taaluma ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.
- Kuvitumia vyuo vikuu vilivyopo kwa kufundisha idadi kubwa ya walimu bora.
- Kuanzisha uhusiano na vyuo vikuu, skuli, taasisi zisizo za kiserikali, vituo vya walimu, taasisi za kidini na vitengo vya utafiti vya Kimataifa.

## 6.4 VITUO VYA WALIMU.

### 6.4.1 Utangulizi.

Vituo vya walimu vinavyotokana na ubunifu katika elimu vimethibitika kuwa na umuhimu mkubwa katika nyanja tafauti - kukuza taaluma na ujuzi wa walimu, ni sehemu ya kukutana katika kubadilishana mawazo na uzoefu, ni sehemu ya ufumbuzi wa matatizo, kujenga kujiamini na kufanya kazi kwa pamoja.

### 6.4.2 Hali ya sasa.

Kwa hivi sasa, kuna kituo kimoja cha Taifa cha walimu na vituo tisa vya walimu katika kanda zote za Unguja na Pemba. Pia kuna vituo vitatu vya mafunzo ya walimu wa maandalizi, kimoja kati ya hivyo ni cha jamii. Vituo vya walimu vinaongozwa na Mratibu wa kituo pamoja na washauri wa masomo. Vituo vyote hivyo vinaongozwa na kamati ya uongozi wakiwemo walimu wakuu kwa kila klasta.

Vituo vya walimu vya kanda vimeunganishwa pamoja na kituo cha Taifa cha walimu ambacho kinaongozwa na mkuu wa kituo akisaidiwa na wakuu wa seksheni tatu, mkuu wa mafunzo na huduma za ushauri, mratibu wa vituo vya walimu na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Washauri wa vituo vya walimu wa kanda wanafanya kazi pamoja na mkuu wa washauri aliyeko katika kituo cha Taifa cha walimu.

Kwa hivi sasa, vituo vya walimu vinatoa mafunzo kazini kwa walimu na vinahusika na masomo ya walimu ya kila siku kwa kuwaendeleza walimu kitaaluma pamoja na kuwapa mbinu bora za kufundishia. Lengo la jumla ni kuendeleza vituo vya walimu kuwa ni vituo vya kijamii.

#### 6.4.2.1 Mafanikio.

- Walimu walio wengi wanaweza kuvifikia vituo vya walimu.
- Mafunzo katika vituo vya walimu hutolewa ili kukidhi mahitaji ya walimu.
- Vituo vya walimu hutilia mkazo katika kutengeneza vifaa tafauti vya kufundishia.
- Wajumbe wa kamati ya uongozi ya vituo vya walimu wana uzoefu katika masuala ya kielimu.
- Vituo vya walimu vinakubalika sana na walimu pamoja na jamii.

#### 6.4.2.2 Mapungufu.

- Uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.
- Uwezo mdogo wa wafanyakazi katika kuendesha vituo vya walimu.
- Vituo vya walimu vya kanda vinahudumia walimu wengi wa msingi na sekondari ya awali.
- Idadi kubwa ya skuli katika klasta kunapelekea vifaa viliopo katika vituo vya walimu kuwa havitoshelezi.

#### 6.4.2.3 Tamko la Sera.

- Vituo vya walimu vitatumika katika kuimarisha taaluma za walimu kwa mujibu wa miongozo iliyopo.
- Mfumo wa vituo vya walimu utasaidia kubadilishana uzoefu, ubunifu pamoja na matokeo ya utafiti hasa kwa kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT).

#### 6.4.2.4 Mikakati.

- Kuboresha vituo vya walimu kwa kuvipatia vifaa vya kutosha pamoja na rasilimali watu.
- Kuviwezesha vituo vya walimu kuibua fursa zilizopo zinazotolewa na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.
- Kufufua paneli za walimu za masomo.
- Kuufanyia marekebisho mfumo wa uongozi wa vituo vya walimu.
- Kuanzisha vituo vipya vya walimu ili kukidhi haja ya ongezeko la skuli na walimu.
- Kuvipa msukumo vituo vya walimu vishughulikie wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
- Kushajiisha jamii kujua kazi na umuhimu wa vituo vya walimu.
- Kuimarisha uwezo wa waratibu wa vituo vya walimu, washauri wa masomo na wafanyakazi.
- Kuanzisha chombo cha kuunganisha pamoja baina ya Chuo cha Ualimu, kitengo cha Mitaala, wakaguzi, skuli, Chama cha Walimu na jamii.

## SURA YA SABA
## UONGOZI KATIKA ELIMU

### 7.0 UTANGULIZI.

Juhudi na mafanikio katika kuongeza kiwango na ufanisi wa elimu katika mitaala, vifaa, nyenzo, muda wa kufundishia na kuongeza ubora wa ufundishaji kama njia muhimu ya kuleta mafanikio ya mwanafunzi inategemea zaidi uwezo wa kiutawala na kitaasisi katika mfumo wa elimu. Hali hii itahitaji mambo matatu yafuatayo:

(i) Muundo wa kitaasisi.
(ii) Uwezo wa uongozi.
(iii) Mfumo wa utoaji habari.

Pia inapasa kuzingatia masuala ya urasimu, hali halisi ya kijamii na kisiasa iliyopo katika jamii ambapo mfumo wa elimu unafanyakazi. Hivyo, muundo wa utawala wa Wizara / elimu kwa ujumla unatakiwa kuakisi na kuwa na uhusiano na muundo wa sekta ya umma (serikali) katika dira yake, malengo, dhamira na misingi ya maadili kwa ujumla.

### 7.1 MUUNDO WA WIZARA.

#### 7.1.1 Utangulizi.

Muundo wa Wizara yoyote yenye jukumu la kusimamia elimu huakisi majukumu, malengo na madhumuni kwa ajili ya utoaji wa huduma za elimu. Muundo lazima uweze:

(i) Kuwapa viongozi katika ngazi zote mamlaka na nyenzo zitakazowawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi
(ii) Kufafanua kwa uwazi wajibu na majukumu ya viongozi au mipaka na mamlaka ya uwakilishi wao.
(iii) Kuanzisha mfumo wa mawasiliano na kufafanua uhusiano wake.

#### 7.1.2 Hali ya sasa.

Wizara inaongozwa na Waziri akisaidiwa na Naibu Waziri. Majukumu ya Viongozi hawa ni ya kisiasa zaidi kuliko ya kitaaluma katika kukuza elimu. Katika utekelezaji wa sera Waziri anashauriwa na Baraza la Elimu ambalo wajumbe wake wameteuliwa kwa mujibu wa Sheria ya elimu. Katibu Mkuu anafanya kazi za kiufundi na kitaaluma; na pia ndie msimamizi mkuu wa utumishi na Ofisa Mkuu wa Uhasibu. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Katibu Mkuu wa Wizara anasaidiwa na Naibu Katibu Mkuu. Kwa upande wa Pemba majukumu ya uongozi wa Katibu Mkuu huendeshwa na Ofisa Mdhamini.

Chini ya Katibu Mkuu, kuna makamishna wawili wenye kusimamia Idara kumi na moja. Ofisi za elimu za Mikoa na Wilaya, vyuo vikuu, vyuo vya elimu na skuli hazikuainishwa kwa uwazi katika muundo wa Wizara, lakini zimeunganishwa kwa mujibu wa Idara zinazohusika. Licha ya kuwepo kwa ofisi za elimu katika mikoa na wilaya, maamuzi makubwa hutolewa katika ngazi ya wizara na maofisa elimu wa mikoa na wilaya wana uwezo mdogo wa kutoa maamuzi.

##### 7.1.2.1 Mafanikio.

- Kuwepo kwa viongozi wataalamu wenye sifa na uzoefu katika ngazi ya Wizara.
- Kuwepo kwa ufafanuzi wa majukumu na wajibu wa kazi.
- Kuwa na mikutano ya mara kwa mara kati ya wakurugenzi na uongozi wa juu wa wizara.

**7.1.2.2.Mapungufu.**

- Muundo wa Wizara umepewa dhamana nzito.
- Uwezo mdogo wa kitaasisi.
- Kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa ugavi wa wafanyakazi.
- Kutokuwepo kwa uhusiano mzuri kwenye mawasiliano ndani ya Idara na baina ya Idara na Idara.
- Muingiliano wa majukumu.

**7.1.2.3 Tamko la Sera.**

- Muundo wa taasisi na kazi za Wizara lazima zitawiana katika ngazi zote.

**7.1.2.4 Mikakati.**

- Kurasimisha na kuimarisha chombo cha usimamizi.
- Kuanzisha programu za kuzijengea uwezo taasisi.
- Kufanya mapitio ya kazi na majukumu ya kila Idara.
- Kuimarisha uhusiano wa ndani na nje.

## 7.2 MGAWANYO WA MADARAKA KATIKA ELIMU.

**7.2.1 Utangulizi.**

Mgawanyo wa madaraka ni uhamisho wa mamlaka ya kiutendaji kutoka serikali kuu kuelekea bodi za serikali za mitaa. Kwa ujumla, mamlaka huhamasisha utafutaji na mgawanyo wa rasilimali. Mgawanyo wa madaraka huimarisha serikali za mitaa kufanya kazi kama sekta mbali mbali za serikali katika ngazi ya mitaa. Hivyo, huduma ya elimu inaweza kutolewa kwa ubora na kwa ufanisi zaidi. Hali hii itaiwezesha Wizara kushughulikia kwa umakini masuala kiujumla zaidi yakiwemo uandaaji wa sera, ufuatiliaji, kuhakikisha ubora, kuandaa mpango mkakati na masuala ya fedha.

**7.2.2 Hali ya sasa.**

Mfumo wa utawala uliopo unaelezwa kuwa haujatoa madaraka kamili kwa ofisi za elimu za Mikoa na Wilaya na hazijapatiwa wataalamu kutoka makao makuu ya Wizara. Wizara imetoa baadhi ya kazi na majukumu yake katika ngazi za elimu Mkoa na Wilaya lakini utoaji wa maamuzi na majukumu ya kifedha bado yamebakia katika Wizara. Maofisa Elimu Mkoa na Wilaya wana madaraka madogo. Maofisa hao wanawajibika kwa uongozi wa Mkoa na Wizara inayohusiana na elimu; jambo ambalo huwa ni chanzo cha mgogoro katika maslahi na uwajibikaji. Pamoja na uanzishwaji wa ofisi za Mikoa na Wilaya, lakini bado maofisa wa ofisi hizo hawajengewi uwezo wa kiutendaji. Kunakosekana uwazi katika uhusiano wa mamlaka na majukumu ya taasisi kutoka ngazi tafauti. Hakuna uhusiano mzuri katika kazi baina ya bodi za elimu za Mikoa au Wilaya na ofisi kuu ya elimu. Kazi na majukumu ya kamati za skuli hayafahamiki vizuri.

**7.2.2.1 Mafanikio.**

- Wizara ya elimu, utamaduni na michezo imeanzisha Idara mbali mbali.
- Kuwepo kwa utayari wa kugawanya madaraka mikoani.
- Kuwepo kwa Baraza la Elimu la Taifa, Bodi za Elimu za Mkoa na Wilaya, kamati za skuli na serikali za wanafunzi.
- Udogo wa nchi na mfumo ulio wazi unayafanya mawasiliano yawe mepesi na rahisi.
- Ofisi ya elimu Pemba hutengewa bajeti yake.

#### 7.2.2.2 Mapungufu.

- Ukosefu wa uwazi katika mipaka ya mamlaka na wajibu.
- Wajumbe wengi wa kamati za skuli ni wa kuteuliwa na sio wa kuchaguliwa.
- Majukumu na kazi za kamati za skuli hazifahamiki vizuri.
- Ukosefu wa uwazi wa majukumu na njia bora za mawasiliano baina ya Baraza la Elimu la Taifa na Bodi za Elimu Mkoa na Wilaya kwa upande mmoja na Wizara kwa upande mwingine.
- Maofisa elimu Mkoa na Wilaya wametilia mkazo zaidi juu ya masuala ya utawala badala ya majukumu ya kitaaluma.
- Wizara kuingilia kati masuala ambayo yanapaswa kutekelezwa na Maofisa Elimu Mkoa na Wilaya.

#### 7.2.2.3 Tamko la Sera.

- Wizara inatakiwa kuelezea na kufafanua majukumu na kazi katika mamlaka za ofisi kuu, Mkoa na Wilaya kwa kuzingatia hali halisi ya kijiografia, udogo ya nchi na uwezo mdogo wa uongozi na maofisa watendaji.
- Vyuo vikuu na vyuo vya elimu vitajitegemea, taasisi zitakuwa huru kuwajibika kwa Bodi zao za elimu ndani ya mamlaka zao.
- Maofisa elimu Mkoa na Wilaya watakua na uwezo wa kitaaluma katika kutoa mwongozo sahihi na msaada kwa skuli na wakati huo huo kuongoza katika kupanga na kusimamia maendeleo katika mfumo wa elimu.

#### 7.2.2.4 Mikakati.

- Kuifanyia ukaguzi wa hesabu za matumizi Wizara ya elimu na taasisi zake.
- Kushirikisha jamii katika maendeleo ya skuli kwa ujumla.
- Kuweka mipango ya maendeleo ya rasilimali watu.
- Kutafsiri upya mgawanyo wa majukumu ya kazi za kamati za skuli.
- Kuimarisha uhusiano wa Wizara na washirika wa maendeleo pamoja na walengwa wa elimu.
- Kuimarisha matumizi ya TEKNOHAMA katika kurahisisha huduma ya mawasiliano yanayohitajika katika kazi za kila siku za usimamizi wa elimu na kubadilishana taarifa kati ya ofisi mbalimbali.

## 7.3 UKAGUZI.

### 7.3.1 Utangulizi.

Ukaguzi wa skuli ni njia muhimu ya ufuatiliaji katika utoaji wa elimu unaoaminika kusaidia katika kuandaa vigezo vya mtaala na kuhakikisha ufanisi na ubora wa elimu. Wakaguzi ni wataalamu waangalizi wa mchakato wa kufundisha na kujifunza ambao hufanyika nje na ndani ya darasa. Pia mkaguzi hufuatilia mwenendo wa elimu pamoja na kuangalia upatikanaji wa nyenzo zifaazo, rasilimali watu na vifaa vya kufundishia ili kutoa ripoti muhimu kwa Wizara na wadau wengine.

### 7.3.2 Hali ya sasa.

Katika muundo wa sasa kunakuwa na Mkurugenzi wa Idara ya Ukaguzi mwenye wajibu wa kusimamia utekelezaji wa sera na kuratibu usimamizi wa Idara. Mkurugenzi anawajibika kwa Kamishna wa Elimu. Mkurugenzi anasaidiwa na waratibu wawili, mmoja kutoka Unguja na mmoja kutoka Pemba. Maofisa wawili hawa huratibu shughuli za kila siku za ukaguzi wa skuli.

Ukaguzi unafanyika kwa skuli za serikali na za binafsi. Skuli za serikali na za binafsi zinatakiwa kufuata vigezo vilivyowekwa na Wizara.Huduma ya ukaguzi inaendeshwa na Wizara. Aidha, kuna washauri wa masomo katika vituo vya walimu. Kuongezeka kwa kasi kwa idadi ya skuli kunapunguza uwezo wa wakaguzi kukagua skuli zote, matokeo yake ni kuwa skuli nyingi za serikali na za binafsi hazikaguliwi mara kwa mara.

**7.3.2.1 Mafanikio.**

- Walimu wakuu wamepatiwa mafunzo juu ya hatua za ukaguzi.
- Mikutano baada ya ukaguzi hufanyika katika ngazi za skuli kujadili matokeo ya ukaguzi.
- Washauri wa masomo hufanya ziara ili kuchunguza, kuelekeza na kuwashauri walimu.
- Kuwepo kwa uhusiano mzuri kati ya wakaguzi na walimu.

**7.3.2.2 Mapungufu.**

- Kutofanya ukaguzi wa skuli mara kwa mara na kwa utaratibu.
- Uwezo mdogo wa Idara ya Ukaguzi.
- Hakuna uhusiano kati ya wakaguzi, washauri wa masomo katika Vituo vya Walimu na Idara ya Elimu.
- Kuwepo kwa msisitizo katika masuala ya utawala kuliko msaada wa taaluma ya ufundishaji.
- Kutotumika vizuri kwa ripoti za ukaguzi katika kuimarisha ubora wa elimu.
- Kutokuwepo kwa uhusiano mzuri baina ya Idara ya Ukaguzi na Idara nyengine.
- Hakuna ufuatiliaji wa ripoti za ukaguzi.
- Uhaba wa fedha.
- Hakuna uhuru wa ukaguzi.

**7.3.2.3 Tamko la Sera.**

- Idara ya Ukaguzi itafanyiwa marekebisho na kuimarishwa zaidi ili iwe Bodi inayojitegemea.
- Idara ya Ukaguzi, Vituo vya Walimu na Vyuo vya Mafunzo ya Ualimu vitaunganishwa ili viweze kuratibu programu na shughuli zao kwa pamoja.

**7.3.2.4 Mikakati.**

- Kuifanyia marekebisho Idara ya Ukaguzi ili iwe Bodi inayojitegemea.
- Kuwajenga uwezo wakaguzi.
- Kuyafanyia kazi maoni ya wakaguzi ili kuhakikisha hatua zinazofaa zinachukuliwa.
- Kuanzisha uhusiano baina ya Vituo vya Walimu, Vyuo vya Mafunzo ya Ualimu, Ofisi za Elimu Mkoa na Wilaya, Kamati za Walimu, Kamati za skuli na Idara nyengine zinazohusika.

## 7.4 UFUATILIAJI NA TATHMINI.

### 7.4.1 Utangulizi.

Programu za elimu zimelenga kutoa matokeo yanayohitaji kufuatiliwa na kufanyiwa tathmini. Ufuatiliaji na tathmini ni kiini cha kuleta marekebisho katika utekelezaji wa majukumu na kuhakikisha ubora wa shughuli za serikali. Mfumo bora wa ufuatiliaji na tathmini ni lazima uanzishwe. Vile vile, kuwepo na uwezo wa kitaaluma na nyenzo za kufanyia ufuatiliaji na tathmini. Mambo ya msingi katika mafanikio yoyote ya ufuatiliaji wa mfumo wa tathmini ni:

- Kukusanya na kuhifadhi takwimu halisi na za kuaminika katika ngazi zote za skuli na taasisi zinazohusiana.
- Utaratibu wa kukusanya takwimu na kuzichambua kwa kutumia gharama nafuu.
- Kuwepo na uongozi unaotumia taarifa zinazotokana na takwimu katika kupanga na kutoa maamuzi.
- Kuwa na mtaalamu wa kufanya ufuatiliaji na tathmini.
- Mfumo ulio wazi wa kupeana taarifa.

**7.4.2. Hali ya sasa.**

Divisheni ya takwimu katika Idara ya Mipango na Fedha ya Wizara ya Elimu ndiyo yenye wajibu wa kufuatilia programu za elimu kwa njia ya ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa. Divisheni inasimamia mgawanyo wa madodoso kwa skuli na kukusanya taarifa za uandikishaji wa wanafunzi, mahudhurio na idadi ya walimu. Skuli pia huwasilisha ripoti za maendeleo kwa robo mwaka na za kila mwaka kuhusu hali halisi ya skuli ikiwa ni pamoja na majengo, vifaa na masuala ya kitaaluma ya skuli. Wakaguzi, kamati za skuli na bodi za skuli hutowa takwimu kwa ajili ya ufuatiliaji. Utekelezaji wa programu za maendeleo zinafuatiliwa na Idara zinazohusika kwa kushirikiana na Idara za Mipango na Fedha.Tathmini hazifanywi mara kwa mara.

**7.4.2.1 Mafanikio.**

- Katika kila Idara kumekuwa na seksheni zenye wajibu wa kukusanya takwimu na kuziweka pamoja.
- Kuwepo kwa Divisheni ya Takwimu katika Wizara.
- Mwamko wa Wizara kuhusu umuhimu wa ukusanyaji takwimu.
- Urahisi wa kuzifikia skuli kwa ajili ya ukusanyaji na usambazaji wa takwimu mara kwa mara.

**7.4.2.2 Mapunguf**u.

- Upungufu wa rasilimali ambazo zingewezesha kuchambua takwimu kwa ufanisi.
- Elimu duni juu ya uhifadhi wa takwimu.
- Upungufu wa viashiria vya ufuatiliaji na tathmini ya elimu.
- Kutokuwepo kwa programu maalumu (software) kwa ajili ya uchambuzi wa takwimu.
- Matokeo yasiyo tosheleza.
- Takwimu zisizo na uhakika.

**7.4.2.3 Tamko la sera.**

- Ufuatiliaji na tathmini utaimarishwa katika ngazi zote za elimu ili kupima ufanisi wa mfumo wa elimu.
- Viashiria katika ufuatiliaji na tathmini vya programu za elimu na mafanikio ya kujifunza vitaimarishwa.

**7.4.2.4 Mikakati.**

- Kupitia upya zana za ukusanyaji wa takwimu ili kuweza kuzitumia kwa urahisi zaidi.
- Kuupitia mfumo wa ukusanyaji wa takwimu wa skuli na utoaji wa taarifa.
- Kutumia kompyuta katika utayarishaji na uchambuzi wa takwimu.
- Kuendeleza uwezo wa kitaalamu katika ngazi zote.

- Kuanzisha uhusiano na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) pamoja na kukuza uhusiano wa ndani.

## 7.5 UTAFITI.

### 7.5.1 Utangulizi.

Matokeo ya utafiti hutoa taarifa zinazosaidia katika utekelezaji wa maamuzi na mageuzi ya sera. Wataalamu na waandaaji wa sera hutumia utafiti katika kuboresha mfumo wa elimu. Vile vile, matokeo ya utafiti wa kielimu lazima yahakikishe kwamba, mazingira ya darasani yanaimarishwa. Ili kuhakikisha malengo ya elimu yanafikiwa, mfumo wa elimu unahitaji kufanyiwa utafiti mara kwa mara.

### 7.5.2 Hali ya sasa.

Kwa hivi sasa, shughuli za utafiti zinaratibiwa na Idara ya Mipango na Fedha. Hata hivyo, utafiti haujatiliwa mkazo unaostahiki, umakini na kuthaminiwa. Mabadiliko mengi ya kisera katika elimu yamekuwa yakilenga katika kutatua matatizo yanayojitokeza kuliko kutatua matatizo kwa kutumia matokeo ya utafiti. Tafiti nyingi hutegemea ufadhili na zinalenga katika uandaaji wa mtaala na utekelezaji wa mradi.

#### 7.5.2.1 Mafanikio.

- Shughuli za utafiti zimewekwa ndani ya Idara inayostahiki.
- Kuna idadi kubwa ya nyaraka za stadi mbali mbali za kielimu zinazoweza kusaidia katika utafiti.
- Kuna uwezo mzuri wa kufanya utafiti katika Vyuo Vikuu na Vituo vya Walimu.
- Kuna mwamko mkubwa kwa wafadhili kutoa msaada katika kufanya utafiti.

#### 5.2.2 Mapungufu.

- Ukosefu wa uwezo wa kufanya utafiti kutokana na upungufu wa rasilimali watu na rasilimali fedha.
- Ukosefu wa motisha na utamaduni wa kufanya utafiti kwa kutumia takwimu zilizopo.
- Kutotumika ipasavyo matokeo ya utafiti katika kufanya maamuzi.
- Hakuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu masuala yanayohusiana na kufundisha na kujifunza.

#### 2.5.2.3 Tamko la Sera.

- Wizara itaanzisha kitengo cha utafiti kitakachowezeshwa vizuri kifedha na kiutendaji.
- Maamuzi makubwa ya kisera yatategemea matokeo ya utafiti.

#### 7.5.2.4 Mikakati.

- Kuanzishwa kituo cha kujitegemea cha utafiti.
- Kuimarisha uwezo wa taasisi na rasilimali watu katika eneo la utafiti.
- Kuhakikisha kuwepo kwa fedha kwa ajili ya utafiti.
- Kuimarisha uwezo uliopo katika vyuo vikuu na vituo vya walimu kufanya utafiti.
- Kusambaza matokeo ya utafiti kwa umma na kwa wadau.
- Kuanzisha uhusiano na vyuo vikuu, vituo vya walimu, skuli, mashirika yasiyo ya kiserikali na vitengo vyengine vya utafiti vilivyomo nchini.

## 7.6 MFUMO WA USIMAMIZI WA TAARIFA KATIKA ELIMU (EMIS).

### 7.6.1 Utangulizi.

Lengo kuu la mfumo wa usimamizi wa taarifa katika elimu (EMIS) ni kukuza na kuendeleza takwimu katika uandaaji wa sera za elimu. Uimarishaji wa mfumo wa usimamizi wa taarifa katika elimu utasaidia sana katika mipango bora ya mfumo wa elimu. Takwimu na taarifa za kielimu zinahitajika kuchambuliwa mara kwa mara.

### 7.6.2 Hali ya sasa.

Mfumo wa usimamizi wa taarifa za kielimu (EMIS) umeanza tokea katikati ya miaka ya tisini kwa kutoa taarifa juu ya uandikishaji wa wanafunzi, matokeo, vitendea kazi na rasilimali watu. Divisheni ya mfumo wa usimamizi wa taarifa katika elimu ni msimamizi mkuu wa takwimu na taarifa nyengine za kielimu. Miongoni mwa kazi zake ni pamoja na kutaarisha zana za kukusanya na kuchambua takwimu na kutoa mafunzo kwa walimu wakuu na walimu wa takwimu pale inapohitajika.

Hata hivyo, divisheni haikushirikishwa kikamilifu katika mchakato wa upangaji na usimamizi katika ngazi ya kitaifa na ngazi za jamii kutokana na mapungufu ya kiufundi na kitaasisi. Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ina jukumu kubwa katika kuratibu na kutoa msaada wa kiufundi kwa mfumo wa usimamizi wa taarifa za Wizara mbali mbali ikiwemo Wizara ya Elimu.

#### 7.6.2.1 Mafanikio.

- Kuwepo kwa divisheni ya usimamizi wa takwimu katika Wizara ya Elimu.
- Upatikanaji wa msaada wa kiufundi kutoka vyanzo vya nje na ndani.
- Mfumo mzuri wa utoaji wa taarifa za mara kwa mara kutoka skuli kwenda katika divisheni ya takwimu.
- Ushirikiano wa karibu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

#### 7.6.2.2 Mapungufu.

- Uhaba wa wafanyakazi na rasilimali.
- Uwezo mdogo wa kupata habari duniani kote.
- Matumizi madogo ya TEKNOHAMA katika mfumo wa usimamizi wa taarifa katika elimu.
- Hakuna uhamasishaji mzuri juu ya umuhimu wa takwimu.

#### 7.6.2.3 Tamko la Sera.

- Divisheni ya usimamizi wa takwimu itapewa uwezo wa kuwasaidia watumiaji wengine wa ngazi zote kuweza kukusanya takwimu.
- TEKNOHAMA itatumika katika kukuza na kusaidia upatikanaji, usambazaji na usimamizi wa taarifa.
- Mfumo wa usimamizi wa taarifa katika elimu utatumika kama chombo cha kuongoza maamuzi sahihi ya kisera katika ya ngazi zote.

**7.6.2.4 Mikakati.**

- Kuanzisha hifadhi kuu ya takwimu kwa watumiaji mbalimbali.
- Kuimarisha uwezo wa Divisheni ya usimamizi wa taarifa katika elimu kwa kuajiri wafanyakazi wa kudumu na kuwapatia mafunzo.
- Kukuza uwezo wa Divisheni ya usimamizi wa taarifa katika elimu kupitia vifaa vya kompyuta na programu zake
- Kuimarisha uhusiano wa kiidara pamoja na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Wizara nyengine.

## SURA YA NANE
## CHANGAMOTO ZINAZOJITOKEZA

### 8.0 UTANGULIZI

Mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na mengine yanayotokea katika jamii yanawafanya watoto na vijana hususani wanawake kuwa katika hatari ya kukabiliwa na vikwazo mbalimbali. Vikwazo hivyo ni pamoja na ukandamizaji, ajira za watoto, unyanyasaji wa watoto, UKIMWI, dawa za kulevya na uharibifu wa mazingira. Hali hii inazuia fursa ya kusoma na hivyo kuleta changamoto katika mfumo wa elimu, changamoto ambazo hazinabudi kutatuliwa na mfumo huo. Kwa vile skuli zimo ndani ya jamii uendeshaji wake huathiriwa moja kwa moja na hali ya kiuchumi, kisiasa na kijamii inayotokea katika jamii husika, kutokana na hilo skuli lazima ziwe na mchango muhimu kwa jamii. Kwa hiyo, mfumo wa elimu haunabudi kuimarisha mikakati na uwezo wa kukabiliana na hatari na vikwazo vinavyo wakabili watoto na vijana kwa haraka na kwa ufanisi zaidi.

### 8.1. ELIMU YA AFYA YA UZAZI KWA VIJANA.

#### 8.1.1. Utangulizi

Jitihada za kufikia upatikanaji wa fursa ya elimu ya lazima kwa wote katika nchi za Afrika, zimekuwa zikirejeshwa nyuma na matatizo yanayohusiana na afya ya uzazi kwa vijana. Vijana wanakabiliwa na changamoto nyingi za afya ya uzazi, zikiwemo kutokuwa na uwezo wa kujizuwia kupata ujauzito, utoaji mimba usio salama, maradhi ya kujamiiana na aina zote za ukandamizaji na ubakaji. Elimu ya afya ya uzazi kwa vijana ni muhimu kwa ustawi wao wa kimwili, kimtazamo na kifikra. Kuongezeka kwa uelewa, fursa mbalimbali na ushiriki wa vijana kutawawezesha kuishi wakiwa na afya njema na kushiriki katika uzalishaji ili kuchangia kikamilifu katika jamii na Taifa kwa ujumla.

Mara nyingi vijana hawapati taarifa sahihi, wamekosa fursa ya kupata huduma ya elimu ya afya ya uzazi, hawajitambui na hawajiamini; mambo yanayopelekea kutokuwa salama na kutokuwajibika.

Jinsia na utamaduni ni masuala yenye mchango muhimu katika elimu ya afya ya uzazi kwa vijana. Ndoa za umri mdogo zina madhara makubwa ya kijamii na kiafya kwa watoto wa kike. Watoto wa kike waliopata ujauzito na kuolewa ni nadra kumaliza elimu yao na wale wanaopata ujauzito bila ya kuolewa wanaweza kunyanyapaliwa na kutengwa. Vile vile wanapata tabu kutokana na uchungu wa muda mrefu wa kujifungua kwa vile miili yao haijakomaa. Hali hii inaweza kupelekea ulemavu wa kudumu au hata kifo.

#### 8.1.2. Hali ya sasa.

Kadhia ya ndoa za mapema na ujauzito ni sababu ya kuongezeka kwa idadi ya watoto wa kike wanaoacha masomo hususan katika ngazi ya elimu ya lazima. Mwamko mdogo wa baadhi ya wazazi juu ya umuhimu wa elimu na umasikini uliokithiri ni miongoni mwa sababu za ndoa za mapema. Kwa upande mwengine, kuongezeka kwa idadi ya watoto wa kiume wanaoacha masomo katika ngazi ya elimu ya lazima kunakotokana na ukosefu wa kuhamasishwa katika masomo na msukumo wa vikundi rika, kunachangia kuwaingiza katika vitendo vya kujamiiana. Katika mwaka 2003 yaliripotiwa matukio 56 yanayotokana na ujauzito wa umri mdogo miongoni mwa wanafunzi pamoja na ndoa 74. Katika baadhi ya maeneo, wazazi bado

wanapendelea kuwaozesha watoto wao katika umri mdogo hata kabla ya kumaliza elimu yao ya lazima. Ingawa mila na desturi za jamii zinawazuia vijana kujiingiza katika vitendo vya kujamiana wakiwa katika umri mdogo, utafiti unaonesha kuwa bado kuna kundi kubwa la wanafunzi wanaojiingiza katika vitendo vya kujamiiana. Maradhi ya kuambukiza yanayotokana na kujamiiana na maradhi ya UKIMWI yana taathira kwa kiwango kikubwa.

Katika mwaka 1992 Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusiana na idadi ya watu (UNFPA) ilianzisha elimu ya maadili na mazingira (MEES) kutoka darasa la 6 hadi sekondari ya awali kupitia masomo mbalimbali. Programu hii ilitayarisha vifaa vya kujifunzia kwa wanafunzi vikiwemo vitabu na kukuza vikundi vya elimu ya maadili na mazingira katika skuli kwa ajili ya kushughulikia masuala yanayohusiana na UKIMWI, mazingira na idadi ya watu. Programu hii ilianzishwa pia kwenye vyuo vya ualimu.

Jitihada nyengine zilizochukuliwa na Wizara ya Elimu, Utamaduni na Michezo katika kulinda afya ya uzazi kwa vijana waliopo katika skuli ni pamoja na kuanzisha huduma za ushauri nasaha na kuanzisha programu ya elimu kwa vikundi rika ambayo ililenga kufundisha stadi za maisha kwa vijana. Licha ya jitihada hizo vijana wengi bado wapo kwenye hatari.

**8.1.2.1 Mafanikio**

- Kuwepo kwa programu ya maadili na mazingira.
- Kuwepo kwa programu ya ushauri nasaha na walimu washauri nasaha katika skuli zote.
- Kuwepo kwa programu ya masomo kwa makundi ya vijana juu ya maendeleo ya stadi za maisha.
- Kuanzishwa “klabu za afya" katika baadhi ya skuli.
- Walimu wakuu tayari wamehamasika juu ya umuhimu wa kuandaa mazingira rafiki juu ya elimu ya afya ya uzazi kwa vijana na utowaji wa taarifa.

**8.1.2.2 Mapungufu.**

- Walimu washauri hawajapatiwa mafunzo ipasavyo.
- Kukosekana kwa uwazi baina ya wazazi na watoto wao juu ya masuala yanayohusiana na elimu ya afya ya uzazi.
- Ukosefu wa uelewa miongoni mwa vijana juu ya madhara ya ujauzito wa umri mdogo.
- Ukosefu wa elimu, mfumo wa utamaduni usio na usawa na umasikini katika familia baadhi ya wakati vinachangia maamuzi ya wazazi kukubali ndoa za umri mdogo kwa watoto wao.
- Wanaume watu wazima huwachukulia wanafunzi wa skuli wapo salama na hawana virusi vya UKIMWI.
- Fursa hafifu ya upatikanaji wa taarifa sahihi juu ya elimu ya afya ya uzazi kwa vijana.

**8.1.2.3 Tamko la sera**.

- Ukuzaji wa programu za stadi za maisha katika skuli utaimarishwa na kusimamiwa vyema ili kuwafikia walengwa.
- Pogramu madhubuti za jamii zitazowashirikisha wazazi na vijana katika kutoa elimu sahihi kuhusu elimu ya afya ya uzazi zitaandaliwa.

**8.1.2.4 Mikakati**.

- Kukuza na kuimarisha mafunzo kwa walimu juu ya elimu ya afya ya uzazi kwa vijana.
- Kukuza na kuimarisha ufundishaji wa masomo ya maadili na mazingira.
- Kuanzisha elimu rika juu ya ukuzaji wa stadi za maisha kwa wanafunzi katika skuli zote.
- Kutoa elimu juu ya VVU/ UKIMWI pamoja na elimu ya afya ya uzazi.
- Kuanzisha mbinu zifaazo za kiutamaduni katika kushughulikia masuala ya elimu ya afya ya uzazi kwa vijana.
- Kukuza programu za habari, elimu na mawasiliano zenye kuzingatia utamaduni.
- Kutoa mafunzo ya ujuzi pamoja na shughuli za burudani.
- Kuzifanyia utafiti programu mbalimbali zinazolenga elimu ya afya ya uzazi ili kutoa matokeo bora.
- Kushawishi kuacha kabisa kufanya vitendo vya kujamiiana.
- Kuanzisha uhusiano na taasisi husika,Taasisi zisizo za kiserikali, Taasisi za Dini, Mashirika ya Kimataifa, wazazi na kamati za skuli.

## 8.2 ELIMU YA VVU/UKIMWI

### 8.2.1 Utangulizi

Janga la maradhi ya UKIMWI ni tishio kubwa kwa maendeleo endelevu ya binadamu. Kuongezeka kwa madhara ya UKIMWI nchini na sehemu nyengine kunailazimu Serikali kufanya mapitio ya mambo ya msingi, mfano njia za ushughulikiaji, mitazamo ya watu, uhusiano wa wadau na jamii. Elimu lazima ifanye kazi muhimu ya kudhibiti maradhi hayo.

### 8.2.2 Hali ya sasa.

Kwa mujibu wa taarifa za Tume ya UKIMWI ya Zanzibar, zaidi ya watu 6,000 visiwani Zanzibar wanaishi na virusi vya UKIMWI. Wastani wa kiwango cha UKIMWI kwa watu wote Zanzibar ni asilimia 0.6. Kiwango cha maambukizi kwa wanawake ni asilimia 4.6 hadi 7 zaidi ya wanaume. Inakadiriwa kuwa asilimia 86 ya maambukizi yanawaathiri watu wenye umri kati ya miaka 20 na 49. Hakuna maelezo ya kina kuhusu kiwango cha maambukizi katika sekta ya elimu kwa vile utafiti haujafanywa katika eneo hilo.

Wizara ya Elimu, Utamaduni na Michezo inatambua ulazima kwa wanafunzi kupata taarifa za msingi kuhusu VVU na UKIMWI. Wizara ikishirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) pamoja na Taasisi ya Kuhudumia Vijana Afrika (AYA) wameendesha mafunzo ya waelimishaji rika kwa ajili ya wanafunzi wa skuli za msingi na sekondari, mafunzo ya kuelimisha juu ya namna ya kukabiliana na UKIMWI pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mafunzo hayo pia yameendeshwa kwa walimu wakuu na washauri wa masomo katika vituo vya walimu. Sambamba na hayo warsha juu ya hali ya UKIMWI Zanzibar na hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kushughulikia suala la UKIMWI katika skuli zimeendeshwa kwa walimu wakuu wote.

#### 8.2.2.1 Mafanikio.

- Tume ya UKIMWI Zanzibar imeanzishwa kwa ajili ya kuratibu mapambano dhidi ya UKIMWI.
- Eneo la UKIMWI limefanyiwa utafiti wa kutosha na kuandikiwa nyaraka mbalimbali.
- Kuongezeka kwa muamko miongoni mwa wanafunzi juu ya uelewa wa athari za ya VVU na UKIMWI.
- Suala la mapambano ya VVU na UKIMWI katika elimu limevuta hisia na kuungwa mkono na taasisi mbalimbali zisizo za kiserikali pamoja na Washirika wa Maendeleo.

- Elimu ya UKIMWI imeingizwa kwenye mitaala ya ualimu kupitia Elimu ya Maadili na Mazingira (MEES)
- Kuanzishwa kwa programu za elimu rika katika skuli.
- Mpango wa utekelezaji wa mapambano ya VVU na UKIMWI kwa kiasi kikubwa umetoa nafasi maalumu ya kuingiza masuala ya UKIMWI katika shughuli kuu za Wizara.
- Masuala ya VVU na UKIMWI yameingizwa katika mtaala wa ngazi ya elimu ya msingi na sekondari.

**8.2.2.2 Mapungufu.**

- Uratibu na ushirikiano dhaifu wa shughuli za mapambano ya VVU na UKIMWI miongoni mwa wadau mbalimbali.
- Pamoja na kuongezeka kwa kampeni, mabadiliko chanya ya tabia kwa walengwa yameongezeka kwa kiwango kidogo sana.
- Uwezo mdogo katika kuandaa na kutekeleza programu za kupambana na VVU na UKIMWI.
- Kukosekana muongozo ulio wazi juu ya elimu ya UKIMWI katika skuli.

**8.2.2.3 Tamko la sera**

- Muongozo sahihi wa kisera juu ya elimu ya mapambano ya VVU na UKIMWI katika kada ya elimu utaandaliwa.
- Elimu ya mapambano juu ya VVU na UKIMWI itajumuishwa katika shughuli kuu za wizara.
- Wanafunzi, walimu na watendaji wengine walioathirika kutokana na kuambukizwa UKIMWI hawatonyanyaswa, kufukuzwa, kusimamishwa kazi au kusumbuliwa na taasisi za elimu.

**8.2.2.4 Mikakati**

- Kuandaa miongozo na kujumuisha masuala ya VVU na UKIMWI katika mtaala wa skuli.
- Kutoa taarifa na stadi za maisha ambazo ni muhimu kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya VVU na UKIMWI.
- Kufanya tathmini mara kwa mara kuangalia matokeo ya programu za kupambana na VVU na UKIMWI.
- Kuandaa programu kwa ajili ya maeneo yaliyombali juu ya masuala ya VVU na UKIMWI na maradhi mengine ya kuambukiza yanayo tokana na kujamiiyana.
- Kuanzisha mtandao wa mawasiliano juu ya VVU na UKIMWI.
- Kuongeza uwezo katika kujumuisha masuala ya VVU na UKIMWI kwenye shughuli kuu za wizara.
- Kuanzisha ushirikiano na wadau wote zikiwemo taasisi zisizo za kiserikali (NGOs), mashirika ya kimataifa na tasisi za dini katika kusambaza taarifa sahihi, ujuzi pamoja na kuratibu shughuli zao kupitia taasisi za elimu.

## 8.3 ELIMU YA MAZINGIRA.

### 8.3.1 Utangulizi.

Maisha ya Wazanzibari wote yanahusiana na yanategemeaana moja kwa moja na mazingira. Maisha yetu na ya vizazi vyetu vya siku zijazo yanategemea uimarishwaji wa uhusiano bora na ulio endelevu na maumbile yanayotuzunguka. Kwa hakika elimu ni kada muhimu ambayo inaweza kutumika kukuza na kuimarisha uelewa wa elimu ya mazingira kwa ufanisi, elimu hii inaweza kuwa ama rasmi (kuanzia ngazi ya maandalizi hadi chuo kikuu) au isiyo rasmi (kwa vijana, wazee na watu tofauti kupitia taaluma zao, biashara na viwanda). Elimu ya mazingira imeleta msukumo mkubwa hususan katika uandaaji wa mtaala na maandalizi ya mwalimu.

### 8.3.2 Hali ya sasa.

Suala la mazingira limekuwa changamoto kubwa ulimwenguni, hali ambayo imepelekea kutilia mkazo elimu ya mazingira. Kwa upande wa Zanzibar, elimu ya mazingira imelenga zaidi katika uhifadhi wa misitu, fukwe, matumbawe na taathira za uchafuzi wa mazingira. Katika skuli, elimu ya mazingira imejumuishwa katika masomo tafauti kama vile lugha, masomo ya Dini ya Kiislam na jiografia. Skuli mbalimbali zimeanzisha vikundi vya mazingira. Vikundi vinashirikiana na jamii katika shughuli nyingi kama vile ulinzi wa vianzio vya maji, upandaji miti, mmong’onyoko wa ardhi na uhifadhi wa matumbawe. Shughuli za darasani zinajumuisha kusoma na kuandika filamu na kutembelea maeneo husika.

#### 8.3.2.1 Mafanikio.

- Msimamo madhubuti wa serikali katika ulinzi wa mazingira.
- Kampeni endelevu kuhusiana na uhifadhi wa mazingira kupitia vikundi vya skuli.
- Kujumuisha elimu ya mazingira katika mtaala.
- Utayari kwa wazazi na taasisi zisizo za kiserikali (NGOs) kuzisaidia skuli katika miradi ya mazingira.

#### 8.3.2.2 Mapungufu.

- Tabia na matendo ya baadhi ya wanajamii yaliyojengeka kwa muda mrefu hayaendani na jitihada za kulinda mazingira.
- Umasikini na ukosefu wa fursa za kujiongezea kipato vinarejesha nyuma jitihada za kuhifadhi mazingira
- Kutokubali mabadiliko.
- Ukosefu wa elimu.
- Ukosefu wa nyenzo za kuimarisha shughuli za vikundi.
- Hakuna mfumo wa ufuatiliaji wa mara kwa mara.

#### 8.3.2.3 Tamko la sera

- Mtaala wa elimu ya mazingira utafanyiwa mapitio, utaimarishwa na kufuatiliwa ili kuimarisha ufahamu na ujuzi wa wanafunzi na hatimae kukuza uelewa wa kimazingira na kuchangia katika maendeleo endelevu ya jamii na taifa kwa ujumla.

#### 8.3.2.4 Mikakati

- Kuendesha kampeni na kuanzisha programu za elimu ya mazingira
- Kuandaa nyenzo kwa ajili ya kutoa elimu, habari na mawasiliano kuhusu mazingira rafiki.
- Kuvitambua vyanzo mbadala vya mapato.

- Kuyafanya mazingira ya skuli kuwa kigezo cha ubora wa mazingira.
- Kuanzisha uhusiano baina ya taasisi husika na taasisi zisizo za kiserikali katika kushughulikia mazingira.

## 8.4 JINSIA

### 8.4.1 Utangulizi

Elimu ni haki ya msingi ya binaadamu na ni kitu cha lazima kwa ajili ya kufaidika na haki zote nyengine za binadamu. Kutokuwepo kwa usawa wa kielimu unaopelekea mwanamke au mwanamme kukosa elimu iliyo bora ni uvunjaji wa haki za msingi za binadamu. Katika nchi nyingi wanawake ndio wanaobeba machungu ya kutokuwepo usawa wa kijinsia unaohusiana na mfumo wa ugawaji wa rasilimali na mgawanyo wa kazi kuanzia ngazi ya familia na jamii kwa jumla.

### 8.4.2 Hali ya sasa

Serikali ya Zanzibar imetambua kwamba ushirikishwaji kikamilifu wa wanawake na wanaume katika mchakato wa maendeleo ni kiini cha kufikia maendeleo endelevu. Katika kuondoa hali ya kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia serikali imeandaa muundo wa kitaasisi ili kuingiza masuala ya jinsia katika mipango ya maendeleo ya Taifa.

Takwimu za Wizara ya Elimu Utamaduni na Michezo za mwaka 2004 / 2005 zinaonesha kuwa tafauti ya kijinsia katika uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya msingi na elimu ya lazima imepungua kwa kiwango cha kufikia asilimia 50.4 ya wanawake ukilinganisha na asilimia 49.6 ya wanaume, lakini kiwango cha uandikishaji kinaongezeka zaidi kwa wanaume kufikia asilimia 71 dhidi ya asilimia 29 ya wanawake kila mwanafunzi anapopanda ngazi za juu za elimu.

Kwa upande wa wanaorejea madarasa na wanaoacha masomo kiwango kinaonekana kuwa sawa kwa wanaume na wanawake, lakini wanapofikia mwisho wa elimu ya lazima, wanaume zaidi huacha masomo kuliko wanawake. Sababu kubwa zaidi za kuacha masomo kwa wanaume na wanawake ni mazingira yasiyoridhisha ya skuli, umasikini wa familia, ndoa za mapema na ujauzito katika umri mdogo.

Mfumo wa elimu wa Zanzibar unatoa fursa sawa za elimu, lakini bado ushiriki wa wanawake hasahasa katika masomo ya sayansi na teknolojia ni mdogo ukilinganisha na wanaume. Miongoni mwa mambo yanayochangia ushiriki mdogo wa wanawake katika masomo ya sayansi na teknolojia ni imani potofu kwamba sayansi, hisabati na teknolojia ni masomo ya wanaume. Kwa kuongezea sababu nyengine zinazochangia ni; mitazamo hasi ya kijamii, mazingira ya majumbani na utamaduni usio na usawa.

Miongoni mwa utamaduni usio na usawa ambao unaathiri ushiriki wa wanawake, ni pamoja na kuwaachisha watoto wa kike skuli kwa sababu ya ndoa za mapema na ujauzito wa umri mdogo. Kwa mfano katika mwaka 2000-2003 kiasi cha watoto wa kike 650 waliachishwa skuli kutokana na ndoa za mapema na ujauzito katika umri mdogo. Sekta ya elimu, imefanya juhudi tafauti na shughuli mbalimbali katika kukuza uwiano wa kijinsia. Miongoni mwa juhudi hizo ni uanzishwaji wa madarasa ya sayansi maalumu kwa wanawake ambayo ni ya majaribio, kuwepo kwa usawa wa kijinsia na kuondoa dhana potofu dhidi ya wanawake katika mtaala na zana za kufundishia/kujifunzia na uanzishwaji wa utoaji wa huduma za ushauri nasaha katika skuli ambazo zinawasaidia wanawake kufanya vizuri katika masomo yao. Mazingira ya nje ya skuli na vikundi rika vina athari hasi kwa watoto wa kiume kuendelea na masomo hususan katika ngazi

ya juu ya elimu ya msingi na sekondari ya awali.Watoto wa kiume wengi wanaacha skuli kutokana na kujiingiza katika biashara ndogo ndogo.

**8.4.2.1 Mafanikio.**

- Tafauti za kijinsia katika uandikishaji wa wanafunzi kwenye ngazi ya elimu ya lazima unapungua.
- Ukuaji wa uelewa juu ya haki za wanawake.
- Kuwepo Jumuiya ya Ustawi na Maendeleo ya Wanawake (FAWE).
- Elimu mbadala na elimu ya kujiendeleza inatoa fursa nyengine ya kusoma kwa walioacha masomo.
- Kuwepo kwa kitengo cha jinsia na utoaji wa huduma za ushauri nasaha kwa wanafunzi katika skuli.
- Kuwepo utetezi kwa wanafunzi wa kike waliopata ujauzito kutokuachishwa skuli.
- Kutilia mkazo masomo maalumu kama sayansi na hisabati katika programu za jinsia moja.
- Wizara imetilia mkazo elimu kwa wanawake hususan katika elimu ya juu.
- Kukuza shughuli za michezo zilizochangia kwa kiasi fulani kuwavutia wanafunzi wa kiume kutokuacha skuli.

**8.4.2.2 Mapungufu.**

- Ushiriki mdogo wa wanawake katika elimu ya juu.
- Upungufu wa watu wanaoweza kuwa vigezo kwa watoto wa kike.
- Kuwepo kwa kanuni zinazowazuia wanafunzi wenye ujauzito na walioolewa kuhudhuria skuli.
- Kuwepo kwa itikadi potofu za kitamaduni zinazobagua watoto wa kike katika jamii.
- Wazazi kuwalazimisha watoto wao kuolewa kwa sababu ya umasikini uliokithiri.
- Kukosekana kwa programu zinazoelekeza utatuzi wa matatitizo ya kielimu ya wanafunzi wanaume.
- Kuchelewa kuanza skuli kunaathiri kuendelea na masomo.

**8.4.2.3 Tamko la sera.**

- Uwiano ya kijinsia utaimarishwa katika ngazi zote za elimu.
- Wanafunzi wanaoolewa, wanaopata ujauzito na wanaojifungua wakiwa na umri mdogo wapewe nafasi nyengine ya kuendelea na elimu.

**8.4.2.4 Mikakati.**

- Kuanzisha skuli zenye wanafunzi wa jinsia moja pamoja na huduma zao za dakhalia.
- Kutoa huduma za ushauri nasaha na kutoa fursa kwa wanafunzi walioolewa, wajawazito na waliojifungua katika umri mdogo kuendelea na masomo.
- Kuajiri walimu wengi wa kike na kuwapa mafunzo kwa ajili ya skuli za sekondari.
- Kushirikiana na wadau wengine katika kukuza uwiano wa kijinsia katika elimu.
- Kuanzisha ushirikiano na wizara husika inayoshughulikia masuala ya vijana, wanawake, ajira na maendeleo ya watoto, wizara inayohusika na mambo ya fedha na uchumi na taasiai zisizo za kiserikali.

## 8.5. MATUMIZI MABAYA YA DAWA ZA KULEVYA

### 8.5.1 Utangulizi

Matumizi ya pombe, tumbaku na vilevi vyengine vilivyoharamishwa yameongezeka miongoni mwa vijana ndani na nje ya skuli. Miongoni mwa sababu zinazochangia matumizi haya ni msukumo wa vikundi rika, kupata ushawishi wa kutumia dawa hizo kupitia matangazo, filamu, televisheni na kushuka kwa maadili katika familia.

Matumizi ya vilevi miongoni mwa vijana sio tu kuwa yanaharibu afya zao lakini pia ni chanzo cha kutoweka kwa nidhamu na kuwepo kwa vurugu katika skuli. Vile vile wanafunzi ambao hutumia dawa za kulevya mara nyingi hutoroka skuli na hatimaye huwa kwenye hatari ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI.

### 8.5.2 Hali ya sasa.

Kiwango cha matumizi ya dawa za kulevya na vilevi vyengine miongoni mwa wanafunzi katika skuli hakijulikani. Inaaminika kuwa matumizi ya dawa za kulevya yanaongezeka miongoni mwa wanafunzi mjini na vijijini. Wanafunzi hao wanatoka katika familia zenye mazingira tafauti. Hakuna programu madhubuti za kupambana na matumizi mabaya ya dawa za kulevya na vilevi vyengine katika ngazi ya taifa na skuli. Jitihada za kuanzisha programu za marekebisho ya tabia katika ngazi ya taifa hazijafanikiwa. Kwa upande wa skuli kwa kiasi fulani tatizo hili limekuwa likishughulikiwa kwa kupitia programu ya Maadili na Mazingira.

#### 8.5.2.1 Mafanikio.

- Kuwepo kwa programu ya Maadili na Mazingira.
- Kuanzishwa kwa "klabu za afya" katika skuli.
- Kuwepo kwa mtandao madhubuti wa mawasiliano kupitia vyombo vya habari.
- Kuwepo kwa kitengo cha ushauri nasaha katika kuzuia utumiaji wa dawa za kulevya katika wizara ya Wanawake na Watoto.
- Kuwepo kwa taasisi zisizo za kiserikali zinazoshughulikia mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya.

#### 8.5.2.2 Mapungufu.

- Ukosefu wa uratibu katika kusambaza taarifa na mikakati ya kupambana na dawa za kulevya miongoni mwa wadau.
- Ukosefu wa programu madhubuti za elimu ya afya katika skuli.
- Ukosefu wa vituo vya kurekebisha tabia.
- Vyombo vya usimamizi wa sheria kukosa umakini.
- Tabia ya kuacha mambo yaende kiholela.
- Ukosefu wa programu madhubuti ya kuzuia matumizi ya dawa za kulevya.

#### 8.5.2.3 Tamko la sera.

- Kutakuwa na programu madhubuti za kuzuia dawa za kulevya katika skuli.

#### 8.5.2.4 Mikakati.

- Kufufua programu za elimu ya afya katika skuli
- Kuratibu na kujumuisha shughuli za taasisi mbalimbali zinazoshughulikia mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya.

- Kuongeza matumizi ya Elimu, Habari na Mawasiliano katika kusambasa taarifa sahihi juu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya.
- Kutoa fursa za burudani na michezo kwa vijana ndani na nje ya skuli.
- Kutoa mafunzo zaidi ya stadi za maisha kwa vijana.
- Kuanzisha mtandao wa mawasiliano kwa watu wanaoshughulikia utekelezaji wa sheria dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya.
- Kuanzisha kampeni madhubuti dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya kwa watoto wenye mahitaji maalumu.
- Kufanya tafiti zenye dhamira ya kubaini kiwango cha matumizi ya dawa za kulevya katika skuli.
- Kuanzisha ushirikiano na Wizara inayohusika na mambo ya afya, wizara inayohusika na Vijana, Ajira Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Taasisi Zisizo za Kiserikali, Mkemia Mkuu wa serikali, wasimamizi wa sheria na mashirika ya kimataifa.

## 8.6 AJIRA ZA WATOTO

### 8.6.1 Utangulizi

Inafahamika kuwa kiasili wazazi wanayohaki ya kuwafundisha watoto utamaduni na desturi za jamii ili kuwafanya kuwa watu wanaowajibika katika jamii, kuwa tayari kuzidumisha tamaduni hizo kwa mujibu wa wakati. Vilevile inafahamika kuwa watoto ni watu wanaonufaika kwa matendo mazuri yanayotokana na jamii na kwa hivyo jamii inayohaki ya kutaraji kuona watoto wanafanya matendo mazuri. Lakini ajira za watoto zinawanyima watoto uwezo wa kukua vizuri na zinainyima jamii fursa ya kunufaika na uwezo wa watoto wao.

Tukinukuu tafsiri iliyotolewa na Mkataba Juu ya Ajira Mbaya za Watoto wa mwaka 1999 (worst form of child- labour convention 1999), tafsiri ya ajira za watoto inayofaa zaidi kwa mazingira yetu ni "kazi ambayo kwa maumbile yake au mazingira inapofanyika inaweza kuathiri usalama, afya au maadili ya watoto". Kwa kujiingiza katika aina hii ya kazi mtoto hunyimwa fursa ya kupata elimu. Kwa kiasi kikubwa ajira za watoto husababishwa na umasikini na hivyo ufumbuzi wa muda mrefu unategemea ukuaji endelevu wa uchumi ambao utapelekea maendeleo ya kijamii, kuondoa umasikini na kufikia fursa ya elimu kwa wote.

### 8.6.2 Hali ya sasa

Wastani wa asilimia 20 ya watoto wenye umri wa kuanza skuli hawaandikishwi au hutoroka wakiwa katika ngazi ya chini ya elimu ya msingi. Hakuna utafiti uliofanywa kubaini athari za ajira za watoto katika elimu, lakini kuna ushahidi unaoonesha kuwa watoto wanashirikishwa katika kazi mbalimbali kama vile; uvunjaji wa kokoto, kupara samaki na biashara ndogo ndogo. Hali hii imepelekea wanafunzi kutoroka na kuacha skuli katika maeneo ambayo kazi hizo zinafanywa. Madhara ambayo watoto wanayapata hayana bima ya afya na wala hawapatiwi uangalizi mzuri wa afya, baadhi yao hukabiliwa na ulemavu wa maisha unaowapelekea kuacha skuli. Wakati mwengine watoto wanaochukuliwa kwa ajili ya kulelewa au kusaidia kazi za nyumbani wananyanyaswa.

#### 8.6.2.1 Mafanikio

- Utetezi dhidi ya ajira za watoto umekuwa wa hali ya juu katika ajenda za maendeleo.
- Kuwepo kwa mwamko wa jamii juu ya ajira za watoto na unyanyasaji wa watoto.
- Kuanzishwa Idara ya ajira katika wizara ya Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto inayoshughulikia ajira za watoto.

#### 8.6.2.2 Mapungufu.

- Kuongezeka kwa umasikini katika familia ni miongoni mwa sababu za ajira kwa watoto
- Watoto wanaochukuliwa kwa ajili ya kulelewa wakati mwengine wanalazimishwa kuingia kwenye ajira za watoto.
- Sheria zilizopo dhidi ya ajira kwa watoto hazina nguvu.

#### 8.6.2.3 Tamko la Sera

- Kutaanzishwa sheria madhubuti dhidi ya ajira kwa watoto.
- Muongozo wa sheria unaowataka watoto wote waliofikia umri wa kuhudhuria skuli utafanyiwa mapitio na kutekelezwa.

#### 8.6.2.4 Mikakati

- Kuendelea kutambua kuwa wazazi na jamii ni washirika katika malezi na makuzi ya watoto.
- Kutekeleza sheria ambazo zinamtaka mtoto kuhudhuria skuli.
- Kuwezesha majadiliano baina ya Wizara ya Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto na taasisi nyengine juu ya malezi bora ya watoto.
- Kukuza mwamko wa jamii juu ya ubaya wa ajira za watoto.
- Kuweka njia mbadala zitakazosaidia kupambana na unyanyasaji wa watoto.
- Kuanzisha ushirikiano na Wizara ya Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Programu za Kupunguza Umasikini, Jumuiya za Vijana, Taasisi zisizo za Kiserikali, jumuia za kiraia na taasisi za fedha.

## 8.7 UNYANYASAJI WA WATOTO

### 8.7.1 Utangulizi

Watoto ni rasilimali yenye thamani kubwa kwa jamii kwa vile wanatarajiwa kuwa raia wa siku zijazo, wazazi wa siku zijazo na nguvu kazi ya baadae. Watoto wana haki ya kuishi katika mazingira yasiyo ya unyanyasaji na matendo mabaya. Unyanyasaji wa watoto kama vile wa kimwili, maneno au kingono unawaathiri kisaikolojia na unaweza kuathiri mahudhurio na matokeo yao ya skuli. Unyanyasaji wa watoto hutokea katika mazingira tafauti kama vile nyumbani, kwenye jamii na skuli. Unyanyasaji husababisha majeraha makubwa kwa watoto, kukosa kujiamini, kujitambua na unaweza kuwapelekea kifo na wakati mwengine majeraha ya maisha. Ingawa watoto wa kike na wa kiume ni wahanga wa unyanyasaji, lakini watoto wa wa kike na wenye ulemavu wapo katika hatari zaidi ya kunyanyaswa.

### 8.7.2 Hali ya sasa

Taarifa za matukio mengi ya unyanyasaji wa watoto kutoka kwa wazazi wao au marafiki hazitolewi nyumbani. Ni kawaida kwamba wazazi wanaweza kuwaadhibu watoto ikiwa hawatofuata maelekezo yao.

Taarifa za matukio ya watoto na wanawake wanaofanyiwa vitendo vya kingono na watu wazima kwa kawaida huripotiwa katika Wizara ya Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto na vituo vya polisi. Hata hivyo kesi nyingi za matukio ya unyanyasaji wa kingono haziripotiwi

kutokana na wasiwasi na aibu kwa wazazi na wanaonyanyaswa. Kutokana na kuongezeka kwa uelewa juu ya haki za watoto, malalamiko juu ya watu wanao nyanyaswa aidha kwa maneno au kwa bakora yameongezeka. Adhabu za bakora zinaaminika kuwa ni miongoni mwa sababu za wanafunzi kuacha skuli na inalalamikiwa kuwa adhabu hizo huathiri matokeo ya wanafunzi.

**8.7.2.1 Mafanikio**

- Utetezi dhidi ya ukandamizaji wa wanawake umekuwa ukiongezeka.
- Mwamko wa jamii juu ya haja ya kutengeneza mazingira rafiki na salama kwa wanafunzi umeongezeka katika skuli na majumbani.
- Serikali imechukua hatua mbali mbali za kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji.
- Kuwepo kwa kitengo cha ushauri nasaha katika skuli.

**8.7.2.2 Mapungufu**

- Matukio mengi yanayohusiana na unyanyasaji dhidi ya watoto hayaripotiwi kwenye vyombo vya kusimamia sheria.
- Wafanyakazi wachache wa jamii waliopo hawajatilia umuhimu masuala ya unyanyasaji wa watoto.
- Programu za kudhibiti unyanyasaji wa watoto ni chache.
- Ushirikishwaji wa jamii katika kutambua na kudhibiti unyanyasaji wa watoto ni mdogo.

**8.7.2.3 Tamko la Sera**

- Zitaandaliwa sheria kali dhidi ya unyanyasaji wa watoto na kutekelezwa.

**8.7.2.4** Mi**kakati**

- Kuingiza sheria zitakazowalinda watoto katika sheria ya elimu.
- Kutoa mafunzo kwa walimu ili kutambua unyanyasaji wa watoto na matatizo yanayohusiana nayo na kutoa ushauri kwa wanaonyanyaswa na wazazi wao.
- Kuwaelimisha wazazi juu ya suala la malezi bora litakalowapelekea kutambua na kuepuka vitendo vya unyanyasaji.
- Kuanzisha ushirikiano na Wizara ya Kazi,Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Wizara ya Afya, mashirika ya kimataifa, vyombo vya kisheria na Taasisi zisizo za kiserikali.

## 8.8 AFYA NA USALAMA KATIKA MAZINGIRA YA SKULI.

### 8.8.1 Utangulizi

Watoto wanapaswa kuwa na afya njema ili wasome vizuri. Lakini pia wanahitaji kuelimishwa juu ya umuhimu wa kuwa na afya njema. Tamko la Elimu Kwa Wote linasisitiza kuwa mazingira ya kujifunzia lazima yawe safi, salama na yaliyo hifadhika. Mazingira bora ya kujifunzia lazima yajumuishe mazingira rafiki, yenye usalama na majengo yanayozingatia watu wenye mahitaji maalumu, huduma za afya na lishe, maji ya kutosha na vyoo, vifaa kwa ajili ya dharura na majanga, vifaa kwa ajili ya kushughulikia matatizo ya kiafya na kisaikolojia kwa walimu na wanafunzi.

### 8.8.2 Hali ya sasa

Wanafunzi wengi wanatoka katika familia au maeneo ambayo mazingira yake sio salama kwao kimwili na kiakili. Huenda skuli bila ya kuwa na lishe bora. Hawafanyiwi uchunguzi wa afya wa

mara kwa mara. Maradhi ya malaria, utapiamlo na kichocho ni miongoni mwa matatizo makubwa ya kiafya yanayowakabili watoto. Hali hii huchangia kurejesha nyuma ufanisi wao katika kujifunza.

Katika mwaka 1992 Wizara ya Elimu ilianzisha mradi wa mtoto kwa mtoto ambao ulielezea masuala ya afya kuhusiana na mazingira, usafi wa mwili na afya bora.Walimu walipewa mafunzo juu ya njia za kuchukua katika kujikinga na maradhi yanayosababishwa na maji. Pia kuna jitihada za kusambaza maji safi na salama na ujenzi wa vyoo kupitia programu ya mazingira na vyoo.

Baadhi ya skuli hazina nafasi ya kutosha, sehemu za kuingizia hewa na mwagaza hali inayoathiri afya za walimu na wanafunzi. Pia hazina maji safi na salama, vyoo vya kutosha na viwanja salama vya michezo, vifaa vya dharura na vya kukabiliana na majanga, vifaa kwa ajili ya huduma za afya na usalama. Hakuna muongozo ulio wazi juu ya mambo yanayopaswa kujumuishwa kuwa ni vigezo vya mazingira safi na salama ya skuli.

**8.8.2.1 Mafanikio**

- Kujumuishwa kipengele cha elimu ya afya katika mtaala wa skuli.
- Kujengwa vituo vya afya vilivyo karibu na maeneo ya watoto.
- Kuwepo kwa vilabu vya afya katika skuli.
- Kuanzisha mradi wa mazingira, maji safi na salama katika skuli 82.

**8.8.2.2 Mapungufu**

- Hakuna matengenezo ya mara kwa mara katika skuli.
- Hakuna tathmini ya kimazingira inayoonesha madhara ya kimazingira kabla ya ujenzi wa skuli.
- Hakuna mafunzo na vifaa kwa ajili ya dharura na majanga.
- Hakuna kumbukumbu na uangalizi wa kiafya kwa wanafunzi wa mara kwa mara.
- Skuli nyingi hazina sehemu za kuchezea na viwanja vya michezo.
- Hakuna chombo kinachosimamia ubora wa viwango kwa ajili ya vifaa vinavyo tumiwa na walimu na wanafunzi.
- Hakuna uratibu mzuri katika utekelezaji wa programu ya afya inayowalenga wanafunzi.
- Hakuna mafunzo yanayohusiana na sheria za usalama barabarani, tabia na jinsi ya kujikinga na majanga.

**8.8.2.3 Tamko la sera**

- Mpango wa ushirikishwaji wa sekta mbalimbali utaanzishwa ili kuimarisha mazingira safi na salama katika skuli.
- Ulinzi na usalama wa afya kwa watoto vitakuwa vipengele muhimu katika programu ya elimu.
- Afya na usalama wa mwalimu utalindwa wakati akitekeleza majukumu yake kazini.

**8.8.2.4 Mikakati**

- Kuanzisha kitengo cha kusimamia na kukuza viwango vya usalama katika skuli.
- Kuanzisha mfumo wa kumbukumbu za afya katika skuli.
- Kuanzisha tena programu za mafunzo kwa ajili ya usalama, afya na mazingira

- Kukuza utamaduni wa kufanya matengenezo ya mara kwa mara kwa ajili ya vifaa vya skuli.
- Kuandaa miongozo juu ya namna ya kuimarisha usalama wa afya na viwango katika skuli
- Kuzipatia skuli zote vifaa vya msingi kwa ajili ya usalama na dharura.
- Kutoa mafunzo kwa walimu na wanafunzi juu ya kukabiliana na matokeo ya dharura na majanga.
- Kuanzisha matumizi ya mazingira yaliyo salama na rafiki katika skuli.
- Kuanzisha mazingira ya skuli ambayo ni rafiki kwa watoto nchi nzima.
- Kutoa elimu kwa askari polisi, madereva, kamati za skuli na jamii juu ya sheria za usalama barabarani na namna ya kukabiliana na majanga.
- Kuanzisha ushirikiano na Wizara ya Afya, jumuiya za kimataifa, Taasisi zisizo za Kiserikali, askari wa usalama barabarani na wazazi.

## 8.9 USHAURI NASAHA

### 8.9.1 Utangulizi

Utoaji wa elimu unatakiwa uwe zaidi ya ufundishaji na kujifunza. Elimu itolewayo inapaswa kuhakikisha kuwa wanafunzi wanajivunia fursa na faida zinazopatikana katika elimu. Ushauri nasaha huhakikisha kuwa wanafunzi wote wananufaika na elimu bila kujali mazingira wanayotoka. Wanafunzi sio kwamba tu wanahitaji kupewa elimu lakini pia kufuatiliwa ili vipaji vyao vilindwe dhidi ya mambo yote yanayoweza kuwazuia kupata elimu. Kwa kuyaelewa mambo hayo, uwezo wa mwanafunzi katika kujifunza utakuwa umetiliwa maanani. Ushauri nasaha pia unatoa nafasi ya kuwashauri vijana namna ya kwenda sambamba na kukabiliana na mahitaji ya jamii na msukumo wa vikundi rika.

### 8.9.2 Hali ya sasa

Hivi sasa kipo kitengo cha ushauri nasaha katika Wizara ambacho kazi yake ni kuratibu huduma za ushauri nasaha katika skuli. Kuna walimu washauri wawili, mwanamke mmoja na mwanamme mmoja katika kila skuli. Mafunzo wanayopewa walimu yamejikita zaidi katika kuwashauri wanafunzi kuwa na tabia zinazokubalika na hayakujikita katika kutoa ushauri kwenye masuala ya kitaaluma, kimaono au kisaikolojia au kukabiliana na changamoto zinazojitokeza.

#### 8.9.2.1 Mafanikio

- Kuwepo kwa kitengo cha ushauri nasaha katika Wizara.
- Kuwepo kwa walimu wa ushauri nasaha katika kila skuli.
- Kuingiza programu ya ushauri nasaha katika mafunzo ya ualimu.
- Kuwepo kwa programu maalumu kwa vikundi rika juu ya stadi za maisha.

#### 8.9.2.2 Mapungufu

- Walimu wa ushauri nasaha hawajapatiwa mafunzo ya kutosha juu ya ushauri nasaha.
- Dhana nzima ya ushauri nasaha haijafahamika vizuri.
- Umuhimu wa kuwaona walimu kama washauri nasaha haujazingatiwa ipasavyo.
- Hakuna kada ya huduma za ushauri nasaha katika skuli.
- Idadi ya walimu wa ushauri nasaha katika skuli hailingani na idadi ya wanafunzi waliopo.

#### 8.9.2.3 Tamko la sera

- Huduma za ushauri nasaha katika skuli zitaimarishwa na kusambazwa ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi.
- Ushauri nasaha utaimarishwa ipasavyo na kuingizwa katika mafunzo ya ualimu.
- Kutakuwa na huduma za ushauri nasaha kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

#### 8.9.2.4 Mikakati

- Kuandaa miongozo katika utoaji wa ushauri nasaha.
- Kuzipatia skuli taarifa zinazokwenda na wakati juu ya fursa za ushauri nasaha na changamoto zinazojitokeza.
- Kutoa mafunzo zaidi kwa walimu washauri.
- Kuvihamasisha vikundi rika kuwa na tabia njema.
- Kuanzisha ushirikiano na vyama vya wafanya kazi, Mamlaka ya kuimarishaji Uekezaji ya Zanzibar, Taasisi zisizo za Kiserikali na Wizara ya Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto.

.

# SURA YA TISA
# UGHARIMIAJI WA ELIMU

## 9.0 UTANGULIZI

Kwa vile elimu inatoa mchango mkubwa katika maendeleao ya Taifa, lazima itolewe kwa jamii nzima. Mchango wa elimu katika nguvu kazi hauwezi kuepukika. Kadri mfanyakazi anapokuwa na elimu ya kutosha, ndivyo anavyokuwa na utendaji mzuri wa kazi. Kwa ujumla, kuwekeza katika elimu kunaimarisha ujuzi wa kitaaluma ambao una mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa. Dira 2020 inalenga kupunguza hali ya kutokuwepo kwa usawa na kuongeza fursa za upatikanaji wa huduma ikiwemo elimu.

Jamii ndiyo inayonufaika na elimu, kwa hivyo inatarajiwa kuchangia katika utoaji wa elimu. Serikali inalazimika kutoa elimu na kuigharimia kama njia ya kuwekeza fedha za umma ambazo huchangiwa na wananchi kwa njia moja au nyengine. Hali hii inasababisha kuwepo kwa wasiwasi na malalamiko dhidi ya matumizi ya fedha za umma. Baadhi ya maendeleo ya elimu yanachangiwa na serikali kwa ukamilifu na mengine yanachangiwa na wazee/jamii.

## 9.1 FEDHA ZA UMMA.

### 9.1.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa malengo ya Mpango wa Utekelezaji wa Malengo ya Elimu kwa Wote wa Dakar wa mwaka 2000, utoaji na ugharimiaji wa elimu kwa serikali ni muhimu ili kubaini mwenendo wa utekelezaji wa malengo ya elimu kwa wote bila ya hilo Zanzibar inaweza kushindwa kufikia baadhi ya malengo yaliyomo katika Mpango wa Kupunguza Umaskini. Kukosekana kwa mchango wa fedha wa serikali kutapelekea kuzorotesha maendeleo ya elimu hususan katika ngazi ya elimu ya lazima.

### 9.1.2 Hali ya sasa

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejidhatiti kutoa elimu na kuigharimia. Serikali inagharimia ujenzi wa skuli, ununuzi wa vifaa, utoaji huduma, masuala ya kiutawala na ya kiufundi.
Hivi sasa, Wizara inatumia takriban asilimia 90 ya bajeti kwa malipo ya mishahara ya wafanyakazi na kupelekea kukosa fedha za kutosha za kugharimia vipengele muhimu kama vile uimarishaji wa ubora wa elimu. Hata hivyo Serikali itaendelea kuwa ni chanzo kikubwa cha kugharimia sekta ya elimu.

#### 9.1.2.1 Mafanikio

- Upatikanaji wa fedha za Serikali umepelekea kufuta udhaifu wa soko la utoaji wa elimu.
- Ugharimiaji wa Serikali katika suala la elimu umewezesha utoaji wa elimu kuenea nchi nzima.
- Kutokana na Serikali kugharimia elimu, uandikishaji wa wanafunzi umeongezeka kwa kasi.
- Ugharimiaji wa Serikali katika elimu umewezesha watoto wengi kutoka katika familia masikini kupata fursa za elimu.

#### 9.1.2.2 Mapungufu

- Kiwango kikubwa cha bajeti kinachotolewa kwa ajili ya matumizi ya mishahara ya wafanyakazi kuliko matumizi mengine, kinadhoofisha mambo mengine muhimu yanayopaswa kutolewa kwa ajili ya maendeleo ya elimu.
- Udhaifu katika usimamizi wa fedha, mara nyingi unapelekea ugawaji mbaya wa rasilimali.
- Hakuna usawa wa ugawaji wa fedha za Serikali kwenye Mikoa na Wilaya na katika ngazi nyengine za elimu.

#### 9.1.2.3 Tamko la sera

- Serikali itaendelea kugharimia elimu katika ngazi zote ambapo kipaumbele kitawekwa katika elimu ya lazima.
- Serikali itatoa udhamini kamili wa masomo au usio kamili kuwezesha wanafunzi wengi kupata fursa za elimu ya juu.

#### 9.1.2.4 Mikakati

- Kuimarisha masuala ya fedha na kudhibiti matumizi yake katika masuala yote ya elimu
- Kupitia matumizi kwenye MTEF/PER.
- Kupunguza matumizi ili kutoa kipaumbele katika masuala muhimu ya elimu.
- Kushajiisha upatikanaji wa fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali vya nje.
- Kuongeza matumizi mengine yasiokuwa ya mishahara ili kuimarisha ubora wa elimu.
- Kuanzisha uhusiano na vyombo vya fedha, washirika wa maendeleo, jamii na wazazi.

## 9.2 MFUKO WA ELIMU

### 9.2.1 Utangulizi

Sababu kubwa ya Serikali kugharimia elimu ni kuleta usawa na ufanisi. Elimu kwa Wote inasisitiza kuwa, Serikali inapaswa kuwa msitari wa mbele katika utoaji wa elimu, ili kukuza usawa na ufanisi. Baadhi ya wakati, kuna haja ya kugharimia programu maalum ili kutoa fursa, usawa, ubora na ufanisi. Uanzishwaji wa mfuko maalumu wa elimu unapaswa kulenga katika kufikia malengo haya. Mfuko huu utatumika kudhamini utafiti wa kielimu, kukuza ufanisi wa kiutawala katika Wizara ya elimu na kutoa udhamini wa masomo kwa wanafunzi wenye vipaji maalumu.

### 9.2.2 Hali ya sasa

Mfuko wa elimu ya juu umeanzishwa lakini haukulenga kudhamini masuala ya utafiti au kulenga kuimarisha ubora wa elimu.

#### 9.2.2.1 Mafanikio

- Kuna utashi wa kisiasa katika kuanzisha mfuko wa elimu.
- Washirika wa maendeleo, Taasisi zisizo za Kiserikali, jumuia ya wafanyabiashara wa Zanzibar wanachanga ipasavyo.

#### 9.2.2.2 Mapungufu

- Hakuna mfuko maalumu kwa kugharimia elimu.

- Maeneo ambayo yanayohitaji kugharimiwa hayajabainishwa.
- Vyanzo vya upatikanaji wa fedha havijabainishwa.

**9.2.2.3 Tamko la sera**

- Mfuko wa elimu utaanzishwa kisheria.
- Ada za elimu zitaanzishwa na kutambuliwa kisheria.

**9.2.2.4 Mikakati**

- Kuainisha vyanzo vya ada za elimu kama vyanzo vya ziada vya kukuza bajeti.
- Kutangaza na kushawishi upatikanaji wa fedha.
- Kuhamasisha sekta binafsi katika kuchangia mfuko wa elimu
- Kuanzisha muongozo wa kisheria utakaoelezea uendeshaji wa mfuko.
- Kuwaombea misaada sekta binafsi,watu binafsi, wasamaria wema na kadhalika kutoka ndani na nje ya nchi,

## 9.3 MCHANGO WA JAMII

**9.3.1 Utangulizi**

Taasisi za elimu, hususan skuli, zina faida mbalimbali kwenye shughuli za kiuchumi na kijamii. Jamii inanufaika kutokana na matunda ya wasomi, hivyo jamii zinapaswa kushirikishwa katika shughuli mbalimbali za skuli katika kuzifanyia matengenezo na kuziimarisha.

### 9.3.2 Hali ya sasa

- Ushiriki wa jamii una umuhimu mkubwa katika kuchangia utoaji wa vifaa muhimu vya kielimu, ujenzi wa madarasa na kusaidia uongozi wa skuli.

### 9.3.2.1 Mafanikio

- Kuwepo kwa ushiriki madhubuti wa jamii katika ujenzi na matengenezo ya skuli
- Kuwepo kwa uungaji mkono wa jamii katika utoaji na utafutaji wa vifaa vya skuli
- Wahitimu wanarejea katika Mikoa wanayotoka na kusaidi katika shughuli mbali mbali za kimaendeleo.
- Kuwepo kwa uungaji mkono kwa viongozi wa kisiasa wa ngazi za Mikoa, Wilaya na shehia.

### 9.3.2.2 Mapungufu

- Jamii hainufaiki ipasavyo na matunda yanayotokana na elimu.
- Jamii haitoi kipaumbele katika uekezaji kwenye maeneo ambayo mafanikio yake hayapatikani kwa haraka.
- Matokeo mabaya ya mitihani ya skuli hurejesha nyuma uchangiaji wa jamii.
- Vipato vya wanajamii vikiwa viko chini na ushiriki wao katika uchangiaji wa elimu hua mdogo.

### 9.3.2.3 Tamko la sera

- Jukumu la jamii katika uchangiaji wa elimu litafafanuliwa.

### 9.3.2.4 Mikakati

- Kuandaa miongozo ya uchangiaji kwa jamii.
- Kuanzisha mawasilino ya karibu baina ya jamii na mamlaka za elimu.
- Kuhamasisha jamii kuunga mkono maendeleo ya elimu hususan kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
- Kuanzisha uhusiano na asasi za kiraia, viongozi wa Serikali za mitaa, Wizara na viongozi wa kisiasa.

## 9.4 MCHANGO WA WAZAZI

### 9.4.1 Utangulizi

Elimu Kwa Wote inatambua jukumu la wazazi, familia na jamii kama mwalimu wa kwanza kwa mtoto. Wazazi ni walezi wakuu wa watoto. Ustawi wa watoto na ushiriki wao katika jamii unategemea kwa kiasi gani wazazi wanashiriki katika kuhakikisha watoto wao wanapata elimu. Ingawa serikali ya Zanzibar imejidhatiti katika kutoa na kugharimia elimu, bado michango ya wazazi ina umuhimu mkubwa.

### 9.4.2 Hali ya sasa

Sera inaeleza wazi kwamba elimu inatolewa bila ya malipo, kwa vile wanafunzi hawalipii ada ya masomo. Wazazi wanaunga mkono elimu ya watoto wao katika kulipia vifaa muhimu kama vile, madaftari, kalamu, penseli, sare, usafiri, kulipia gharama ndogo ndogo kwa ajili ya ukarabati wa majengo. Wastani wa mchango wa wazazi ni asilimia 3 ya matumizi yote ya elimu katika kipindi cha mwaka 1996 hadi 1999. Katika kipindi hicho mchango wa Serikali kuu ulikuwa wastani wa asilimia 25.5 ya bajeti ya maendeleo. Mchango huu ni mara nane zaidi ya uchangiaji wa jamii lakini ni mdogo sana kulinganisha na mchango wa wahisani ambao ulikuwa wastani wa asilimia 70 ya bajeti ya maendeleo. Utayari wa wazazi katika kuchangia ni wa kupongezwa hasa ukizingatia umasikini walionao. Lakini uwezo wa kuzitatua changamoto hizi umetafautiana kutoka Wilaya moja hadi nyengine. Mnamo mwaka 2000 kiwango cha uchangiaji kilikadiriwa kuwa asilimia 27.3 kwa ngazi ya msingi, asilimia 37.3 kwa ngazi ya sekondari ya awali na asilimia 60 kwa sekondari ya juu. Hii ni sawa na wastani wa jumla wa asilimia 41.5 katika mfumo wa elimu.

### 9.4.2.1 Mafanikio

- Kuwepo kwa uelewa kwa wazazi juu ya umuhimu wa elimu kwa watoto wao na wanajua kuwa kuna uhaba wa rasilimali zinazotolewa na Serikali kuu.
- Pamoja na umasikini kwa familia nyingi, michango ya wazazi ina umuhimu mkubwa.

### 9.4.2.2 Mapungufu

- Kuwepo kwa umasikini uliokithiri unarejesha nyuma uchangiaji kwa wazazi juu ya elimu.
- Kukosekana kwa rasilimali za kutosha kutoka Serikali kuu kunamaanisha kwamba fedha zaidi zinahitajika kutafutwa kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo wazazi.

### 9.4.2.3 Tamko la sera

- Itaandaliwa miongozo sahihi ili wazazi waweze kuchangia katika elimu.

### 9.4.2.4 Mikakati

- Kuandaliwa utaratibu maalumu kwa wazazi kuweza kuchangia.
- Kuhamasisha na kushawishi uchangiaji wa wazazi.
- Kuwepo kwa uwazi wa uchangiaji kwa wazazi.
- Kuazishwe uhasibu na ukaguzi wa fedha za matumizi ya skuli.
- Kuanzisha uhusiano baina ya Wilaya na Mkoa, bodi za elimu na skuli za jirani.

"Elimu bila ya malipo inamaanisha ni kutolipia ada ya masomo. Gharama za ada ya masomo zinajumuisha vifaa na zana za kufundishia, vitabu vya maktaba, miongozo ya walimu, huduma za kompyuta, mitihani ya ndani, huduma za afya, michezo, mishahara ya walimu, gharama za uendeshaji pamoja na gharama za matengenezo".

## 9.5 MCHANGO WA SEKTA BINAFSI

### 9.5.1 Utangulizi

Elimu ni mali ya jamii ambapo kila mwanajamii ana haki ya kuipata. Kwa vile utoaji wake una gharama, inampasa kila mwanajamii kuchangia kwa njia moja au nyengine. Faida za elimu zinaigusa jamii, ambapo watu binafsi na taasisi binafsi zinachangia. Hivyo, mchango wa sekta binafsi katika elimu unathaminiwa. Vile vile sekta binafsi lazima zihamasishwe kushiriki katika utoaji wa rasilimali watu ambao hatimae watashiriki katika shughuli zao.

**9.5.2 Hali ya sasa**

Mchango wa sekta binafsi katika elimu unaongezeka siku hadi siku. Wawekezaji binafsi katika sekta ya utalii, hoteli pamoja na wafanya biashara wazalendo wamechangia kwa kiasi kikubwa katika ujenzi wa skuli na vyoo, utoaji wa huduma hususan umeme, vifaa vya michezo na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Katika skuli za jamii, watu binafsi huchangia katika malipo ya mishahara ya walimu, ada ya masomo na vifaa. Sekta binafsi pia huchangia masomo ya juu. Kwa kuongezea wawekezaji binafsi wamejenga na kusimamia uendesahji wa skui binafsi.

Kwa ujumla sekta binafsi zimetambua mchango wa elimu na zinashiriki kikamilifu katika kuunga mkono na kuchangia utoaji wa elimu.

### 9.5.2.1 Mafanikio

- Sekta binafsi zinatambua umuhimu wa elimu kwa maendeleo.
- Sekta binafsi imekuwa mdau wa karibu katika kugharimia elimu.
- Sekta binafsi imekuwa ni mshirika muhimu katika mafunzo ya walimu.

**9.5.2.2 Mapungufu**

- Kutokuwepo kwa kodi ya elimu.
- Ushirikiano mdogo baina ya sekta za binafsi na Serikali.

**9.5.2.3 Tamko la sera**

- Kutaanzishwa mfumo kwa ajili ya sekta binafsi katika kugharimia elimu.

### 9.5.2.4 Mikakati

- Kuhamasisha na kushajiisha sekta binafsi ili kuongeza ushiriki wao karika ugharimiaji wa elimu.

- Kuanzisha utaratibu wa kisheria ili kuengeza ushiriki wa sekta binafsi katika kugharimia elimu.
- Kuanzisha uhusianao baina ya taasisi zinazohusiana na masuala ya fedha na uchumi, mamlaka ya uwekezaji na vitega uchumi ya Zanzibar na mamlaka nyengine za uwekezaji.

## 9.6 FEDHA ZA NJE

### 9.6.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa mkutano wa elimu Duniani uliofanyika Dakar Senegal mwaka 2000. jumuiya za Kimataifa zimeahidi kusaidia nchi zinazoendelea katika jitihada za kuhakikisha kuwa nchi hizo zinafikia malengo ya elimu kwa wote ifikapo mwaka 2015.

Hivyo ni wajibu wa kila nchi kuweka vipaumbele na malengo yalio wazi katika sera ya elimu na kuhakikisha kuwa nchi hizo zinaimarisha utoaji wa elimu kwa mujibu wa malengo ya elimu kwa wote na malengo ya milenia (MDGs). Haja ya kuyafikia malengo haya imebainishwa pia katika ripoti ya ufuatiliaji iliyotayarishwa kwa pamoja baina ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Ulimwenguni ya mwaka (2004).

## 9.6.2 Hali ya sasa

Kwa Zanzibar, washirika wa maendeleo wana mchango mkubwa katika kugharimia shughuli za maendeleo kama vile ujenzi na usanifu wa majengo, ununuzi wa samani za skuli, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, vifaa vya maabara na huduma za usafiri. Kwa upande wa misaada ya kiufundi na kitaalamu pamoja na kujenga uwezo, wanatoa udhamini katika kada ya elimu kwa baadhi ya wafanyakazi.Vile vile washirika wa maendeleo wanawagharimia wataalamu kwa baadhi ya Idara katika Wizara,wanatoa fedha kwa ajili ya mapitio na tafiti mbalimbali, ubunifu wa miradi na kuimarisha uhusiano na taasisi nyengine nje ya Zanzibar. Mchango wa washirika wa maendeleo katika elimu ni muhimu na unaongezeka siku hadi siku Vipaumbele vilivyowekwa kwa sasa ni kwa ajili ya elimu ya lazima.

#### 9.6.2.1 Mafanikio

- Washirika wa maendeleo wameonesha utayari mkubwa katika elimu.
- Kuwepo kwa mawasiliano mazuri baina ya Wizara na washirika wa maendeleo.
- Ushirikishwaji wa washirika wa maendeleo umeleta mafanikio makubwa katika elimu.

#### 9.6.2.2 Mapungufu

- Kutokuwepo uratibu mzuri katika miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo kumepelekea mchanganyiko wa shughuli mbali mbali na udhaifu katika utekelezaji wa miradi.
- Kutokuwepo kwa mfumo wa kitaasisi katika miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo.
- Kutokuwepo kwa mipango madhubuti ya kisekta katika utekelezaji wa miradi kumepelekea utegemezi kwa baadhi ya miradi.

#### 9.6.2.3 Tamko la sera

- Mpango wa utekelezaji kisekta utakuwa ndio mtazamo wa baadae katika kugharimia elimu.

- Kwa mujibu wa mpango kazi wa utekelezaji wa Dakar na matamko mengine ya Kimataifa washirika wa maendeleo kwa kushirikiana na Serikali wataongeza ugharimiaji katika elimu ili kuhakikisha kuwa malengo makuu ya elimu yanafikiwa.

#### 9.6.2.4 Mikakati

- Kuweka kipaumbele katika programu kwenye fedha za nje.
- Kutumike mpango wa utekelezaji kisekta katika utekelezaji wa programu zinazofadhiliwa na wahisani.
- Kuanzisha mashirikiano ya kitaasisi kwa ajili ya miradi inayofadhiliwa na wahisani.
- Kuhakikisha kuwa washirika wazalendo wanakuwa mstari wa mbele.
- Kuanzisha uhusiano na Wizara inayohusika na fedha na uchumi, taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya Kimataifa na Wizara nyengine.

## 9.7 UDHAMINI KWA WANAFUNZI

### 9.7.1 Utangulizi

Familia zenye kipato cha chini zina mzigo mkubwa wa kusomesha watoto wao kwa sababu ya kukosa uwezo wa kufanya hivyo ingawaje wako tayari. Wanachangia zaidi kwa ajili ya sare, usafiri, gharama ndogo ndogo kwa ajili ya vifaa vya skuli kama ni mchango wa wazazi. Wanafunzi katika familia hizo wanahitaji kusaidiwa kifedha kwa ajili ya elimu. Misaada hiyo inaweza kutolewa kwa njia tafauti kama vile mikopo na misaada.

### 9.7.2 Hali ya sasa

Kwa sasa Serikali inalipia ada ya masomo kwa baadhi ya wanafunzi katika ngazi ya elimu baada ya elimu ya lazima na vyuo vikuu. Serikali pia inalipia gharama za mitihani ya kidatu cha "4" na kidatu cha "6" pamoja na mitihani ya kuhitimu mafunzo ya ualimu katika ngazi za cheti na stashahada. Ingawa kuna baadhi ya gharama ambazo hazilipwi na Serikali. Familia nyingi za Wazanzibari hazimudu gharama hizo. Hivyo, kuna haja kubwa ya kuwafadhili wanafunzi kwa kuanzisha mfuko wa maendeleo ya elimu kwa ajili ya ustawi wa wanafunzi.

#### 9.7.2.1 Mafanikio

- Kuna baadhi ya taasisi zisizo za Kiserikali na watu binafsi wanaotoa ufadhili kwa wanafunzi.
- Baadhi ya wafanyabiashara wa Zanzibar wamekubali kulipa baadhi ya gharama kwa ajili ya elimu ya juu.

#### 9.7.2.2 Mapungufu

- Hakujaanzishwa taasisi ambayo wanafunzi wangeweza kuomba ufadhili.
- Hakuna njia mbadala za kupata fedha kwa ajili ya ufadhili wa masomo kwa wanafunzi.

#### 9.7.2.3 Tamko la sera

- Kutaanzishwa mfuko wa fedha kisheria kwa ajili ya ustawi wa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya lazima.
- Kutaanzishwa mfuko wa fedha kisheria kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa ngazi baada ya elimu ya lazima na taasisi za elimu ya juu.
- Kutaanzishwa mashirika kwa ajili ya kutatua matatizo ya kifedha kwa wanafunzi.

#### 9.7.2.4 Mikakati

- Kuanzisha taratibu, miongozo na sheria kwa ajili ya kushughulikia masuala ya ufadhili wa wanafunzi.
- Kuanzisha na kusimamia mfuko wa fedha katika ngazi za Wilaya
- Kuanzisha ushirikiano kati ya bodi za elimu za Wilaya, kamati za skuli na jamii.

## 9.8 MATUMIZI MAZURI YA FEDHA

### 9.8.1 Utangulizi

Kiwango cha utekelezaji wa mipango ya elimu kwa kiasi kikubwa unategemea uwepo wa fedha, mkazo wa uwajibikaji katika matumizi ya fedha na matumizi sahihi ya rasilimali. Hii inajumuisha udhibiti mzuri wa rasilimali, kuchagua vipaumbele na kuweka matarajio katika matokeo.

### 9.8.2 Hali ya sasa

Kwa muda mrefu sasa, serikali imekuwa ikipata changamoto katika kufikia malengo ya bajeti za maendeleo na bajeti za kawaida. Kwa hivi sasa, serikali imeanzisha jitihada mbali mbali zenye lengo la kuimarisha uwajibikaji katika masuala ya fedha na kuongeza uwazi katika matumizi ya fedha za umma. Serikali imeazisha mpango wa matumizi wa muda wa kati (MTEF). Wizara ya elimu imeandaa mpango ZEDP ambao malengo yake yanaendana na mpango wa kupunguza umasikini Zanzibar (ZPRP) na kufanyiwa mapitio kila mwaka. Kuaandaa bajeti zenye uhalisia ni jambo la muhimu sana. Mashirika yanayotoa ufadhili wa fedha, yaweke mikakati madhubuti. Bajeti isitegemee ahadi lakini zitegemee fedha zilizopo.

#### 9.8.2.1 Mafanikio

- Kuwepo kwa kitengo cha uratibu katika Wizara ya Fedha na Uchumi.
- Kuwepo kwa Idara ya Mipango katika Wizara ya Elimu kuandaa programu, miradi na kusimamia utekelezaji wake.
- Kuanzishwa Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) na Mpango wa Mapitio ya Matumizi ya Serikali (PER) utakaowawezesha viongozi kutathmini utekelezaji wa matumizi kwa mujibu wa malengo yaliyopangwa.
- Kuwepo kwa kitengo cha ukaguzi wa hesabu za ndani.
- Kuwekwa mfumo mzuri wa utoaji wa taarifa kwa washirika wa maendeleo kumepunguza gharama.

#### 9.8.2.2 Mapungufu

- Uwezo mdogo katika kuainisha vipaumbele.
- Hakuna upatikanaji endelevu wa fedha za ndani na fedha za wahisani.
- Baadhi ya washirika wa maendeleo hawatowi takwimu zote zinazohusiana na mtiririko wa fedha (hususan taarifa za washauri elekezi).
- Fedha kutoka vianzio vyengine hazipatikani vizuri.
- Hakuna uwazi wa kutosha katika bajeti na katika matumizi ya fedha.
- Teknolojia ya Habari na Mawasiliano haijatumika kikamilifu katika mfumo wa uhasibu.
- Hakuna jitihada za pamoja baina ya washirika wa maendeleo.

#### 9.8.2.3 Tamko la sera

- Zitaanzishwa hatua madhubuti za mgawanyo wa rasilimali ili kuhakikisha kuwa dhamira kuu ya kufundisha na kujifunza inapewa kipaumbele cha kwanza.
- Mifumo ya uhasibu itatumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

#### 9.8.2.4 Mikakati

- Kukuza taaluma ya uhasibu.
- Kulazimisha matumizi ya mpango wa matumizi wa muda wa kati (MTEF) na Mpango wa Mapitio ya Matumizi ya Serikali (PER).
- Kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha katika ngazi zote (mfano: hata katika ngazi za skuli).
- Kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika udhibiti wa fedha.
- Kuanzisha ushirikiano na Wizara inayoshughulikia masuala ya fedha na uchumi, washirika wa maendeleo, taasisi zisizo za Kiserikali, mpango wa kupunguza umasikini Zanzibar, taasisi za kijamii na skuli.

# BIBLIOGRAFIA

1. **Kongamano ya Elimu ya Kimataifa (2000): "Mpango wa Utekelezji wa Dakar: Elimu Kwa Wote: Maoni ya Mikutano" Senegal.**
2. **Mapuri, O.R (1995): Mpango wa utekelezaji wa sera ya elimu, mapitio ya sera.**
3. **Mpango wa Kupunguza Umasikini wa Zanzibar (2003)**
4. **Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (2003): Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Elimu, Utamaduni na Michezo ya mwaka 2003/2004 Zanzibar.**
5. **Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dira ya 2020 ya Zanzibar.**
6. **Tamko la Umoja wa Mataifa la Millenia (2000): "Malengo ya Maendeleo ya Millenia" Marekani**
7. **Wizara ya Elimu (1991) Sera ya Elimu ya Zanzibar mapitio ya toleo la 1995.**
8. **Wizara ya Elimu, Utamaduni na Michezo (1996): Mpango Mkuu wa Utekelezaji wa Elimu Zanzibar 1996/2006, Zanzibar.**
9. **Wizara ya Elimu, Utamaduni na Michezo (1999): Tathmini ya Tamko la Elimu kwa Wote Zanzibar (2000).**
10. **Wizara ya Elimu, Utamaduni na Michezo (2003): Ripoti ya Hali ya Elimu ya Nchi ya Zanzibar.**